Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA PILI

**Kikao cha Kwanza - Tarehe 7 Februari, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na shughuli za leo napenda kutoa taarifa kwamba jumla ya maswali yote tuliyoyapata ni maswali 108, kwa kikao cha siku 9 ilistahili tuwe na maswali yasiyopungua 135. Kwa hiyo, kwa uwezo niliopewa chini ya Kanuni za Bunge nimeruhusu kwamba maswali yatakayoulizwa kwa kila kikao yatakuwa ni maswali 12 yaani pungufu ya maswali matatu, nina hakika hapo siku za usoni hali ya maswali itaongezeka.

Lakini kwa mujibu wa Kanuni ya 33(4) inakatazwa kwa Mbunge yeyote kwa Mkutano mmoja aulize maswali zaidi ya manne, hiyo ni kwa Mkutano mmoja, sasa katika hiyo jumla ya maswali 108 wapo Waheshimiwa ambao wameuliza maswali zaidi ya manne na kwa hiyo, tukiifuata Kanuni hii tutayapunguza tena maswali mengine.

Kwa hiyo, nilikuwa nataka kushauri Kanuni hii iweze kutenguliwa. Kwa hiyo, nitamwita Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu ili atoe hoja ya kutengua Kanuni halafu tutaiamua.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI):** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Kanuni ya 33(4) itenguliwe ili kuwezesha Waheshimiwa Wabunge wenye maswali zaidi ya manne waweze kuyauliza katika Mkutano huu wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA YA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Hoja ya kutengua Kanuni ya 33(4) ilikubaliwa na Bunge)*

**SPIKA:** Walioafiki wameshinda na kwa hiyo Kanuni ya 33(4) sasa imetenguliwa na tunaendelea na shughuli. Ahsante sana.

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na :-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU:**

Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na nyongeza zake zilizochapishwa tangu Kikao cha Mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaingia kwenyekipindi cha Maswali na Majibu ninalo tangazo kuhusu wageni, pale kwenye *gallery* ya Spika nyuma yenu hapo tunao wageni kutoka Bunge la Malawi, nchi rafiki ya Malawi na hawa ni Maafisa Waandamizi kutoka Ofisi ya Spika kule Malawi.

Waheshimiwa Wabunge, wageni hawa wamekuja kama jinsi tunavyosaidiana kujifunza kutoka kila mmoja kwa mwingine, maafisa hao ni Ndugu Vin Phir, Mhariri wa *Hansard* katika Bunge la Malawi, Ndugu Emans A. Mwale ambaye ni Meneja wa Utawala katika Ofisi ya Spika Malawi, Nelson Nahumwa huyu ni Afisa Mwandamizi masuala ya fedha na Ndugu Blatson Mkupatila ambaye ni Mhariri wa *Hansard,* katika Bunge la Malawi. *(Makofi)*

Tunawakaribisha sana. *(Makofi)*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 1

### Maoni ya Wananchi Juu ya Uchaguzi Mkuu wa 2005

**MHE. ALI SAID SALIM a**liuliza:-

Kwa kuwa taarifa ya utafiti imeonyesha kuwa katika uchaguzi wa tarehe 14/12/2005 asilimia 55 ya Watanzania wamesema wameridhika na taratibu za uchaguzi ulioendeshwa, asilimia 39 wamesema hawakuridhika na uchaguzi ulivyoendeshwa na asilimia 7 wamesema hawajali:-

Je, Serikali inachukuliaje maoni ya asilimia 39 ya Watanzania waliosema hawakuridhika na zoezi zima la uchaguzi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ali Said Salim, Mbunge wa Ziwani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali haijapata taarifa za tafiti rasmi zinazoweza kuthibitisha aliyoyaeleza Mheshimiwa Mbunge. Nafahamu wapo wananchi waliotoa maoni yao na kuonyesha kuridhika sana na mwenendo wote wa Uchaguzi Mkuu uliofanyika nchi nzima tarehe 14 Desemba, 2005. Lakini pia wapo wananchi walioonyesha kutoridhika ambao wametumia haki yao ya kutoa maoni na kujieleza ambayo imewekwa na Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, takwimu halisi za kitaalamu za mambo ya uchaguzi ni muhimu ili ziweze kutumika vema kutoa uamuzi na taarifa sahihi. Tafiti zinazohusiana na uchaguzi lazima zionyeshe pamoja na mambo mengine sehemu utafiti ulikofanyika kwa maana *study area* au *study location,* idadi ya walengwa, sampuli iliyotumika na mbinu zilizotumika kupata taarifa zilizothibitishwa na kukubalika. Haiwezekani mtu au kundi la watu, kwa kusikia tu kwa watu wengine au kupitia uvumi unaovumishwa kwa lengo maalum kutambuliwa na kuwa hoja ya msingi inayotokana na utafiti.

Mheshimiwa Spika, Serikali inajivunia mwenendo wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005 kwani mazingira ya mchakato mzima wa uchaguzi huo ambao hatimaye ulifanyika tarehe 14 Desemba, 2005 yalikuwa ya amani, uhuru na ya haki na kwa uhakika taratibu zote zilizowekwa na sheria za Uchaguzi zilizingatiwa. Hapakuwa na matukio yoyote ya fujo yaliyojitokeza na kuripotiwa kitu ambacho kingeashiria kwamba taratibu zilikiukwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika Uchaguzi huo watu 11,875,927 walijitokeza kupiga kura sawa na asilimia 72.41 ya waliojiandikisha. Hayo ni mafanikio makubwa. Iwapo taratibu zingekiukwa, idadi kubwa hiyo ya watu isingeweza kujitokeza na kupiga kura.

Mheshimiwa Spika, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge wa Bunge hili Tukufu kwamba taarifa mbalimbali zilizotolewa na watazamaji wa Uchaguzi wa ndani na nje ya nchi, wakiwemo *East African Community Observers Mission, SADC Parliamentary Forum* na *International Election Observer Group,* wamekiri kuwa Uchaguzi Mkuu wa Tanzania uliofanyika tarehe 14 Desemba, 2005 ulizingatia taratibu zote zilizowekwa na sheria za Uchaguzi. Napenda kuitumia fursa hii, kuipongeza Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kazi nzuri iliyofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo na mimi nampongeza sana nilitaka kuelewa tu kwa kuwa kigezo cha kukubali na kutokukubali kwenye uchaguzi ni ile siku ya upigaji kura kwenye kisanduku.

Sasa Je, Mheshimiwa Waziri ataweza kulieleza Bunge hili nini tathmini ya Serikali kutokana na uchaguzi wa mwaka 2000/2005 matokeo ni kwamba vyama vya upinzani vimezidi au vimepungua uwezo wake?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa hakika wale watu makini ambao hufuatilia mienendo ya chaguzi wataona kwamba mwaka 2000 kura za wapinzani zilikuwa nyingi kuliko za mwaka 2005, kwa hali hiyo, mwenendo mzima ni kwamba kura zao zimepungua.

Na. 2

**Mradi wa *Quick Start***

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA** aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka 2003/2004 wananchi wa Wilaya ya Karatu walichangishwa fedha na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa Mahakama ulioitwa *Quick Start* na kwa kuwa mradi huo ulikuwa unasimamiwa na Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba lakini ilipobainika kuwa fedha hizo zinatumika vibaya suala hilo lilipelekwa kwenye Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; na kwa kuwa fedha zilizochangwa ni zaidi ya shilingi milioni 13 na fedha hizo hazijulikani zilipo na vitabu vya michango zaidi ya 160 vimeripotiwa kupotea mikononi mwa Makatibu Tarafa na *WEO:*-

(a) Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu fedha hizo ambazo zimechangwa kwa lengo la kujenga Mahakama lakini hadi sasa fedha hizo hazijulikani zilipo na wala Mahakama hazijajengwa?

(b) Kwa kuwa watu waliokuwa wakikusanya fedha hizo na walipewa vitabu vilivyokuwa na zaidi ya shilingi milioni sita wanafahamika kuwa ni Watendaji wa Serikali, je, ni kitu gani kinachozuia watu hao wasichukuliwe hatua zipasazo hadi sasa? Kama hatua zimeshachukuliwa dhidi yao, ni hatua gani hizo na wahusika ni akina nani kwa majina?

(c) Je, ni nini hatma ya fedha hizo hasa baada ya mradi huo kufutwa na wafadhili?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mbunge wa Karatu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mradi wa kuzijengea uwezo Mahakama za Mwanzo za Wilaya na za Mikoa *(Quick Start Project)* ulianza kutekelezwa kwa majaribio Januari, 2003 Mkoani Arusha na Manyara kwa kuhusisha nguvu za wananchi, Serikali Kuu na msaada wa Serikali za Norway, Denmark, Sweden, Canada, Uholanzi na Finland kwenye awamu ya mwanzo ya uanzishaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Spika, kwa Wilaya ya Karatu mradi huu ulihusu ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ambao uongozi wa Wilaya ulikwishaanza kwa kuhamasisha wananchi wake kuchangia ujenzi wa Mahakama hiyo. Lengo la mradi ilikuwa ni kuchangia shilingi12,800,000/=. Fedha zilizokuwa zimechangwa na wananchi wakati mradi unaanza zilikuwa shilingi 9,242,100 na kati ya hizo shilingi 3,148,900 zilitumika kununulia matofali, mawe na mafuta ya gari. Kiasi cha shilingi 6,092,200 zilizobaki zilipelekwa kwenye akaunti ya Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Karatu kwenye Akaunti ya *Quick Start Project*. Kutokana na kutokamilika kwa ramani za majengo, ujenzi wa Mahakama za hiyo ulikuwa bado kuanza hadi mradi ulipofungwa mwezi Desemba, 2004 kwa sababu muda wa mradi ulikuwa umemalizika. Mradi huu utaendelea tena wakati wowote chini ya Mpango wa Maboresho ya Sekta ya Sheria unaolenga kuimarisha shughuli za Mahakama zote hapa nchini.

(b) Mheshimiwa Spika, idadi ya vitabu vilivyotumika kukusanya michango kutoka kwa wananchi ni 212 na vilivyorejeshwa ni 190. Vitabu 22 havikurejeshwa kutokana na baadhi wa Watendaji aidha, kuacha kazi au kutoroka kazi au kwa sababu mbalimbali kwa mfano, Watendaji wa Vijiji vya Karatu, Endabashi, Rohotia na Qungdad. Pia kuvunjwa kwa Ofisi ya Kijiji cha Karatu kulisababisha baadhi ya vitabu na mali nyingine kuibiwa. Suala hili linaendelea kushughulikiwa na polisi.

Aidha, Watendaji wa Vijiji waliotuhumiwa kwa upotevu wa vitabu na mali nyingine ni Bwana Salustinian Michael Hjando wa Kijiji cha Karatu, Bwana Shauri Qamara, Mtendaji wa Kijiji cha Endabash na Mtendaji wa Kijiji cha Qungdad

Mheshimiwa Spika, watumishi hawa walirejesha vitabu na watafikishwa Mahakamani na kuachishwa kazi.

(c) Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa mradi wa *Quick Start Project* ulifungwa rasmi kwa maelekezo ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba iliyokuwa inaratibu mpango huo na siyo wafadhili. Aidha, kama nilivyokwisha kusema, fedha zilizobakia kiasi cha shilingi 6,092,200/= zimewekwa kwenye akaunti ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Karatu zikisubiri utekelezaji chini mpango wa maboresho ya Sekta ya Sheria na uimarishaji wa Mahakama nchini.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali madogo mawili ya nyongeza na ningependa kumshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri lakini napenda niweke ifuatavyo:-

Kwanza ningependa kujua kama Waziri taarifa aliyoletewa imefanyiwa kazi kweli na Wizara au ni taarifa iliyoletwa na ofisi na kama imeletwa na ofisi Waziri anakiri kwamba amepotoshwa?

Swali la pili, Waziri amepotoshwa kwa sababu hakuna kitu kinaitwa Akaunti ya *Quick Start* kwa sababu akaunti zote za Halmashauri zinaidhinishwa na Baraza la Madiwani na hakuna akaunti yoyote iliyoidhinishwa na Baraza na wala hakuna *signatories* walioteuliwa na Baraza kwa hiyo, kwa maana hiyo Waziri atakubali sasa kufanya utafiti wa kina kuhusu suala hili ili kugundua pesa za wananchi zimekwenda wapi?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. *(Makofi)*

Pili napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dr. Willbroad Slaa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa kwamba taarifa ni sahihi na zimetoka kwenye ofisi za Serikali.*(Makofi)*

Pili, mradi ulikuwa ukiratibiwa na Wizara ya Katiba na Sheria lakini ulikuwa ukitekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Karatu. Kwa hiyo, utaona kwamba ofisi hizi mbili zilikuwa zikishirikiana kwa karibu, hata hivyo Wizara yangu pamoja na ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu tutaendelea kulifuatilia jambo hili lakini nataka kumhakikishia kazi iliyofanywa mpaka hivi sasa ni sahihi. *(Makofi)*

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, mradi huu wa *Quick Start* ulikuwa kwa ajili ya Mikoa ya Arusha na Manyara, je, Waziri anataka kutuambia kwamba mradi huo sasa umefutwa kwa Wilaya nyingine zote za Mikoa ya Arusha na Manyara? Na kama ndivyo sababu ni hizo za Karatu au kuna sababu nyingine? Ahsante.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Omar Kwaangw', kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli mradi ulikuwa ukitekelezwa katika Mikoa miwili ya Arusha na Manyara na kwamba kwa vyovyote vile ni maeneo yaliyochaguliwa siyo Wilaya zote za mikoa hiyo miwili.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo nataka kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kwamba muda wa mradi ule ulikwisha mwezi Desemba, 2005 lakini uimarishaji wa Mahakama bado uko palepale kupitia mradi wa maboresho ya Sekta ya Sheria na Katiba.

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuulizwa swali dogo la nyongeza.

Kwa vile huu mradi wa *Quick Start* umechangiwa na wananchi hususan katika Mikoa ya Arusha na Manyara katika Wilaya ya Kiteto wananchi wamekusanya mawe, wamechanga, wamefyatua matofali katika sehemu hizo ambazo zimechaguliwa ili waweze kujengewa katika huo mradi inasikitisha sana kwamba mradi umekwisha kabla haijajenga hata jengo moja.

Je, hii gharama ya wananchi Serikali itawarudishia?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Benedict Losurutia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa *Quick Start* kama ilivyo miradi yote una muda ambao ulikuwa umepangiwa na kama nilivyokuwa nimeeleza katika jibu langu la awali. Muda wake umekwisha mwezi Desemba, 2005.

Narudia tena kwamba kupitia mradi wa maboresho ya Sekta ya Sheria bado tutajenga Mahakama na kuimarisha Mahakama ndani ya Mikoa hiyo miwili iliyokuwa ya mradi pamoja Mikoa mingine ya Tanzania.

Sasa kuhusu michango ya wananchi ni dhahiri kwamba pale ambapo Mahakama hazipo zitatakiwa kujengwa na kwa hivyo Wizara yangu itaifuatilia kwa karibu sana michango hiyo ilipo kusudi kupitia huu mradi mwingine tutakapokuwa tunajenga Mahakama na kuimarisha Mahakama ili zile fedha za wananchi ziweze kutumika ipasavyo.

Na. 3

**Bandari ya Kasanga na Barabara ya Sumbawanga - Mbale**

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA** aliuliza:-

Kwa kuwa upo umuhimu wa kibiashara kati ya Tanzania na Zambia, Kongo *(DRC)* na Burundi;

Je, Serikali inaweza kutamka rasmi ni lini Bandari ya Kasanga itakamilika kujengwa na lini barabara ya lami kati ya Sumbawanga na Mbale Zambia itajengwa?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Dr. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya, Mbunge wa Kwela, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kibiashara uliopo kati ya Tanzania na nchi za jirani za Zambia, Kongo *(DRC)* na Burundi. Kwa kuzingatia

umuhimu huo, mwezi Novemba, 2004 Serikali ya Awamu ya Tatu ilianzisha Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari zote nchini *Tanzania Ports Authority (TPA)* kwa madhumuni ya kusimamia na kuziendesha Bandari za Maziwa kwa kasi kubwa zaidi. Aidha, ipo mipango na mikakati ya kutumia kikamilifu fursa ya kuwa na bandari hizi ili ichangie vema katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2005/2006, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi milioni 400 kwa ajili ya kuziendeleza Bandari za Maziwa. Kati ya hizo, Bandari za Ziwa Tanganyika ikiwemo Kasanga zimetengewa shilingi milioni 150. Kiasi hiki cha fedha zilizotengwa ni kidogo sana ikilinganishwa na hali mbaya ya miundombinu katika bandari za Maziwa. Juhudi za kutafuta fedha zaidi zinaendelea ambapo Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari katika mwaka wa fedha wa 2005/2006, imepangwa kufanya utafiti kamambe na tayari Benki ya Dunia imekubali kutoa Dola za Kimarekani 800,000 kwa kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara, Serikali inatekeleza miradi ya ujenzi wa barabara kuu za lami kwa kufuata Kanda Kuu za Usafirishaji ambayo nayo inategemea upatikanaji wa fedha. Kwa msingi huo miradi hii ya barabara kuu za lami inatekelezwa kwa awamu. Kwa upande wa Ukanda wa Usafirishaji wa Magharibi ambao unajumuisha barabara ya Sumbawanga - Kasesya - Mbala kule Zambia, Serikali imeona ianze kwanza ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara ya Tunduma kwenda Sumbawanga na hatimaye Sumbawanga - Mpanda - Kigoma kwa awamu. Pia ujenzi wa sehemu ya barabara ya Sumbawanga - Kasesya - Mbale kwa kiwango cha lami utatekelezwa kwa awamu itakayofuata kutegemea upatikanaji wa fedha. Kutokana na umuhimu wa barabara hiyo, matengenezo kwa kiwango cha changarawe yataendelea ili kuhakikisha kuwa barabara wakati wote.*(Makofi)*

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara inafahamu kwamba mwekezaji fulani alipewa fedha na Serikali milioni 180 ili atengeneze Bandari ya Kasanga na uchunguzi ambao Serikali yenyewe ilifanya waligundua kwamba fedha ile haikutumika na bandari haikutengenezwa.

Kwanza, je, Serikali inaweza kusema sasa ni hatua gani inachukuliwa kwa fedha iliyotolewa na uchunguzi ukafanyika lakini hatuna majibu mpaka sasa.

Pili, Waziri anasema kwamba zimetengwa milioni 150 mimi nataka kuuliza swali, ziko wapi hizi fedha kwa sababu bandari haijatengenezwa na inazidi kuharibika mpaka sasa?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, ningependa kujibu maswali ya Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba kuna mwekezaji ambaye alikuwa amepewa fedha ili ashughulikie bandari hiyo kama anavyosema Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya na ni kweli kwamba kutokana na hoja aliyotoa Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya hapa Bungeni, Serikali ilifanya utafiti na kugundua kwamba ilikuwepo ulazima wa kuchunguza zaidi ili kusahihisha makosa yaliyojitokeza.

Suala hili linashughulikiwa kati ya Wizara ya Fedha na Wizara ya Kilimo ambayo kwa mujibu wa utaratibu huo ndiyo walikuwa wahakikishe kwamba huyo aliyepewa hizo fedha ametekeleza wajibu uliohusika.

Mheshimiwa Spika, ninaweza kukuahidi kwamba nitalifuatilia jambo hili ili kati yetu sisi wa Miundombinu, Kilimo na Hazina tuweze kutekeleza yale ambayo yalikuwa yamependekezwa na yale ambayo hayajatekelezwa mpaka sasa. *(Makofi)*

La pili ni kuhusu hizi fedha ziko wapi, hizi fedha ziko kwenye Bajeti yangu na mwaka bado haujaisha kwa hiyo, kazi yangu ni kuhakikisha kwamba fedha zinatumika kabla ya tarehe 30 Juni. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nitawaomba radhi sijawatambua wote lakini baada ya miezi michache nitawatambua.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulizie swali moja nyongeza.

Kwa kuwa barabara iliyotajwa ya kutoka Sumbawanga kupitia Kasesia hadi kuingia Mbale, Zambia ndiyo barabara pekee ambayo inaunganisha Mkoa wa Rukwa na nchi ya nje. Barabara hii hata kwa changarawe ni mbaya mno, lakini kwa upande wa Zambia barabara zao ni nzuri mno kwa upande huo huo.

Na kwa kuwa sasa hivi magari mengi yanasafirisha mahindi, maharage na mchele kupeleka huko Zambia na wananchi wengi wanatibiwa hospitali kubwa ya pale Mbale wanaotoka upande wa Tanzania lakini wanapata tatizo kubwa la usafiri kwa vile barabara ni mbaya.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali italiangalia suala hili kuhakikisha kwamba barabara inatengenezwa angalau kwa kiwango cha changarawe haraka iwezekanavyo badala ya kutupatia maneno ya ahadi kila siku, kila siku. Je, sio aibu kwa Tanzania ambayo barabara yake ni mbaya na Zambia barabara yake ni nzuri sana?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi tatizo la utengenezaji na ukarabati wa barabara zetu ni tatizo la kifedha.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa barabara hii ambayo na sisi tunatambua umuhimu wake ya kutoka Sumbawanga/Kasesia hadi Mbale Zambia nimeeleza kwamba barabara

hii ina umuhimu na itakuwa inatengewa fedha kwa ajili ya matengenezo kwa kiwango cha changarawe kwa sasa hadi hapo uwezo wa Serikali utakapokuwa mzuri kuweza kutengeneza kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Na. 4

**Barabara ya Mbande – Kongwa – Mpwapwa**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** anauliza:-

Kwa kuwa katika Wilaya ya Mpwapwa kuna Taasisi mbalimbali kama vile Kituo cha Utafiti wa Mifugo Kanda ya Kati *(LPRI),* Kituo cha Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo *(VIC),* Chuo cha Mifugo *(LITI),* Chuo cha Ualimu Mpwapwa, Shule za Sekondari 14 ikiwemo *Mpwapwa High School* na Chuo cha Maafisa wa Afya Mpwapwa; na kwa kuwa Taasisi hizo na wananchi kwa ujumla wanahitaji mawasiliano mazuri ya barabara ya kutoka Mbande - Kongwa hadi Mpwapwa.

(a) Je, Serikali haioni kwamba upo umuhimu wa kuifanyia matengenezo makubwa barabara ya Mbande - Kongwa hadi Mpwapwa kwa kiwango cha lami?

(b) Kama mpango huo upo, je, utekelezaji wake utaanza lini ili kuboresha mawasiliano ya barabara Wilaya Mpwapwa?

(c) Je, Serikali inafahamu kwamba barabara ya Mbande, Kongwa hadi Mpwapwa inatumiwa na magari mengi yakiwemo magari makubwa ya kubeba madini ya *Gypsum* kutoka machimbo ya kijiji cha Msagali Wilayani Mpwapwa?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mbande – Kongwa – Mpwapwa inayojumuisha barabara tatu za Mkoa zinazohudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS).*

Kutokana na uwezo mdogo wa fedha kwa sasa, Serikali haina mpango wa kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Hata hivyo, katika mwaka wa fedha 2004/2005, sehemu ya barabara hiyo kutoka Mbande hadi Kongwa (kilometa 16) ilifanyiwa ukarabati *(rehabilitation)* kwa kiwango cha changarawe kwa gharama ya shilingi milioni 297.53. Aidha, katika mwaka huu wa fedha 2005/2006, sehemu ya Chunyu – Mpwapwa yenye jumla ya urefu wa kilometa 4 katika barabara ya Kongwa – Ng'ambi – Chunyu hadi Mpwapwa (kilometa 37.7) itafanyiwa matengenezo kwa

gharama ya shilingi milioni 64. Sehemu ya barabara iliyosalia itafanyiwa matengenezo ya kawaida ili iweze kupitika wakati wote.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa George Lubeleje kuwa Serikali inatambua kwamba barabara ya Mbande – Kongwa hadi Mpwapwa inatumiwa na magari mengi yakiwemo magari makubwa yanayobeba madini ya jesi *(Gypsum)* kutoka machimbo yaliyoko kijiji cha Msagali, Wilayani Mpwapwa. Kutokana na hesabu za idadi ya magari zilizofanyika katika kituo cha Mbande mwaka 2004 wastani wa magari 380 kwa siku hutumia barabara hii. Kutokana na umuhimu wa barabara hii, Serikali itaendelea kuipa kipaumbele katika kuifanyia matengenezo makubwa ya muda maalum na ya kawaida ili iweze kupitika wakati wote, kadri fedha zitakavyopatikana.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali la nyongeza.

Kwa kuwa barabara hii ya Mbande - Kongwa - Mpwapwa iliwekwa kwenye mpango wa *HIPC* kufanyiwa matengenezo makubwa. Lakini matengenezo yaliyofanyika ni kuanzia Mbande kwenda hadi Kongwa. Lakini kuanzia Kongwa hadi Mpwapwa matengenezo haya hayakufanyika.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba iko haja ya kuweka kwenye mpango wa *HIPC* ili ifanyiwe matengenezo makubwa kwa Bajeti ya 2006/2007? Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, kwanza ningependa nimpongeze sana Mheshimiwa George Lubeleje kwa jinsi ambavyo amekuwa kama kumbukumbu zinavyoonyesha akifuatilia kwa karibu sana ujenzi na ukarabati wa barabara katika Wilaya yake ya Mpwapwa. Hivi ndivyo inavyotakiwa Mbunge kuwajibika kwa wananchi na jimbo lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kama nilivyosema katika jibu langu la msingi. Wizara na Serikali kwa ujumla inatambua umuhimu wa barabara hii na ndiyo maana tumekuwa tukifanyia matengenezo. Hoja yake kwamba sasa baada ya kutengeneza ile barabara ya Mbande kwenda Kongwa basi mradi huo uendelee. Wizara imezingatia na itafanyia kazi.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Miundombinu ameeleza kwamba kipande cha barabara ya kilometa 16 ya kutoka Mbande hadi Kongwa kimekarabatiwa katika kipindi kifupi kilichopita kwa ndani ya miezi sita kwa shilingi milioni 297. Lakini barabara hiyo tayari imekwishaharibika kabisa na Mkandarasi aliyepewa kazi hiyo ni wa daraja la kwanza. Sasa swali.

Je, Wizara ina mpango gani wa kupitia tena makandarasi wake na kuangalia madaraja yao kwa sababu baadhi yao kazi yao sio nzuri?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwamba wapo Makandarasi ambao kazi zao si nzuri na Wizara yangu imedhamiria kama alivyopendekeza kupitia upya madaraja yao ili tuweze kuwaondoa wale ambao hawafai katika madaraja husika na Bodi inayohusika na kazi hii Bodi ya Usajili wa Mkandarasi imekuwa ikifanya kazi hiyo, lakini Wizara itaendelea kuwasisitiza waweze kuwachukulia hatua na kubadilisha madaraja kwa wale Makandarasi ambao kazi zao hazifai.

Na. 5

**Bei ya Pamba**

**MHE. RICHARD M. NDASSA** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi hivi sasa wanajitahidi sana kulima licha ya hali ya hewa kuwa mbaya, kwa kuwa kwa bahati mbaya sana bei ya mazao yao kwa miaka mingi imekuwa si nzuri kibiashara hasa pamba, korosho, kahawa na kadhalika; na kwa sababu Rais Mstaafu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, alishawahi kusema kuwa wanunuzi wa mazao hayo wanunue kwa bei angalau isiyopungua asilimia 60 ya bei ya Soko la Dunia na pia alipofanya ziara yake Vietnam tuliambiwa kuwa zao la Pamba litakuwa linapelekwa moja kwa moja Vietnam bila ya kupitia kwa watu wa kati *(Middleman)*.

Je, Serikali inawaeleza nini wakulima wa pamba, zao ambalo mahitaji yake ni makubwa kila siku kufuatana na ongezeko la watu duniani?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Richard Ndassa, Mbunge wa Sumve, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla bei za mazao ghafi kama vile pamba, kahawa, korosho zimekuwa zikipanda na kushuka mwaka hadi mwaka katika Soko la Dunia. Hivyo hali na mwenendo na bei imekuwa ikiathiri mapato ya wakulima. Pamoja na kuteremka kwa bei katika Soko la Dunia, Serikali imekuwa ikifanya jitihada za kuhakikisha kuwa wakulima wa pamba wamekuwa wakipata bei ya angalau asilimia 60 ya bei ya Soko la Dunia. Kwa mfano, kuanzia msimu wa mwaka 2001/2002 hadi msimu wa 2004/2005 bei ya pamba kwa mkulima imekuwa ni zaidi ya asilimia 60. Aidha, msimu wa 2005/2006 wakulima walipata bei ya wastani wa asilimia 56 ya bei ya soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kuacha utaratibu kupanga bei za mazao, utaratibu ambao ulikuwa unatumika ni ule ambao Serikali inawakutanisha wakulima na wanunuzi ili wakubaliane bei ya chini yaani bei dira ya kununulia pamba mbegu. Utaratibu huo ulionekana kuwa na matatizo hasa pale ambapo bei ya pamba nyuzi katika

Soko la Dunia inashuka chini ya bei dira ya pamba inayolipwa kwa wakulima. Utaratibu huo ulileta manung'uniko kutoka kwa wakulima ambao walilazimika kupata bei ya chini ya bei dira au wafanyabiashara ambao walikuwa wanalazimika kuwalipa wakulima bei kubwa kuliko ile ambayo wangeipata baada ya kuuza pamba nyuzi katika Soko la Dunia. Kutokana na hali hiyo, mfumo wa hivi sasa wa ununuzi wa pamba, wakulima na wanunuzi kukubalina bei wao wenyewe kulingana na uwezo wa kujadiliana wakati wa ununuzi.

Mheshimiwa Spika, biashara ya pamba nyuzi kati ya Tanzania na Vietnam imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka. Kwa mfano, msimu wa mwaka 2001/2002 Tanzania iliuza Vietnam marobota ya pamba nyuzi 1,660 yenye thamani ya Dola za Marekani 310,516 ikilinganishwa na msimu wa mwaka 2004/2005 ambapo Tanzania iliuza marobota 27,446 yenye thamani ya Dola za Marekani 5,510,939. Hata hivyo, Serikali inaendelea kuwahamasisha wamiliki wa viwanda vya kuchambua pamba kuuza pamba nyuzi Vietnam moja kwa moja bila kupitia kwa watu wa kati. Katika kufanikisha azma hii, mwezi Desemba, 2005 hadi Bodi ya Pamba iliongoza ujumbe wa wafanyabiashara weye viwanda kwenda Vietnam kwa madhumuni hayo. (*Makofi)*

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante pamoja na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

Je, bei ya pamba katika Soko la Dunia kwa msimu wa mwaka 2005/2006 ilikuwa dola ngapi? Lakini pili, kwa nini bei ya pamba mbegu kwa Tanzania inakuwa chini siku zote?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, bei ya pamba mwaka 2005/2006 ilikuwa senti za Marekani 99 kwa kilo. Kwa *exchange rate* kwa kipindi hicho yaani ya msimu uliopita inakuwa ni shilingi 1,089 pesa ya Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusu kwa nini bei ya pamba inashuka nina sababu nne. Ya kwanza ubora wa pamba tangu mwaka1994 umekuwa ukishuka, tuliongea katika soko huria la pamba. Ubora wa pamba unatokana na uchafu wakati mwingine pamba inaingia maji ama inaingia mavumbi au kutozingatia usafi wakati wa uchumaji. Lakini vile vile ruzuku inayotolewa na nchi zilizoendelea kwa mfano Australia, Amerika, Greece yaani *European Union* nayo vile vile inasaidia ama inadhoofisha bei yetu ya pamba kwa sababu wale wakulima wanavyopata *subsidy* sisi tunashindwa ku-*manage.*

Mheshimiwa Spika, lakini sababu ya tatu ni zile kodi ambazo tunawatoza wakulima wa pamba ambazo wanakatwa. Kwa mfano sasa hivi ama kipindi kilichopita wakulima wanakatwa shilingi 20 kwa kilo kwa ajili ya kuendeleza Mfuko wa Pamba. Shilingi 5/= kwa ajili ya elimu, shilingi 8/25 kwa ajili ya Halmashauri na shilingi 5/= kwa ajili ya Bodi ya Pamba. Kwa hiyo, kwa ujumla wake ni shilingi 38 kwa kilo ambapo kwa sababu pamba mbegu bei yake ingekuwa ni shilingi 220 kwa maana

wangekuwa hawakatwi wangekuwa wanapata shilingi 258 ambapo ni asilimia 65 ya bei ya pamba ya Soko la Dunia kwa sasa hivi walikuwa wanapata shilingi asilimia 56.

Mheshimiwa Spika, lakini sababu ya nne ni kutokana na kwamba viwanda vyetu vinavyochukua pamba hapa nchini sasa hivi tunachukua asilimia 80 tu ya pamba inayozalishwa. Kwa hiyo, hatuwezi kuongeza lile zao la pamba kwa maana hiyo kupeleka nje inakuwa ni gharama zaidi. *(Makofi)*

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwa vile Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kabisa kwamba mkulima wa pamba amekuwa akibebeshwa mzigo mkubwa wa kodi na makato mbali mbali; na kwa kuwa mkulima huyo huyo kwa kupitia mtindo wa *passbook* huwa anakatwa fedha kwa ajili ya pembejeo ambayo hawezi kupewa pembejeo hiyo. Je, Serikali iko tayari kukubaliana na sisi kwamba haya makato yote kwa mkulima yaondelewe?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO**: Mheshimiwa Spika, kwanza nakubali kabisa kwamba hizi *levy* zinapunguza mapato ya mkulima. Msimu uliopita ule wa mwaka 2004/2005 tulivyogundua kwamba bei ya Soko la Dunia imeshuka zile *levy* ambazo alikuwa anakatwa mkulima zilipungua. Kwa mfano, walikuwa wanakatwa shilingi 5 kwa kilo moja ikapunguzwa ikafikia *zero* yaani ilikuwa hamna hela yoyote wanayokatwa. Walikuwa wanakatwa shilingi 12/50 kwa ajili ya Halmashauri ikapunguzwa ikafikia shilingi 8/25. Kwa hiyo, nakubaliana na wewe kwa maana ya kwamba tutaendelea kuangalia ni vipi tunaweza tukapunguza baadhi ya *levy* hizi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko napenda kuongezea tu kwa swali la Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ukiangalia haya makato ambayo yalikuwa yanakatwa si kama kodi. Tanzania tumekosa kupata bei nzuri kama alivyoeleza katika suala la msingi kwa sababu tunashindwa kuuza pamba ambayo ni *premium quality* yaani ile yenye ubora wa hali ya juu. Kwa hiyo, tunapata bei ndogo.Sasa hayo ukija kuona tuna *Cotton Development Levy* ina maana ya kuendeleza uboreshaji wa pamba.

Kuna *Tanzania Cotton Board Levy* ambayo hii inasaidia kutafuta masoko mbalimbali ambayo yanawezesha huyu mkulima. Kuna mengine kama *education levy* hii ni elimu tu kutokana na maeneo yale ambayo pamba inalimwa halafu *District Council Levy* kwa sababu lazima kuna vitu ambavyo wanavihitaji kama miundombinu ya kuwasaidia saidia. Lililopo tu ni kuangalia tu kwamba hizi haziwi juu sana na pale ambapo zimekatwa inafanya kazi ilivyotarajiwa kwa sababu zina hakikisha kwamba ile pamba ambayo tunaitoa inaendelea ubora na ubora ili kumsaidia mkulima apate bei nzuri ya dunia. (*Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa zao la pamba linategemewa na watu zaidi ya milioni kumi na kwa kuwa Serikali imekubali kwamba kuna mzigo wa kodi mbalimbali pamoja na makato ya pembejeo ambayo isiyopatikana kwa wakulima, je, Serikali inafikiria vipi kutumia zana ya ruzuku kama vile inavyotumia kwa wakulima wengine kwa mfano ruzuku kwa ajili ya mbolea?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kipindi kilichopita na kipindi hiki Serikali imekubali kupeleka mifuko ya mbolea katika ngazi za mikoa na kuiuza kwa shilingi 17,000 hadi 18,500 badala ya shilingi 22,500 na bei yenyewe ilikuwa ni shilingi 22,500 lakini imekubali kuuza kwa shilingi 17,000 kwa maana ya kuwaongezea au kuwapunguzia ile 5,000/=. Kwa hiyo, pamoja na usafiri wa kule kutoka Dar es Salaam mpaka Mikoani.

Na. 6

**Ubinafsishaji wa Viwanda**

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO** aliuliza:-

Kwa kuwa karibu viwanda vyote hapa Manispaa ya Moshi, kama Kiwanda cha Magunia, Kiwanda cha Ngozi, Kiwanda cha Kutengeneza Dawa za Kuulia Wadudu wanaoharibu Kahawa pamoja na Hoteli ya Moshi vilibinafsishwa zaidi ya miaka mitano sasa na vyote vimefungwa na haviendelezwi:-

(a) Je, hatua ya Serikali kuvibinafsisha na kuvifunga sio kudhoofisha uchumi wa Moshi na ni sababu zipi zilipelekea viwanda hivyo kufungwa na Serikali itawachukulia hatua gani wale wote waliovihujumu viwanda hivyo?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani kuona viwanda hivi vinaendelezwa na vinafanya kazi?

( c) Je, kama vikifufuliwa wale wafanyakazi waliokuwa wameajiriwa watapewa kipaumbele wakati wa kuajiri?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Lengo la ubinafsishaji wa viwanda siyo kuvifunga na hivyo hudhoofisha uchumi wa Moshi. Ubinafsishaji hulenga kuvifufua viwanda, kuwa na ajira endelevu na kuongeza mapato kwa Serikali.

Kwa upande wa Kiwanda cha Ngozi, baada ya ubinafsishaji, Kiwanda kiliendelea kuzalisha ingawa kwa kiwango kidogo. Tatizo kubwa lililojitokeza ni kwa wafanyabiashara kuuza ngozi ghafi nje ya nchi na kwa nchi jirani ya Kenya ngozi ilivushwa kwa njia za panya. Hii ilivikosesha viwanda vya ngozi malighafi muhimu.

Kuanzia mwaka 2003/2004 Serikali imeamua kutoza ushuru wa asilimia 20 ya ngozi ghafi inayopelekwa nje na kutoa kivutio cha kila ngozi moja inayosindikwa. Msindikaji anaruhusiwa kuuza nje ngozi mbili ghafi. Kutokana na hatua hii, viwanda vipya vya kusindika ngozi vinaanzishwa na vya zamani ikiwa ni pamoja na cha Moshi vinafanyiwa matengenezo ili vianze uzalishaji mara moja. Juhudi za kuwekeza mtaji mpya wa shs. 620 milioni zinafanywa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Kiwanda cha Magunia, kiwanda hiki kilikuwa kimefungwa wakati wa ubinafsishaji wake. Kiwanda cha Magunia Moshi hakikufufuliwa mapema kutokana na mwekezaji *TPM (1998)* ambaye ana kiwanda pia cha Magunia Morogoro kukosa soko la kuuza magunia yatokanayo na nyuzi za katani. Hii inatokana na kuwepo mifuko ya *plastic* na *jute bags* toka Bangladesh zenye bei ya chini kuliko gharama za uzalishaji wa gunia la Mkonge. Kwa sasa *TPM (1998) Ltd.* ameanza ukarabati wa Kiwanda cha Magunia Moshi kwa kutumia mitambo ya ziada ya Kiwanda cha Magunia Morogoro na kama hatua hizi za Serikali zitafanikiwa basi kiwanda hiki pia kitaanza kazi siku za karibuni. Bado kuna mashauriano ndani ya Serikali kuhusu hatua za kuchukua kuongeza soko la *sisal bags*.

Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha Madawa ya Kuulia Wadudu kimebinafsishwa mwaka 2003 kwa *Twiga Chemicals*. Wawekezaji baada ya kukabidhiwa walikuta kuna madai mbalimbali ikiwa ni pamoja na kodi za huko nyuma. Pia mwekezaji alitaka apewe umiliki wa hisa pamoja na ardhi kwa eneo la Kiwanda. Masuala haya hayakukamilika mara moja. Kwa sasa yamekamilika. Mwekezaji ameanza ukarabati mwezi Novemba, 2005 na unatazamiwa kukamilika mwezi Machi, 2006. Baada ya hapo uzalishaji utaanza kwa majaribio na hali ikiwa nzuri uzalishaji wa kibiashara utaendelea.

Suala la kuajiri wafanyakazi wa zamani litategemea uwepo wa wafanyakazi hao, lakini kwa kuwa ajira sasa hivi ni ya ushindani Mwekezaji ataajiri kulingana na sifa za kila mmoja kwa kila nafasi. Kwa kifupi watu wataajiriwa kwa mikataba mipya.

**MHE. PHILLEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, majibu ya Waziri hayakuniridhisha. Kwa sababu hawa watu walionunua hivi viwanda walikuwa wafanyabiashara na haviendelezi. Lakini tangu wavinunue hawakuviendeleza wameviua. Pili, viwanda hivi wakati vikiuzwa vilikuwa na mashine na zana nyingi ndani ya vile viwanda. Kwa sasa hivi Serikali inajua vimetolewa vyote na haviko tena ndani ya vile viwanda?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, walichokifanya *TPM* ni kung'oa baadhi ya mashine Moshi na kupeleka Morogoro na mengine kutoka Morogoro kupeleka Moshi. Lengo lake lilikuwa ni *product diverstification* yaani kuzalisha zaidi ya *product* moja. Kwa mfano, kwa kufanya hivyo wanaweza kuzalisha *Asian Bag* kwa *Mill One* kile Kiwanda cha Moshi lakini wanaweza

pia kuzalisha mifuko ya kuchumia chai kwa *Mill Two.* Kiwanda cha Morogoro kingeweza kuzalisha *jute bags* pamoja na kuzalisha magunia ya kawaida kama ubadilishaji wa mashine utafanyika. *(Makofi)*

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ningependa kuuliza swali moja la nyongeza. Morogoro kulikuwa na viwanda vingi, ni mtandao wa viwanda kama ulivyokuwa kule Moshi. Lakini kwa bahati mbaya kuna viwanda vingi ambavyo vimebinafsishwa pale Morogoro mpaka sasa hivi havifanyi kazi na wafanyakazi waliokuwa mle ndani hawana kazi mpaka leo pamoja na kwamba walishakuwepo wengi waliotoka vijijini kufanya kazi.

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza akatueleza kwamba pamoja na viwanda vya Morogoro vimebinafsishwa na havifanyi kazi Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha kwamba vinarudi katika hali ya kufanya kazi ili vijana na wanawake wa Morogoro waweze kupata ajira na waweze kuishi vizuri?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kuna viwanda vilivyobinafishwa Morogoro hususan Viwanda vya Ngozi ambavyo havikuweza kuendeleza kama tulivyotarajia kwa sababu ya matatizo ya kisera yaliyokuwepo wakati ule. Tulikuwa hatujaweka mbinu ya kuweza kulinda hivyo viwanda kwa hiyo, ikawa ni rahisi mtu kuuza ngozi hiyo nje ama kuagiza ngozi kutoka nje akashindane na viwanda vyetu. Kwa hiyo, huyo aliyewekeza akaweza kukosa ushindani na kufanya biashara. Lakini kwa sasa hivi tumekwishaweka sheria ambayo mtu kama anauza mali ghafi ya ngozi kama alivyojibiwa katika swali la msingi itabidi atozwe kodi ya asilimia 20.

Mheshimiwa Spika, na wewe kama unazalisha hapa hutatozwa chochote utatengeneza ngozi na kuruhusiwa katika kila ngozi moja kuuza ngozi mbili nje bila kutoza hiyo kodi ya asilimia 20. Hiyo imeuhamasisha kwenye viwanda na sasa hivi wameanza kuvikarabati na hivi karibuni tutaona kwamba vitafanya kazi.

Lakini Wizara yangu vile vile bado kwa kushirikiana na Wizara ya Mipango *(PSRC)* na sekta nyingine Wizara mbalimbali kuweza kuangalia na kuchunguza vile viwanda vyote vilivyobinafsishwa kuona kama kweli vinafanya kazi kama ilivyotarajiwa. Pale ambapo tutagundua kwamba havifanyi kazi iliyotarajiwa hatua zitachukuliwa. *(Makofi)*

Na. 7

**Uanzishwaji wa Bodi na Mfuko wa Kusaidia Wanafunzi - Vyuo vya Juu**

**MHE. JOB Y. NDUGAI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeanzisha Bodi na Mfuko wa Kusaidia Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu nchini; na kwa kuwa kumekuwa na malalamiko mengi juu ya Watendaji wa Mfuko huo:-

Je, Serikali inasema nini juu ya malalamiko hayo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Kongwa, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi ilianzishwa kwa Sheria Na. 9 ya mwaka 2004 kwa lengo la kuwasaidia waombaji wenye sifa za kujiunga na Elimu ya Juu na ambao hawana uwezo kumudu gharama za elimu hiyo. Utoaji wa mikopo unachangia kupanua udahili katika Vyuo vya Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa Bodi ya Mikopo ni utekelezaji wa Sera ya Elimu ya Juu ya mwaka 1999 ambapo kila mwanafunzi wa Elimu ya juu anahitajika kuchangia gharama za elimu yake.

Kwa kutambua uwezo mdogo wa wananchi kuchangia, gharama za elimu ya juu, Serikali imeanzisha Bodi ya Mikopo kuwawezesha wanafunzi wenye sifa za kitaaluma na uwezo mdogo kiuchumi kukopa ili kugharamia elimu yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Job Ndugai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kumekuwepo na malalamiko mengi kuhusu utoaji mikopo pamoja na watendaji wa Bodi. Malalamiko hayo yanaweza kuwekwa katika makundi yafuatayo:-

(a) Viwango vya mkopo vinavyotolewa na Bodi, kwamba viwango vya mkopo vinavyotolewa na Bodi ni vidogo mno ikilinganishwa na mahitaji halisi.

(b) Ucheleweshaji katika kutoa mikopo, kwamba mikopo inachelewa sana kutolewa na kusababisha usumbufu kwa wanafunzi na hata wakati mwingine maandamano katika ofisi za Bodi.

( c) Ugumu katika kuijaza fomu za maombi, kwamba fomu hizo ni ngumu kujaza na ina vipengele vingi ambavyo ni kero kwa waombaji mkopo.

Mheshimiwa Spika, tatizo la viwango vidogo vya mikopo vinavyotolewa na Bodi ni tatizo la kibajeti.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mikopo iliotea kuwepo waombaji 33,000 wa mikopo kwa mwaka 2005/2006. Bajeti iliyoidhinishwa na Serikali ni shilingi bilioni 32.5. Ufinyu huu wa Bajeti umepelekea Bodi kuwataka waombaji wa mikopo kuchangia upungufu unaojitokeza. Aidha, kuchelewa kupatikana kwa programu ya Kompyuta yenye kuchambua maombi ya kukadiria uwezo wa mwombaji kuchangia gharama, umefanya tatizo kuwa kubwa kwani waombaji mkopo wenye uwezo tofauti wote walikopeshwa kiwango sawa kiwango sawa.

Aidha, uchangiaji huu unaendana na Sera ya Uchangiaji gharama za Elimu ya Juu kama nilivyoelezea hapo awali. Ni muhimu basi wazazi na wadau wengine wakaelewa kwamba jukumu la kugharamia Elimu ya Juu si la Bodi peke yake. Hivyo, wazazi na wadau wengine wanahitajika kuchangia gharama ambazo Bodi haikuweza kuzimudu.

Kuhusu tatizo la mikopo kuchelewa kutolewa, limetokana na kuchelewa kuwasilishwa maombi ya mkopo, uchache wa watendaji katika Bodi na ufinyu wa vitendea kazi. Matatizo haya yatakwisha mara baada ya Bodi kuajiri watendaji wa kutosha na kuweka chombo cha kuchambua maombi ya mikopo na kutambua uwezo wa kiuchumi wa kila mwombaji. Kazi hii inatarajiwa kuwa imekamilika mwishoni mwa mwezi Februari, 2006.

Mheshimiwa Spika, fomu za maombi ya mikopo ambazo zimelalamikiwa sana zinapitiwa upya kwa lengo la kuziboresha. Baada ya rasimu ya fomu kukamilika itajadiliwa na wadau husika kabla ya kuchapishwa na kusambazwa kwa waombaji mikopo. Inatarajiwa kwamba fomu kwa ajili ya waombaji wapya zitasambazwa mapema kunako mwezi Machi, 2006 ili kutoa muda wa kutosha kujazwa, kurejeshwa kuchambuliwa na hatimaye mikopo kutolewa hata kabla ya vyuo kufunguliwa.

Kwa waombaji ambao ni wanafunzi wanaoendelea na masomo watahitajika kujaza aina nyingine ya fomu ambayo ni nyepesi na wala haina mahitaji kama ya fomu ya maombi ya wale wanaoanza. Fomu hizi zitajazwa na wanafunzi ambao wanahitaji mkopo kwa kipindi cha masoma mwaka 2006/2007 na kuzirejesha kwenye Bodi kabla ya vyuo kufungwa mapema mwezi Mei, 2006.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaamini kuwa malalamiko yanayotolewa kuhusiana na utendaji wa Bodi ni matatizo ya kipindi cha mpito na ambayo yatatoweka kutokana na hatua ambazo Serikali inachukua kuimarisha utendaji wa Bodi hii. Mojawapo ya hatua ambazo Serikali na Bodi imechukua ni pamoja na kuajiri Mtendaji wake Mkuu wa Bodi, yaani Mkurugenzi ambaye nafurahi kuwafahamisha kwamba ameanza kazi jana tarehe 6 ofisini. Hatua nyingine zinazochukuliwa ni:-

(a) Kuajiri watendaji wa kutosha kuwezesha kazi za Bodi kufanyika kwa ufanisi.

(b)Kufunga chombo maalum cha kutambua uwezo wa ki-uchumi wa kila mwombaji, hatua ambayo itawezesha waombaji wasio na uwezo kutambuliwa na kusaidiwa ipasavyo hiki chomba kinaitwa *means testin*).

(c) Kuongeza vitendea kazi vya kutosha ikiwa ni pamoja na mtandao wa kompyuta wa kisasa unaompa mwombaji fursa ya kujua taarifa za maombi yake ya mkopo popote alipo kwa kutumia mtandao.

(d) Kutenga fedha za kutosha kuwezesha kukidhi sehemu kubwa ya maombi ya mkopo katika Bajeti tunaomba milioni 142.

(e) Kuanza kukusanya mikopo yote iliyotolewa kuanzia Julai, 1994 ili kuongeza uwezo wa kifedha wa Bodi; na

(f) Kuendelea kuhamasisha wananchi na wadau wengine kuchangia gharama za elimu ya watoto wao badala ya kuitegemea Bodi peke yake.

**MHE. JOB Y. NDUGAI :** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii niweze kuuliza swali la nyongeza na namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana. Serikali imekubali kwamba kwa kweli yapo matatizo mengi kwenye Bodi hii na kwa watendaji wa Mfuko huu. Lakini yapo matatizo ambayo ufumbuzi wake ni fedha, yapo matatizo ambayo ufumbuzi wake ni idadi ya watumishi kama alivyosema. Lakini yapo matatizo mengine ambayo wala si ya pande hizo mbili, kwa mfano;

Kwenye fomu za kuomba mikopo wanafunzi kwa ajili ya masoma ya elimu ya juu kuna kipengele kinamtaka mwanafunzi aonyeshe dhamana ya ardhi au nyumba au kitu cha namna hiyo, wakati mkopo ule unalenga wanafunzi ambao ni maskini wa Tanzania. Vipengele kama hivi vya kimuundo je, navyo vinasubiri nini kuondolewa haraka sana kwa utaratibu wa dharura? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili Mheshimiwa Rais amekwishaahidi kwamba kitajengwa Chuo Kikuu kikubwa kuliko vyote hapa nchini katika awamu hii ya miaka mitano, kwa hili tunampongeza sana tena. Je, Serikali itakubali kwamba Chuo hicho Kikuu kijengwe hapa Dodoma? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kuhusiana na fomu, fomu ile ina vipengele vingi vinavyohusiana na udhamini, kwanza ni mdhamini, mtu ambaye ataweka sahihi kwamba anakubaliana na yule mwombaji na iwapo kutatokea tatizo basi yeye atahusika katika kulipa ile fedha. Lakini ile fomu ina aina nyingi za vitu amabavyo vinaitwa *insurieties* ikiwemo hiyo aliyosema shamba, hati pamoja na utambulisho kutoka kwa mtu yeyote anayemfahamu yakiwemo mashirika ya dini na watu binafsi wanaomfahamu. Lengo la vitu vyote hivi ni kuhakikisha kwamba huyu mtu anafahamika, yupo na ni halisi, siyo mtu ambaye hatutaweza kumpata pamoja na *insurance policy*, kwa hiyo, vitu ni vingi.

Sasa wananchi wengi wakiwemo waombaji wali-*pick* hivi vitu ambavyo *unmovable,* nyumba na hati ndiyo wakavivalia njuga, lakini kimoja wapo katika vile vilivyotajwa vyote vile vinatumika katika kumdhamini huyu mtu. Kwa hiyo, siyo hati peke yake wala nyumba peke yake.

Mheshimiwa Spika, pia naomba niongezee kwamba umaskini wa Mtanzania sio sawasawa na umaskini wa mtu wa India. Mtanzania popote anapoishi ana ardhi, kwa hiyo, bado ile kama zingeweza kuidhinishwa wakapewa hati vijijini bado ingewezekana kutumika kama dhamana. (*Makofi*)

Swali la pili anauliza kuhusiana na Chuo Kikuu ambacho Mheshimiwa Rais ameahidi na alizungumza katika hutoba yake ya ufunguzi ambayo pia tutaijadili katika Mkutano huu. Kuanzisha Chuo iwe shule, iwe chuo hasa Chuo Kikuu inategemea vitu vingi ikiwemo *catchment area* ya mahali pale, maana yake itapata wateja watakao kuja kwa urahisi.

Hata hivyo Tanzania inafikika kwa urahisi popote ulipo, pia inategemea ardhi ya kutosha, kama alivyosema Chuo Kikuu kitakachojengwa lazima kiwe na ardhi ya kutosha sio kibanane kama Chuo Kikuu cha Muhimbili ambacho sasa hivi wanatafuta ardhi.

Hata hivyo naomba nimhakikishie Mheshimiwa Job Ndugai, kwamba Wizara yangu italifanyia kazi ombi lake kwa sababu inawezekana Dodoma ikawa na vigezo ambavyo vitavutia kujengwa Chuo hicho. (*Makofi*)

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona Mimi ndiyo Mheshimiwa Nyawazwa, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri kwa kuwa migomo katika vyuo vikuu hivi na mihura inajulika na hawa walianzisha hii sheria ya mikopo ni kwa ajili ya kuwasaidia watoto wasio kuwa na uwezo ambao wanatoka vijijini. Je, hii migomo sasa Serikali mnaona ndiyo nyezo ya hawa watu kudai haki yao katika vyuo vikuu hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi nimeeleza na kukiri matatizo ambayo yaliipata Bodi kutokana na kuanza kwake kwa haraka na pia ilitakiwa ihudumie wale vijana. Matatizo yaliyojitokeza nimesema ni ya mpito na mengi tumeshayafanyia kazi na hadi sasa hivi vijana wetu wameshakopeshwa, kiasi cha vijana 37,800 wameshapata mikopo yao, kwa hiyo matatizo haya yanaendelea kuisha hadi kipindi kinachokuja hatutakuwa na matatizo, hatutegemei tutakuwa na matatizo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Swali linalofuata, Mheshimiwa Zitto Kabwe Zuberi.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, kabla sijamwomba Mheshimiwa Waziri ajibu swali langu, naomba kufanya marekebisho kwa kuondoa kipengele (b), naomba sasa Mheshimiwa Waziri ajibu swali langu namba 8 (a) na (c). Kipengele (b) kimeshajibiwa katika swali la msingi lililopita.

Na. 8

**Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu**

**MHE. KABWE Z. ZITTO** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeshaunda Bodi ya Mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu.

(a) Je, ni kwa nini bado inahitaji wanafunzi kuandamana ili kupata mikopo yao kutoka kwenye Bodi?

(c) Je, kwa nini wanafunzi wanaoendelea *(continuing students)* walilazimishwa kukopa bila kusubiri kuanza na wanafunzi wapya?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Zitto Kabwe Zuberi, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, napenda pia kutoa maelezo yafuatayo kama nilivyofanya katika swali lililopita.Bodi ya Mikopo ilianzishwa kwa Sheria Na. 9 ya mwaka 2004 ili kuwawezesha wanafunzi wenye sifa za kitaaluma na ambao wana uwezo mdogo kiuchumi kuomba mkopo kwenye Bodi hii ili kugharamia elimu yao.

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa Bodi ya Mikopo ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Elimu ya Juu hususan uchangiaji gharama za Elimu ya Juu. Sera ya Elimu ya Juu pamoja na mambo mengine inamhitaji mwanafunzi katika Vyuo hivyo kuchangia gharama za masomo yao.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa masomo 2005/2006, Wizara yangu ilitakiwa kuanza kutekeleza Sheria Na. 9 ya 2004 ya Mikopo ya Wanafunzi kuwezesha makundi mawili ya kidato cha sita yaani *double cohort* kupata nafasi za masomo.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi ilizinduliwa rasmi tarehe 30 Machi, 2005 huku ikiwa na utata wa ama kuanza kutoa mikopo kwa mwaka wa masomo 2005/2006 au kusubiri mpaka mwaka wa masomo 2006/2007. Hii ilitokana na mahitaji makubwa ya mikopo ya wanafunzi kwa upande mmoja na rasilimali chache yaani ikiwemo fedha, watendaji na vifaa kwa upande wa Serikali. Ili kuwezesha Serikali kutumia nafasi za masomo zilizokuwa katika Vyuo Vikuu Binafsi, Serikali ilichagua kuanza kutekeleza Sheria Na. 9 ya mwaka 2004 licha ya uchache wa rasilimali zilizokuwepo.

Aidha, msimu wa udahili wa Vyuo vikuu, haukuendana vema na msimu wa kufanya maombi ya mkopo ambao ulikuwa kati ya Julai hadi Septemba, 2005. Vyuo vingi vilichelewa kutoa barua za udahili yaani *admission letters* ambazo ndiyo zingewawezesha kuomba mkopo kwa wakati. Wanafunzi wa mwaka wa kwanza walijikuta wakiomba mikopo mara baada ya kufika vyuoni.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, licha ya upungufu uliokuwepo wakati Bodi inaanza kazi, imeweza kupokea maombi 39,800 ya mikopo, kuyafanyia uchambuzi na hatimaye kutoa mikopo. Kati ya maombi hayo ni wanafunzi wachache, ambao aidha, kwa kukosa ustahimilivu au kwa kukosa taarifa sahihi za mikopo, ndio walioandamana. Hivyo, sio kweli kwamba Serikali ilihitaji wanafunzi kuandamana ndipo mikopo itolewe.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge amesema kipengele (b) kisijibiwe.

( c) Mheshimiwa Spika, wanafunzi wanaoendelea na masomo hawakulazimishwa kuchukua mkopo toka Bodi ya Mikopo. Badala yake, Serikali ilikuwa inatekeleza Sheria Na. 9 ya 2004, Kifungu cha 17(e) ambacho kinamtaja mwanafunzi anayeendelea na masomo kuwa ni miongoni mwa wale wanaoruhusiwa kuomba mikopo, *illegible* katika kuomba mikopo kwa hiyo, Serikali haikuwalazimisha kuchukua mikopo isipokuwa wenyewe waliomba.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza na swali langu lina sehemu (a) na (b):-

(a) Mheshimiwa Spika, naaamini kwamba Waziri ana taarifa kuwa mara baada ya Serikali kuruhusu mikopo kutolewa, mikopo ilitolewa kwa wanafunzi wote waliokuwa wamejiunga na vyuo bila kujali wameomba au hawakuomba. Kwa maana hiyo kuna wanafunzi ambao kimsingi wazazi wao waliokuwa na uwezo wa kuwalipia lakini wakawa wamepata udhamini wa Serikali na hii inaendana na kinyume na sera ya kuchangia gharama ambayo Mheshimiwa Waziri ameisema. Sasa je, Serikali itafanya utaratibu gani kuhakikisha kwamba fedha hizi za Serikali zinarudi Serikalini?

(b) Mheshimiwa Waziri amesema kwamba ni wanafunzi wachache tu ambao wanagoma au wanaandamana kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wanapata mikopo yao, lakini ni dhahiri kabisa kwamba mwezi Februari, 2004, wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam waligoma kupinga mfumo wa fomu za mikopo na leo hii Mheshimiwa Waziri anasema kwamba zile fomu zilikuwa zina matatizo.

Sasa je, Waziri atalihakikishia Bunge hili kwamba fomu hizo zitafanyiwa marekebisho kuzuia migomo ya namna hii kutokea? Nashukuru.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli mikopo ilitolewa kwa wote na hii ilitokana na *pressure* iliyokuwepo ya uombaji mikopo na matatizo yaliyojitokeza ya wanafunzi kutaka mikopo kwa wakati mmoja pamoja na hiyo kulikuwa na uharaka wa kuitoa hiyo mikopo, sasa ili kuondoa bugudha ilibidi Serikali itoe mikopo na kwa kweli kuna wengine walipata mara mbili. Tunachofanya ni kuangalia wale waliopata mara mbili kwa sababu *data* tunazo kwa kupitia vyuo vyenyewe. Tunawapunguza tunapowapa mikopo sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ilikuwa ni *pressure* na nafikiri wengi mlishuhudia hali ile ilivyokuwa kwa hiyo, ili kutuliza mambo na ilikuwa inakaribia wakati wa Uchaguzi Mkuu ili kuweka mambo sawa ilibidi mikopo itolewe, lakini sio kwamba

imepotea kwa sababu wale wote waliochukua ile mikopo tunawafahamu, pindi watakapomaliza itarejeshwa na hawatapewa zaidi ya pesa zile ambazo wanahitaji. *(Kicheko/Makofi)*

Swali la pili Mheshimiwa anasema Chuo Kikuu cha Dar es Salaam walipinga na hili ndilo lilikuwa moja ya tatizo walilokuwa wanapinga, unajua pale kuna makundi mawili, kuna wale wa udhamini wa Serikali na kuna wale wa udhamini binafsi.

Mheshimiwa Spika, vijana waliokuwa wanaendelea waliokuwa na udhamani wa Serikali walikuwa na matatizo kadhaa moja wapo ni kupinga ile fomu kwa sababu walidai wanawahurumia wenzao wa udhamini binafsi ambao wao walikopeshwa fedha ya ada peke yake.

Kwa hiyo, waligoma wakitaka na wenzao wakopeshwe pesa ya chakula na malazi. Lakini kiini ni kwamba hawakutaka zile fomu walitaka hali iendelee kama ilivyokuwa, kwa hiyo, hawa wachache waliogoma walikuwa na sababu zao wenyewe na hazikuwa zinaendana na hali halisi ingawa tumekili matatizo yalikuwepo na sasa hivi yanafanyiwa kazi mikopo inatolewa kama kawaida.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha, majibu ya nyongeza.

**MHE. WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu nyongeza ya swali hili la Mheshimiwa Zitto Zuberi, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, kilichotokea ni kwamba Bodi kwa kweli ilikosea, kwa sababu ilionekana kwamba ni kweli kuna wanafunzi ambao walihitaji asilimia 100, lakini kuna wengine ambao pengine wangehitaji asilimia 30 kwa sababu ya uwezo wao. Lakini Bodi ilikosea na kwamba wanafunzi wote wakapewa mkopo wa asilimia 100. Sasa ikabidi kwa kweli fedha zaidi ya zile ambazo zilizohitajika ziweze kupatikana kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, suala kwa kweli sio kwamba suala la uchaguzi lakini ni suala ambalo kwa kweli Bodi ndiyo iliyokosea. *(Makofi)*

Na. 9

**Akiba ya Chakula**

**MHE. GRACE S. KIWELU** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna dalili za uhaba wa mvua nchini, hali inayoashiria kuwepo kwa ukame na maafa kwa mifugo:-

(a) Je, Serikali imejitayarisha vipi kukabiliana na upungufu wa chakula na maafa ya mifugo nchini kote kutokana na uhaba wa mvua?

(b) Je, Serikali ina kiasi gani cha chakula katika *Strategic Food Reserve* na kitatosheleza wananchi wangapi na kwa muda gani?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge ya kwamba katika kipindi hiki cha msimu wa kilimo wa mwaka 2005/2006, nchi yetu inakabiliwa na ukame ambao una athari kubwa kwa wananchi, mifugo pamoja na uchumi kwa jumla.

Kutokana na hali hiyo, Serikali imekwishaanza kuchukua hatua za kukabiliana na tatizo la upungufu wa chakula kama ifuatavyo:-

(i) Kutokana na tathmini zilizofanywa na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Ofisi ya Waziri Mkuu na wadau wengine Agosti, Septemba na Novemba, 2005, Serikali imegharamia ununuzi na usambazaji wa tani 21,499 za mahindi kutoka Hifadhi ya Chakula ya Taifa yaani *SGR* yanayouzwa kwa bei nafuu ya shilingi 50 kwa kilo kwa watu 613,405 na idadi hii ya watu ndiyo iliyobainika kuwa na upungufu wa chakula wakati wa tathimini hiyo niliyokwisha ieleza.

(ii) Serikali imekamilisha hivi karibuni tathmini nyingine katika Wilaya 69 kubaini watu walioathirika na upungufu wa chakula kutokana na mvua kidogo za vuli na kuchelewa kunyesha kwa mvua ndefu za mwaka.Kwa kuzingatia matokeo ya tathimini hiyo Serikali itaendelea kutoa chakula cha bei nafuu kwa watu waliotambuliwa kuwa na upungufu na kutokuwa na uwezo wa kujinunulia chakula kwa bei za kawaida.

(iii) Ili kungeza upatikanaji wa chakula katika soko na kupunguza mfumuko wa bei za vyakula hasa mahindi, Serikali imetoa msamaha wa kodi ya ushuru wa forodha kwenye mahindi yanayoingizwa nchini kwa kipindi cha miezi minne yaani Januari, Februari, Machi na Aprili. Aidha, Serikali imeiagiza Mamlaka ya Bandari kutoa kipaumbele kwa shehena ya mahindi yanayoingizwa nchini na kuondoa taratibu zenye urasimu kwa ajili ya kuharakisha upakuaji na uondoaji bandarini ili kupunguza gharama kwa walaji na kuhakikisha kuwa mahindi yanafika kwenye soko haraka iwezekanavyo.

Serikali pia imewahimiza wafanyabiashara walio na akiba ya chakula katika maghala yao kuuza chakula hicho wakati huu katika soko la ndani ya nchi, ili kuongeza upatikanaji na hivyo kupunguza kupanda kwa bei ya mahindi na vyakula vingine.

(iv) Serikali imewahimiza wakulima nao kwa upande wao kutumia vizuri mvua kidogo zinazonyesha kwa kupanda mazao ya chakula yanayostahimili ukame na yanayokomaa haraka. Pia wananchi wamehimizwa kutumia kikamilifu fursa za umwagiliaji zinazopatikana katika baadhi ya maeneo yao. Aidha, wakulima ambao bado

wana akiba ya chakula kutoka msimu uliopita wameshauriwa kukitumia chakula hicho kwa uangalifu.

(b) Mheshimiwa Spika, akiba ya mahindi iliyopo katika vituo mbali mbali ya hifadhi ya chakula ya Taifa hadi tarehe 6 Februari, 2006 ni jumla ya tani 71,479.88 za mahindi. Chakula hiki kinatosheleza kulisha watu 1,581,413 wasio na uwezo wa kumudu bei ya soko ya chakula kuanzia tarehe 6 Februari hadi tarehe 15 Mei, 2006 wakati ambapo mazao yanayokomaa haraka yanapotarajiwa kuanza kupatikana.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri niliyopata kutoka kwa Naibu Waziri, naomba kumwambia kwamba kumekuwa na manung'uniko kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba tathmini au takwimu za hali ya njaa si sahihi. Je, haoni ni kipindi muafaka sasa kuwashirikisha wabunge ili waweze kutoa hali halisi ya njaa katika Majimbo yao? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE):** Mheshimiwa Spika, tathmini hizi nilizozisema zilizokwisha fanyika kwanza kimsingi zinashirikisha wananchi kule kule vijijini kwa sababu wataalamu wetu hawa wanaotoka Ofisi ya Wazara yetu na Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na wadau wengine wa mashirika ya nje wanashirikiana na viongozi wa Wilaya, pamoja na viongozi wa maeneo ya vijijini na huko Wilayani ndiko tuliko na sisi Waheshimiwa Wabunge na sisi Wabunge wote tunashiriki katika vile vikao vya Kamati ya maafa ya Wilaya na kwa namna hiyo basi katika kushiriki kwetu tunatakiwa kushiriki kwa utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, sasa suala la kusema kwamba Waheshimiwa Wabunge washiriki kama Mbunge kusema kweli pengine itakuwa sio rahisi sana. Hivi sasa tunavyozungumza ndiyo tathimini hii imekamilika ambayo ilikuwa ya nyongeza wakati Wabunge tuko hapa. Naamini kwamba katika uongozi wa pamoja wenzetu walioko huko wameshiriki kwa niaba yetu. *(Makofi)*

Na. 10

**Mradi wa Umwagiliaji Kata ya Ndungu**

**MHE. ANNE K. MALECELA** aliuliza:-

Kwa kuwa mnamo Februari, 1990 Serikali ya Japan ilitoa msaada wa Mradi wa Umwagiliaji kwa nchi ya Tanzania katika Kata ya Ndungu Jimbo la Same Mashariki ulioweza kumwagilia hekta 680 sawa na majaruba 2,230 na eneo hili liliweza kunufaisha takribani kaya 1440; na kwa kuwa baada ya kukamilisha mradi huo ilikabidhi pamoja na mradi zana muhimu za kilimo za mradi kama vile malori 13, tanki la mafuta 1, gari aina ya *Isuzu KB (pick up doube cabin)*, *4 Isuzu (Trooper), 2 (Station Wagon), Tractor 27,* Majembe ya kuvurugia udongo (kuchavanga) aina 2 tofauti 54, Majembe ya kulimia 15, vitrekta vidogo vya kufyekea mpunga 4, Majengo na ghala kubwa moja na zana

nyingine nzito mbalimbali; na kwa kuwa, mradi huo uliwanufaisha sana wananchi wa vijiji vya Ndungu, Msufini na Makokane kwa kuwapatia ongezeko la mapato kwani waliweza kuvuna mara mbili kwa mwaka na kila hekta moja walivuna kati ya tani 5.5 mpaka 6, hali hiyo ikaboresha sana maisha ya wananchi wa Kata ya Ndungu:-

(a) Je, Serikali ina habari kamili kwamba mradi huo sasa unakufa kutokana na uchakavu wa zana zote walizotuachia wafadhili wa nchi ya Japan?

(b) Kama Serikali Kuu ina habari, je, ina mpango gani wa dharura wa kuurudisha mradi huo wa umwagiliaji kwenye sura yake iliyokuwa kipindi kile cha Februari, 1990 wakati wa Japan wanatukabidhi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mradi wa Umwagiliaji Maji Mashambani katika Kata ya Ndugu ulijengwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Japan kupitia shirika lake la Ushirikiano wa Kimataifa yaani *JICA*. Ujenzi wa mradi huo ulikuwa wa awamu mbili, awamu ya kwanza ilikamilika kati ya mwaka 1988 na 1989 na ulihusisha jumla ya hekta 242, awamu ya pili ilihusisha hekta 438 ambazo zilijengwa kati ya mwaka 1989 na 1990. Jumla ikawa hekta 690 za kilimo cha umwagiliaji.Mradi huo ulipokamilika Januari, 1990 ulikabidhiwa kwa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro chini ya usimamizi wa Mkurugenzi wa Maendeleo wa Mkoa wa Kilimanjaro, *RDD* kwa wakati huo. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Same ilihusishwa kikamilifu katika Kamati ya Usimamizi wa mradi huo. Serikali Kuu, kupitia iliyokuwa Wizara ya Kilimo na Maendeleo ya Mifugo, ilitoa misaada na ushauri wa kitaalam kwa Mkurugenzi wa maendeleo wa Mkoa.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Same kwa upande wao walianzisha Chama cha Ushirika wa Wakulima wa Mpunga Yongoma *(CHAWAMPYO)* mwaka 1994, ambacho kilikuwa na majukumu ya ukusanyaji wa ada kwa ajili ya kulipa mishahara ya wafanyakazi, kukarabati matrekta, mitambo na zana mbalimbali, kusambaza mbolea, kushirikisha wataalamu katika uzalishaji, kutunga sheria ndogo ndogo yaani *by-laws* na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji katika mradi. Ilipofika mwaka 1998, Mradi huo ulikabidhiwa rasmi kwa Mkurugenzi wa Halmashauri yaWilaya ya Same ambaye hadi sasa ndiye msimamizi wa mradi huo ikiwemo mitambo, matrekta, magari, majengo pamoja na wataalam wa fani mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuonekana kwamba mradi huo ulikuwa unazorota, Serikali ilituma watalaamu mwezi Oktoba mwaka 2005 ili kutathmini hali halisi ya mradi na kutoa mapendekezo na mikakati ya kuufufua mradi huo. Baadhi ya maeneo yaliyopendekezwea kufanyiwa mabadiliko makubwa ni uongozi na usimamizi wa mradi, uendeshaji wa mradi, zana za kilimo, ukarabati wa majengo na miundombinu, ushirikishaji wa wakulima katika uendeshaji wa mradi, na ushirikishwaji wa wadau wa maji ya mto Yongoma uliopo milimani na wale wa tambarare.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetoa ushauri kwa uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Same kuuweka mradi huu katika Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya yaani *District Agricultural Development Plans (DADP's)* ili utengewe fedha. Serikali kuu itaendelea kutafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali ili kuanza kuurudisha mradi huo kwenye sura yake. Aidha, wananchi wahusika wanaweza kuuombea fedha kutoka *TASAF*.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kwamba mradi unaendelea kuwa madhubuti, Serikali itaimarisha ukaguzi, usimamizi na ushauri katika *CHAWAMPYO* kwa lengo la kuhakikisha kwamba fedha zinazochangwa na wakulima kwa ajili ya uendeshaji na utunzaji wa mradi wao yaani *operation and maintenance* zinaelekezwa kwenye matumizi yaliyotarajiwa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa muda wa maswali uliingiliwa na matangazo tangazo hivi; ninazo dakika tatu za kuongeza. Kwa hiyo, namruhusu Mheshimiwa Anne Kilango Malecela swali la nyongeza.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Rais wa Awamu ya Nne alipofika Jimboni kwangu tarehe 30 Septemba aliliona hili tatizo kubwa la ule mradi na akaahidi wananchi kwamba atajitahidi kurekebisha mradi ule na kwa kuwa mimi mwenyewe nimejihakikishia kwamba Mkoa au Wilaya kwa wakati huu havina uwezo wa kusimamia mradi ule na wala kukarabati. Je, Serikali Kuu kwa kutambua umuhimu wa miradi ya umwagiliaji na umuhimu wa fedha za wafadhili, haioni kwamba kuna umuhimu mkubwa wa Waziri mwenyewe achukue nafasi ya kwenda kuona mradi huu ili aweze kuamini kuliko kutegemea tu taarifa za kupewa na wataalam?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, wakati Wajapani wanaondoka waliacha zana nyingi sana katika mradi huu, lakini Serikali Kuu ilipoona kwamba kuna zana nyingine zinahitaji matengenezo, iliamua kuziuza na sasa hivi zana nyingi katika mradi ule zimeuzwa. Je, Serikali haikuona kwamba ilikuwa ni muhimu zana zile kuwauzia wadau wenyewe yaani wananchi ambao wanahusika na mradi ule kuliko ambavyo asilimia 95 ya zana zile wameuziwa watu wa nje kabisa na kwa bei nafuu?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge ametamka Waziri mwenyewe, nimeona afadhali nijibu mwenyewe kwamba, je, ninauona umuhimu wa kutembelea mradi huo ili niione hali halisi?

Napenda nimhakikishie kwamba, kwa kuwa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi imeweka umuhimu mkubwa sana katika Ibara ya 31(f) wa suala la kupanua umwagiliaji, natarajia mimi mwenyewe kutembelea maeneo yote yaliyoonyeshwa katika *Irrigation Master Plan* ambayo nimekuta Waziri mwenzangu aliyenitangulia alisimamia

ikaandaliwa, ziko hekta milioni 2.3 zilizo katika *priority* ya kwanza*(high potential)* ikiwemo eneo analotoka Mheshimiwa Mbunge. Kwa hiyo, ninamhakikishia kabisa kwamba maeneo yote hayo nitayatembelea mimi mwenyewe katika Kanda zote nane katika kipindi hiki kinachokuja mapema iwezekanavyo.

Kuhusu swali la pili kwamba zana nyingi zimeuzwa kwa watu walio nje ya mradi, hili ni jambo ambalo kama Mheshimiwa Mbunge anavyosema limekwishatendeka. Mimi naona tutizame mbele, tuangalie namna mradi ule tunavyoweza kuuendesha vizuri na zana zilizopungua tuweze kuzipata mapema iwezekanavyo. Tutajitahidi kwamba kosa au kasoro iliyotokea huko nyuma tutajitahidi isiwepo tena kwa kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge. Ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali sasa umekwisha. Ninayo matangazo kabla hatujaingia katika Hoja za Serikali.

Kwanza kabisa, ningesema tu hivi, ukaaji katika Bunge una utaratibu wake. Kwa sasa hivi Waheshimiwa Wabunge kadhaa wamekuwa wakikaa popote wanapopenda kwa siku yoyote wanavyoona. Matokeo, imekuwa ni vigumu sana kwa Spika kuwatambua, lakini pia kwa wasaidizi wetu kuweza kumfikishia Mheshimiwa Mbunge ujumbe wake na bahasha mbalimbali muhimu pale alipo. Kwa hiyo, nawaomba sana kuanzia kesho asubuhi kwa sababu mchana wengi nadhani huwa wanapenda penda kupumzika ili wasipumzike humu. Kwa hiyo, huwa tunakuwa wote asubuhi, ningeomba kesho asubuhi Waheshimiwa Wabunge muwe mmeamua wapi mtaketi, ili kuanzia kesho muweze kutumia nafasi hizo kikamilifu. *(Kicheko)*

**WABUNGE FULANI:** Tayari

**SPIKA:** Aah! Ndivyo tayari hivyo?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo!

**SPIKA:** Basi sasa mjue basi. Nilikuwa nadhani ni Waheshimiwa Mawaziri tu ndiyo wamejipanga vizuri maanake... kumbe sasa ni wote. Tulivyoanza hivi sasa basi kesho tuendelee na huo ndio utaratibu na mtaona shughuli zinakwenda vizuri. *(Kicheko/Makofi)*

Ninao wachangiaji watatu kwa lile Azimio ambalo litafuata, halafu na wachangiaji 83 kwa ile hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu Hotuba ya Rais. Kwa hiyo, sasa nitamwita Katibu tuendele na utaratibu.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, kama mwenyewe jinsi unavyotambua kwa upande wa Kambi ya Upinzani...

**SPIKA:** Unasemea Kanuni ipi sasa?

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, ...

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni zetu, suala lolote linalodai mwongozo wa Spika ili Spika aweze kufanya rejea mara moja na pia suala lolote linalohusu Kanuni, ni lazima itajwe kama kwa mfano kuhusu utaratibu na hoja zote za kusimama hizi ambazo Spika anazitambua, ni muhimu, siyo muhimu tu, inatakiwa kwa mujibu wa Kanuni kutaja Kanuni yenyewe ili mwongozo nao utolewe kwa mujibu wa Kanuni. Kwa hiyo Mheshimiwa Zitto, tunaendelea bila shaka mambo haya yatazidi kueleweka. Kwa hiyo, tuendelee Katibu.

## HOJA ZA SERIKALI

## AZIMIO

### Azimio la Kuridhia Itifaki ya Kuanzishwa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu *(Protocol to the African Charter On Human and People's Rights on The Establishment of an African Court On Human and People's Rights)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA (MHE. DR. CYRIL A. CHAMI ):** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Maazimio ya Kuridhia Mkataba wa Nyongeza wa Kuanzisha Mahakama ya Afrika ya Haki za Binaadam na Watu na Itifaki ya Kuanzisha Mahakama ya Umoja wa Afrika.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuzishukuru kwa dhati kabisa Kamati za Kudumu za Bunge lako Tukufu, Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Kamati hizi mbili zilipitia na kutoa ushauri makini kuhusiana na Mikataba hii miwili. Mchango wao umesaidia sana kuboresha Maazimio haya ninayowasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu leo.

Mheshimiwa Spika, kama Bunge lako Tukufu linavyofahamu, nchi yetu ni mwanachama wa Umoja wa Afrika, Umoja ambao umechukua nafasi ya Umoja wa Nchi Huru za Afrika tangu mwaka 2002.

Kwa mujibu wa Mkataba wa kuanzisha Umoja wa Afrika *(The Constitutive Act of the African Union).* Umoja huu ulirithi Mikataba iliyopitishwa na Umoja wa Nchi Huru za Afrika inayohusu Haki za Binadamu na Watu. Moja ya Mikataba hiyo ni ule unaojulikana kama Mkataba wa Nyongeza wa Haki za Binadamu na Watu *(The Protocol to the African Charter on Human and People's Rights on The Establishment of an African Court on Human and People's Rights)* ambao ulisainiwa Mjini Ouagaudougou, Bukinafaso mwezi Juni, 1998 na mwingine ni wa Mahakama ya Umoja wa Afrika *(The Protocol of the court of Justice of the African Union)* uliosainiwa Maputo, Msumbiji Julai, 2003.

Mheshimiwa Spika, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alisaini Mikataba hiyo mara tu baada ya kupitishwa na hivyo kuonyesha nia na dhamira ya nchi yetu kuridhia Mikataba hiyo.

Kwa mujibu wa Ibara ya 63, (3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977, Bunge lako ndilo lenye Mamlaka ya Kujadili na Kuridhia Mikataba inayohusu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa. Mikataba hii miwili inahitaji nchi ziiridhie baada ya kusaini. Serikali inaileta Mikataba hii katika Kikao hiki cha Bunge ili ijadiliwe na kuridhiwa.

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa Mahakama hii kutasaidia katika utekelezaji kwa vitendo wa mikataba yote ya Umoja wa Afrika. Tanzania kama Muasisi wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika, inakubaliana na Sera ya Afrika ya Kutatua matatizo ya Bara hili kwa kutumia Vyombo vya Afrika kama hii Mahakama. Jambo hili ni muhimu sana kwetu na linapaswa kuungwa mkono kwa dhati kwa kuridhia Mikataba hii miwili.

Mheshimiwa Spika, kama Bunge lako litakubali kuiridhia Mikataba hii, Tanzania itapata fursa ya kupewa nafasi ya kuwa Makao Makuu ya Mahakama itakayounganisha vyombo hivi viwili. Iwapo Tanzania itafanikiwa kupata nafasi hiyo ya kuwa mwenyeji wa Mahakama hiyo, gharama za kuiendeshea Mahakama zitatolewa na Umoja wa Afrika kutokana na michango ya wanachama wake. Jambo hilo kama Waheshimiwa Wabunge wanavyofahamu litaiongezea nchi yetu kipato kitakachotokana na pango la majengo yatakayotolewa kwa ajili ya Mahakama.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakusudia kutoa majengo yanayotumiwa na Mahakama ya Kimataifa ya Makosa ya Jinai ya Rwanda yatumiwe na Mahakama ya Umoja wa Afrika baada ya muda wa Mahakama hiyo ya Rwanda kumalizika mwaka 2008. Katika kipindi cha mpito, Mahakama itatumia majengo mengine ya kituo cha mikutano ya Kimataifa cha Arusha *(Arusha International Conference Centre).*

Mheshimiwa Spika, katika kikao cha Wakuu wa Nchi wanachama wa Umoja wa Afrika kilichofanyika Khatoum, Sudan tarehe 23-24 Januari 2006, Tanzania ilipewa heshima kubwa ya kuchaguliwa kuwa Makao Makuu ya Mahakama ya Afrika ambayo itaunganisha Mahakama ya Haki za Binadamu na Watu na Mahakama ya Umoja wa Afrika. Ili nchi iweze kuwa mwenyeji wa Taasisi muhimu kama hii, ni lazima iwe imeridhia Mkataba unaoianzisha. Serikali inapendekeza Bunge lako Tukufu liiridhie Mikataba hii kwa heshima na maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba Bunge lako Tukufu liyajadili Maazimio haya mawili kwa pamoja na hatimaye kukubali kuiridhia Mikataba inayohusika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.*(Makofi)*

**SPIKA:** Hoja hiyo imetolewa, sasa naomba iende kwenye *floor* na michango itolewe. Maazimo hayajasomwa? Ikamilishe kwa Maazimio. Mheshimiwa Waziri, Maazimio!

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iliridhiwe)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA (MHE. DR. CYRIL A. CHAMI ):** Mheshimiwa Spika, Azimio la Kuridhia Itifaki ya kuanzishwa Mahakama ya Umoja wa Afrika *(Protocol of the Court of Justice of the African Union),* kwa kuwa Tanzania imesaini Itifaki ya Kuanzishwa Mahakama ya Umoja wa Afrika, na kwa kuwa Itifaki hii imetokana na Mkataba wa Afrika wa kuanzisha Mahakama ya Umoja wa Afrika ambao unahitaji nchi wanachama kuridhia ili iweze kufanya kazi na kwa kuwa kwa kuridhia Itifaki hii Tanzania itakuwa inatekeleza wajibu wake katika makubaliano ya Kimataifa na kwa kuwa Umoja wa Nchi za Afrika ambao Tanzania ni mwanachama imekubali kuridhia kuanzishwa Mahakama ya Umoja wa Afrika na kwa kuwa kwa kukubali kuridhiwa Itifaki hii ya kuanzishwa Mahakama ya Umoja wa Afrika, Tanzania itanufaika na haya yafuatayo, yaani itapata fursa ya kuwa Makao Makuu ya Mahakama hiyo.

Pili, itapata heshima zaidi usoni mwa Mataifa mengine kwa kukubali chombo hicho kianzishwe ndani ya nchi. Tatu, utekelezaji wa Mikataba na Itifaki nyingine inayohitaji maamuzi ya Mahakama hiyo utafanyika. Nne, wananchi na Watumishi wa Mahakama hiyo watapata kipato kutokana na watu watakao kuwa wanatumia Mahakama hiyo na Taasisi zitakazokuwa zinafuatilia haki katika Mahakama hiyo. Kwa hiyo, basi kwa kuzingatia umuhimu wa kuridhia Itifaki hii ya Kimataifa na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Bunge hili katika Mkutano wake huu wa pili sasa linaazimia kuridhia Itifaki ya Kuanzishwa kwa Mahakama ya Umoja wa Afrika *(Protocol of the Court of Justice of the African Union).*

**Azimio la Kuridhia Mkataba wa Nyongeza wa Kuanzishwa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu *(Protocol to the African charter on Human and People's rights on the Establishment of an African Court on Human and People's Rights).***

KWA KUWA Tanzania imesaini mkataba wa nyongeza wa kuanzishwa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadam na Watu mnamo mwaka 1998;

NA KWA KUWA Mkataba huu wa nyongeza umetokana na Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu ambao nchi yetu imeridhia na ambao unazitaka nchi za Afrika kukuza ustawi na kulinda haki za binadamu;

NA KWA KUWA suala la kukuza na kulinda haki za binadamu kwa raia ni jambo lililo kwenye Katiba ya nchi;

NA KWA KUWA Umoja wa nchi za Afrika ambao Tanzania ni mwanachama umeamua kuanzishwa Mahakama ya Haki za Binadamu na Watu kwa ajili ya kuiongezea

nguvu Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu katika kushughulikia migogoro inayohusu Haki za Binadamu;

NA KWA KUWA Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekubali Mkataba huo uridhiwe;

NA KWA KUWA Tanzania itafaidika kwa kitakachopatikana kutokana na moja, mapato ya pango la majengo, mbili, ajira ya Watanzania katika Mahakama hiyo, na tatu mapato yanayotokana na huduma mbali mbali zinazotolewa na watumiaji wa Mahakama hiyo;

KWA HIYO BASI, kwa kuzingatia umuhimu wa Kuridhia Mkataba huo wa nyongeza ya Kimataifa na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Bunge hili katika Mkutano wake wa pili sasa linaazimia Kuridhia Mkataba wa Nyongeza ya kuanzishwa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu *(Protocol to the African Charter on Human and People's Rights)*.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunayo maazimio mawili mbele yetu, mbele ya Bunge kwa Hoja hii ya Serikali. Kwa utaratibu, nitamuita kwanza Mwenyekiti wa Kamati ili aweze kutoa maoni ya Kamati kuhusu Azimio hili. Baadaye nitamuita Msemaji wa Upinzani ili naye aweze kutoa maoni na hatima yake na wachangiaji watatu waliokwishaleta majina yao na baada ya hapo basi ndio nitawahoji. Sasa ninamuita Mwenyekiti wa Kamati. *(Makofi)*

**MHE. ANNA M. ABDALLAH - MWENYEKITI KAMATI YA MAMBO YA NJE:** Maoni ya Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nchi za Nje kuhusu Azimio la Kuridhia Itifaki ya kuanzishwa kwa Mahakama ya Umoja wa Afrika na Azimio la Kuridhia Mkataba wa Nyongeza wa Kuanzishwa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijawasilisha maoni ya Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje juu ya Azimio la Kuridhia Itifaki ya Kuanzisha Mahakama ya Umoja wa Afrika na Azimio la Kuridhia Mkataba wa Nyongeza wa Kuanzisha Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri wa Tanzania na Mheshimiwa DR. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kwa kuchaguliwa kwao kwa ushindi wa kishindo kuongoza nchi yetu katika Awamu ya Nne ya uongozi wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuchukua nafasi hii kukupongeza wewe kwa kuchaguliwa kwako kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mheshimiwa Anne Makinda, kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia Mawaziri wote kwa kuteuliwa kushika nyadhifa walizonazo. Vile, vile nawapongeza Wabunge wenzangu wote kwa kuchaguliwa au kuteuliwa kuwa Wabunge wa Bunge hili kwa kipindi cha mwaka 2005 hadi 2010.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nchi za Nje kwa kunichagua mimi kuwa Mwenyekiti wa Kamati hii na naomba niwatambue kama ifuatavyo, Mheshimiwa Mussa Zungu, Makamu Mwenyekiti na wajumbe ambao ni Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Ame Pandu Ame, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, Mheshimiwa Mohammed Gulam Dewji, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Balozi Hamis Kagasheki, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Yono Kevela, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed, Mheshimiwa Balozi Abdul Mshangama, Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa John Shibuda, Mheshimiwa Zaynab Vulu na Mheshimiwa Dr. James Wanyancha.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, kwa mujibu wa Kanuni ya 70(2) ya Kanuni za Bunge Toleo la mwaka 2004, naomba sasa kuwasilisha maoni ya Kamati baada hoja hii kupitiwa na Kamati yangu katika kikao cha pamoja na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Huu ni utaratibu ambao Kamati yangu imejiwekea wa kuhusisha Kamati zinazohusika na Mikataba ambayo inagusa majukumu ya Wizara zilizomo katika dhamana ya Kamati husika. Hapa napenda nieleze kuwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inahusika na Maazimo haya kutokana na jukumu lake la kushughulikia masuala ya Katiba na Sheria ikiwa ni pamoja na Haki za Binadamu.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla baada ya kuyapitia Maazimio haya, Kamati zote mbili zimeyakubali kwa kauli moja na hivyo tunashauri Bunge lako Tukufu likubali kuridhia Maazimio haya hasa kutokana na kazi nzuri iliyofanywa na Serikali kushiriki katika hatua zote za mikataba hii na pia kwa kuzingatia maslahi ya Taifa kama alivyoeleza mtoa hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa pongezi kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudi kubwa alizozifanya kuwashawishi wakuu wa nchi za Afrika mpaka wakakubali Makao Makuu ya Mahakama ya Umoja wa Afrika kuwa katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais hakuomba Makao Makuu ya Mahakama hiyo iwe nchini mwetu kwa kubahatisha, bali ulikuwa ni uamuzi sahihi kabisa kutokana na ukweli kuwa nchi yetu ni kisiwa cha amani na utulivu na ni kielelezo cha utawala bora katika Bara hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa Mahakama ya Umoja wa Afrika kuwepo nchini mwetu, Tanzania itanufaika katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, kupata heshima machoni mwa Mataifa mengine na kielelezo cha dhati kuwa Serikali yetu inathamini haki za binadamu.

Pili, kupatikana kwa ajira kwa Watanzania katika Mahakama hiyo na hasa tukizingatia kuwa moja kati ya mikakati ya Serikali ya Awamu ya Nne ni kuongeza ajira kwa Watanzania na tatu, kupata mapato yatakayotokana na huduma mbali mbali zitakazotolewa kwa watumiaji wa Mahakama hiyo kama vile chakula, malazi, usafiri na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mwisho namalizia kwa kumshukuru Mheshimiwa Dr. Cyril Chami Mbunge wa Moshi Vijijini na Naibu Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa kutoa maelezo fasaha mbele ya Kamati. Pia, nawashukuru Mawaziri wafuatao, Mheshimiwa Philip Marmo,Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Utawala Bora, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu,Waziri wa Katiba na Sheria na Mheshimiwa Hawa Ghasia, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa kuiwakilisha vyema Serikali mbele ya Kamati. Hii imeipa uzito hoja iliyotolewa kwenye Kamati na kuonyesha kuwa Serikali ni moja.

Aidha, nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kuyapitia maazimio haya kwa umakini mkubwa na kutoa michango ya mawazo iliyoiwezesha Kamati yangu kutoa ushauri kwa Bunge kuyaridhia maazimo haya kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, Msemaji wa Kambi ya Upinzani!

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NJE:** Mheshimiwa Spika, na mie napenda nitumie fursa hii kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kutoa maoni kuhusu Kuridhia Itifaki hizo mbili zilizotajwa kwa mujibu wa Kanuni ya Bunge Kifungu cha 43(5)(b) na (c) na 81(1) Toleo la mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, nami nitumie fursa hii kukupongeza wewe pamoja na viongozi wenzako mliochaguliwa kutuongozea Bunge letu na niwapongeze wale wote walioshinda kihalali katika chaguzi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, heshima tuliyopewa na wenzetu, wametupa kwa sababu wanatuamini na sisi Kambi ya Upinzani tumeliona hilo na hatuoni sababu ya kutumia muda mwingi wa Bunge lako katika kusema maneno ambayo mwisho wake ni kukubali na kuridhia jambo ambalo tumepewa kwa heshima kubwa. *(Makofi)*

kimsingi tunapewa Mahakama na Mahakama vyovyote itakavyokuwa hapo baadaye itahukumu mambo ambayo pengine hata sisi wenyewe kama tukikosea mahesabu tunaweza tukaingia katika kuhukumiwa.

Mheshimiwa Spika, sisi Kambi ya Upinzani tunaomba sana kuwa Wabunge waridhie kuridhiwa kwa Itifaki hii, lakini pia tunaomba viongozi wa nchi yetu wajaribu kusimamia kwa karibu masuala ya haki za binadamu na utawala bora ili na sisi tusije tukaingia katika mtego wa kuhukumiwa katika nchi yetu wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na wataalam wake kwa kufanya *lobbing* kubwa ya kukubaliwa nchi yetu na kupewa hadhi hii hasa baada ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano kuchukua maamuzi ya kukubali na kusaini Mkataba huu. Kwa kweli kazi hii waliyoifanya, kwetu sisi ni heshima kwa sababu baada ya Rais kusaini au kutia sahihi, kama tusingepata hii fursa basi ingekuwa ni jambo la kusikitisha sana. Lakini hili waliliona wenzetu waliokuwa pale wataalam wa Mambo ya Nje pamoja na Waziri.

Mimi nashukuru sana kuwa Rais ameliona jambo la heri, Waziri ameliona jambo la heri na nawaomba Waheshimiwa Wabunge tuone hii heri, tusipoteze wakati katika kujadili jambo ambalo lina maslahi kwetu. Naomba tukubali, turidhie ili tuweze kuunga mkono heshima tuliyopewa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia kidogo kuhusu Hoja hizi za Serikali, Maazimio haya mawili lakini hasa kwenye Azimio la Kuridhia Itifaki ya Kuanzishwa kwa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu.

Kwanza napenda awali kabisa niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Bumbuli kwa kumpigia Rais wetu Jakaya Kikwete kura nyingi sana, asilimia 91 dhidi ya wagombea wengine wa Urais. *(Makofi)*

Vile vile, nawashukuru kwa kunipigia kura nyingi, asilimia 83 dhidi ya wagombea wa CHADEMA, *CUF* na *NCCR-MAGEUZI.* Nawashukuru sana.Wananchi wa Jimbo la Bumbuli wanajua tulipotoka, tulipo na tunapoelekea. Kwa hiyo, msimamo ni ule ule. Sasa hivi napenda kuwasisitiza kwamba tujitahidi tukamilishe madarasa tunayojenga ili wanafunzi wote waliochaguliwa waweze kuingia kidato cha kwanza. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza sana Serikali kwa kuchangamkia mambo makubwa haya ambayo yanahusu Afrika. Tumepata heshima kubwa sana ya kupewa nafasi ya kuwa na Makao Makuu ya Mahakama hii ya Haki za Binadamu na ni heshima kubwa sana. Haki za binadamu haziwezi kwenda mahali pengine isipokuwa mahali kama Tanzania ambako kuna utulivu, kuna amani na utawala wa sheria. Tunaipongeza sana Serikali kwa jinsi ilivyotuonyesha huko mbele wanakokwenda. Kwa hiyo, juhudi hizi kwa kweli ziendelee na tunamtakia kila la kheri Rais wetu, Jakaya Kikwete na timu yake ikiongozwa na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mambo napenda kuyasisitiza tu kwamba kuwepo kwa mahakama hii kuna faida kubwa. Ukiacha faida za kisiasa, lakini kuna faida za kiuchumi vile vile kwa sababu kuna michango ambayo itatolewa na wanachama. Kuna *Article 32* inaonyesha kwamba kuna michango itatolewa na wanachama na michango hiyo itakuja kwenye nchi yetu, kwa hiyo, kuna mapato pale. Isipokuwa la kusisitiza ni kwamba nchi yetu iwe ya kwanza kutoa mchango wake ili iwe rahisi kuwahimiza wengine waweze kutoa michango yao.

Mheshimiwa Spika, pia jambo hili lina faida kwetu kwa sababu katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi kuna dhamira ya kuongeza ajira. Sasa hapo tayari tumepata ajira, ni vizuri tukachangamkia ajira hizo kwani kuna ushindani. Kwa hiyo, wataalam walioko wachukue nafasi hiyo ili ajira hizi zisije zikachukuliwa na watu wengine, nafasi kubwa tuipate sisi.

Vile vile, ningependa kuishauri Serikali kwamba wakati watakapokutana tena ni vizuri waangalie ile *Article 35* ya *amendments* kwa sababu humu ndani maandishi mengi ni ya *OAU.* Ni vizuri sisi kama wenyeji tuyapeleke hayo yafanyiwe *amendment* ili itifaki hii iweze kwenda na wakati.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na naunga mkono Maazimio yote na kuipongeza Serikali kwamba kasi hii ndiyo kasi ambayo tunaitaka. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie Maazimio yaliyoko mbele yetu. Kwanza niseme tu kwamba ninaunga mkono Maazimio yote mawili yaliyoko hapa mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninasimama kwa sababu napenda kusisitiza mambo yafuatayo:-

La kwanza, kama tunavyoona kwenye Azimio la Kuunda Mahakama ni suala la ushindani kimsingi. Kwa kuwa ni suala la ushindani, nadhani inatakiwa uharaka wa ajabu katika kuyapitisha ili Majaji wetu waweze kuingia na tuwaingize wale wenye sifa zinazotakiwa. Najua Majaji wenye sifa Tanzania tunao, kwa sababu kama utaratibu unavyotaka, sifa zinazotakiwa ni *integrity* ambapo Majaji wengi wenye *integrity* tunao na hatuna sababu ya Majaji wetu kutokuingia katika nafasi kubwa kama hii. Kwa hiyo, nataka kusema tu kwamba, suala la ushindani halitaki kusubiri na kweli tumesubiri vya kutosha, ni lazima tuingie haraka kadri inavyowezekana katika hili.

La pili, nataka kueleza kuhusu suala la haki za binadamu. Kama tulivyosema kwanza, Mheshimiwa Rais katika hotuba yake Bungeni amekazia suala hili. Mimi nimeyaona malengo ambayo Waziri ametuletea hapa mbele yetu, ya mapato, ya makao kuwa kwetu, nadhani jambo kubwa zaidi ni kwamba nchi yetu itakuwa kioo cha utekelezaji wa haki za binadamu mahakama inapokuwa hapa kwetu, kwa sababu hatuwezi kuwa tuna-*host* mahakama katika nchi yetu halafu na sisi tusiwe kioo. Kama

ilivyo na kama tutakavyoizungumza kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais nadhani *good governance* tunayoisema basi kioo chake cha msingi ni katika Makao Makuu ya jambo hili kubwa kwa Bara zima la Afrika yatakapokuwa hapa kwetu.

Kwa hiyo, nilitaka kusisitiza kwamba hili si suala la kujadiliana, ni suala la Kitaifa, ni suala la maslahi ya Taifa, lakini ni *image* ya nchi yetu katika Afrika nzima na katika dunia nzima, kwa hiyo, hatuna sababu yoyote ya kubishana nalo, ni lazima tulikubali. Lakini tukishakubali, basi ni lazima sisi pia tu-*domesticate* haya yote yanayosemwa humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ingekuwa kuna uwezekano wa kukazia zaidi ninaona pia kwamba sasa hata *individuals* wanaruhusiwa kwenda kwenye mahakama hii. Kwa hiyo, ningependa suala la elimu litolewe kwa watu wetu. Mara nyingi kwa mambo makubwa hasa maazimio makubwa ya Kimataifa watu wetu hawapati elimu ya kutosha. Kwa hiyo, ningesisitiza kwamba, vyombo vinavyohusika vitoe elimu kwa wananchi wetu waweze kujua ni namna gani na taratibu zipi zinatakiwa kufikia chombo kikubwa namna hii kitakapoanza. Kwa hiyo, nadhani isiishie tu kwenye Bunge kuridhia, lakini kuwe na mkakati maalum wa kuwaelimisha wananchi wetu kwamba kuna chombo ambacho si Serikali tu inaweza kukifikia au kupeleka kesi yake au malalamiko yake, lakini hata mwananchi mmoja mmoja dhidi ya Serikali anaweza na ana uwezo wa kupeleka kesi yake pale inapohusu haki za binadamu na haki ya mtu mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kukazia hayo kwa sababu tukiyaachia tu tukaridhia yanabaki kwenye mafaili. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. SAMEER I. LOTTO:** Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Mawaziri na Wabunge wenzangu, *Assalaam Aleykum.*

**WABUNGE FULANI:** *Waaleykum-Salaam.*

**MHE. SAMEER I. LOTTO:** Mheshimiwa Spika, mimi ni mara yangu ya kwanza kuanza mambo haya, kwa hiyo, naomba nitakapokuwa nakosea muwe mnanirekebisha. Kwa upeo wangu mdogo wa kuanzia, naunga mkono kwa hayo yote ambayo yamezungumziwa katika maazimio haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili wazo aliloleta ndugu kwamba tunataka iwe Arusha ni wazo zuri sana, Arusha ni kuzuri na kunafaa na kidogo labda tukiimarisha usalama pale kutapendeza zaidi. Lakini katika suala la *Standard and Speed* ambalo unalizungumzia na kama alivyoongelea mwenzangu hapa Mheshimiwa William Shellukindo na bwana mkubwa hapa ni kwamba tusiende kwa *speed* kubwa ikafikia mahali kwamba tukaacha mambo muhimu.

Hili azimio sisi tumekabidhiwa hapa asubuhi hii, hatujapata nafasi ya kupitia! Mimi nimekaa hapa naona kuna maelezo ya Mawaziri yanaendelea, nataka kusikiliza huko, nataka kusoma hapa, ninashindwa kufuatilia yote kwa pamoja kwa wakati mmoja! Naomba tusiwe tunapelekwa kwa *speed* kubwa ikawa tunaacha mambo muhimu, tupewe

tu nafasi ya kuweza kuyarejea, kuyasoma haya pengine kwa siku moja, usiku, asubuhi, halafu tuwe tunayajadili kwa kina. Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA (MHE. DR. CYRIL A. CHAMI ):**Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru wachangia mada wote, nikianza na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Kiongozi wa Upinzani, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa na Mheshimiwa Sameer Lotto, ambao wote kwa ujumla wao wamepongeza hoja hii ya Serikali na kuiunga mkono.

Napenda kuwahakikishia watoa hoja pamoja na Wabunge wote kwamba Wizara yangu itazingatia yale yote ambayo mmependekeza ili kuhakikisha kwamba tunaupeleka Muswada huu panapotakiwa kwa wakati wake. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Maazimio yaliyotajwa hapo juu yaliridhiwa na kupitishwa na Bunge)*

**HOJA YA KUJADILI HOTUBA YA MHESHIMIWA RAIS**

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, aliyoitoa wakati wa kuzindua rasmi Bunge lako la Awamu ya Nne ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 30 Desemba, 2005 hapa Bungeni Dodoma.

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii kumpongeza tena Mheshimiwa Rais kwa ushindi wa kishindo alioupata katika Uchaguzi Mkuu kupitia Chama cha Mapinduzi. Aidha, nawapongeza tena Waheshimiwa Wabunge wote mlioshinda katika Majimbo yenu na wale wote ambao wameteuliwa kuwa Wabunge katika Bunge hili la Awamu ya Nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nikupongeze wewe binafsi kwa kuchaguliwa kuwa Spika wetu. Nakupongeza sana. Nampongeza pia Naibu Spika kwa kuchaguliwa kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tangu tulipokutana katika kikao cha kwanza hapa Dodoma katika sherehe ya via

Napenda kutumia fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa kuwa Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge ambao ni

Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, (CCM), Kamati ya Fedha na Uchumi; Mheshimiwa John Momose Cheyo, *(UDP),* Kamati ya Hesabu za Serikali; Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai, (CCM), Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa; Mheshimiwa George Malima Lubeleje, (CCM), Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala; Mheshimiwa William Hezekiah Shellukindo, (CCM), Kamati ya Uwekezaji na Biashara; Mheshimiwa Anna Margareth Abdallah, (CCM), Kamati ya Mambo ya Nje na Mheshimiwa William Jonathan Kusila, (CCM), Kamati ya Ulinzi na Usalama.

Wengine ni Mheshimiwa Gideon Asimulike Cheyo, (CCM), Kamati ya Kilimo na Ardhi; Mheshimiwa Omar Shaaban Kwaangw', (CCM), Kamati ya Huduma za Jamii; Mheshimiwa Juma Suleiman Nh'unga, (CCM), Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge; Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, (CCM), Kamati ya Maendeleo ya Jamii; Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, (CCM), Kamati ya Maliasili na Mazingira na Mheshimiwa Mohammed Hamisi Missanga, (CCM) Kamati ya Miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge ambao wameteuliwa na Mheshimiwa Rais kuunda Baraza la Mawaziri katika Serikali ya Awamu ya Nne. Naomba wakubali salaam zangu za pongezi kwa ujumla wao. Uteuzi wao ni ishara ya imani kubwa aliyonayo Mheshimiwa Rais kwamba wataweza kutekeleza yale yote tuliyowaahidi wananchi kufanya katika kipindi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella; Mbunge wa Ukerewe, kwa kuchaguliwa kuendelea kuwakilisha Bunge letu katika Bunge la Afrika. Ni matumaini yetu kwamba, ataendelea kuwa Rais wa Bunge hili la Afrika kwa muda mrefu ujao. Hii ni heshima kubwa kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge wengine wote ambao walichaguliwa kutuwakilisha katika Bunge la Afrika ambao ni Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, Mbunge wa Kiembesamaki (CCM), Mheshimiwa Athumani Janguo, Mbunge wa Kisarawe (CCM), Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mbunge wa Mwanga (CCM) na Mheshimiwa Phares Kabuye, Mbunge wa Biharamuko Magharibi *(TLP).* Naelewa kwamba bado tutaendelea na mchakato wa kuwachagua wawakilishi wetu katika Bunge la Afrika baada ya baadhi ya wawakilishi waliochaguliwa hapo awali kuteuliwa kuingia katika Baraza la Mawaziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jana pia Mheshimiwa Rais amewateua Wakuu wa Mikoa na kutoka miongoni mwetu amewateua Waheshimiwa Wabunge. Naomba nitumie nafasi hii nimpongeze sana Mheshimiwa Monica Mbega, Mheshimiwa Dr. James Msekela, Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz na Mheshimiwa William Lukuvi. Nawapongeza pia Wakuu wa Mikoa wengine wote walioteuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nyote mtakubaliana nami kuwa hotuba aliyoitoa Mheshimiwa Rais hapa Bungeni ilikuwa nzito, inayoonyesha umakini, umahiri na yenye upeo wa hali ya juu, tena iliyowasilishwa kwa ustadi na ufundi wa kipekee kabisa. Hotuba ya Mheshimiwa Rais ilitoa maelekezo na changamoto ya kile tunachotakiwa kufanya katika kipindi cha awamu ya nne.

Mheshimiwa Spika, aidha, imetuonyesha bayana na kwa uwazi maeneo ambayo Serikali ya Awamu ya Nne itazingatia ili kufanikisha ahadi zake kwa wananchi waliotuchagua. Utekelezaji wa maelekezo haya kwa ufanisi ndicho kipimo tutakachopimwa nacho na wananchi waliotupa ridhaa ya kuwawakilisha.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Rais imegusa maeneo mbalimbali ambayo sisi Wabunge tunatakiwa kushirikiana na wananchi na wadau wengine wa maendeleo kuyatekeleza. Kwa kukumbushana, maeneo ya jumla aliyozungumzia Mheshimiwa Rais yalihusu demokrasia ya vyama vingi vya siasa, majukumu ya msingi ya Serikali ya Awamu ya Nne, umoja wa Kitaifa na suala la amani na utulivu. Aidha, aligusia pia masuala ya utawala bora, rushwa, utendaji Serikalini na masuala ya mahakama. Maeneo mengine ni kuhusu mapato na matumizi ya Serikali, maendeleo ya kilimo na kazi za Serikali kwenye uchumi wa soko.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Rais pia imeelezea maeneo mengine muhimu ikiwemo maeneo ya viwanda vidogo na vya kati, sayansi na teknolojia, uchumi unaoshirikisha raia wengi, ajira na viwanda, ushirika na masuala ya huduma za jamii zikiwemo elimu na afya.

Aidha, Mheshimiwa Rais alizungumzia masuala ya maji, UKIMWI, makundi maalum, utalii na masuala ya hifadhi ya mazingira. Aliweka mkazo pia katika masuala yanayohusu michezo, burudani na utamaduni, mipango miji, ujenzi na utunzaji wa barabara, ulinzi na usalama wa Taifa, nishati na mambo ya nje na ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alisisitiza umuhimu wa kila chama cha siasa kuandaa sera zinazolenga katika kulijenga Taifa letu bila kuligawa, kulihujumu, kulisaliti na bila kulidhoofisha au kulibomoa. Alitukumbusha kwamba sasa ni wakati muafaka wa kuangalia upya namna vyama vya siasa vinavyoendeshwa na kwamba ni vizuri tuwe na mjadala wa Kitaifa utakaotuwezesha kuandaa mwongozo wa maadili yatakayoongoza shughuli za kisiasa kwa vyama vyote vya siasa bila kubagua. Hii ni changamoto kubwa kwa vyama vyetu na wanachama wake hasa sisi Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umoja wa Kitaifa, Mheshimiwa Rais alizungumzia suala hili kama mhimili wa amani na utulivu. Alibainisha wazi mambo yatakayotusaidia katika kujenga na kudumisha umoja wa Kitaifa. Mfano mmojawapo ni kufufua Jeshi la Kujenga Taifa ambalo miaka iliyopita lilituwezesha kukuza vijana wetu katika maadili ya umoja, kuheshimiana na kupenda kufanya kazi bila kujali itikadi za dini, jinsia na ukabila.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Kujenga Taifa wakati huo lilikuwa ni kama jando la vijana katika kujenga Utaifa wao. Mafunzo ya awali yaliwaandaa vijana katika stadi mbalimbali kama vile ujenzi, ufugaji bora, kuhifadhi mazingira na kadhalika. Ni vema Waheshimiwa Wabunge tulijadili hili kwa kuzingatia manufaa hayo kama hoja ya msingi

ya kuongeza kasi ya kuamua kurejesha utaratibu wa vijana wetu kujiunga na JKT. Ninaamini tutabainisha faida nyingi zaidi ya hizo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais pia alizungumzia juu ya utawala bora na kwamba Serikali yake itazingatia sera za kuheshimu mgawanyo wa madaraka kati ya mihimili mikuu ya dola yaani Utawala, Bunge na Mahakama.

Mheshimiwa Spika, kuhusu rushwa, Mheshimiwa Rais aliahidi kuendeleza mapambano dhidi ya rushwa. Jambo muhimu ni kuangalia kama mikakati tuliyojiwekea katika kufanikisha zoezi zima la kupambana na rushwa limefanikiwa kiasi gani. Ni wajibu wetu kama Wabunge kutumia Bunge hili Tukufu kumsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza yote aliyosema kwa kuzingatia kwamba Bunge ni moja ya mihimili mikuu ya dola. Tushirikiane na wananchi wetu kubainisha vyanzo na mianya ya rushwa kuanzia kwenye shughuli za kisiasa hadi Serikalini katika ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alisisitiza umuhimu wa kuangalia upya mikataba mikubwa kwa maana ya kuona kama katika mikataba hiyo Serikali imenufaika kwa kiwango kinachostahili au ni watu wachache wamejinufaisha kwa rushwa na kuinyima Serikali mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mahakama, itabidi tushirikiane katika kuhakikisha kwamba wananchi wanapata haki zao kama inavyostahili bila kucheleweshwa. Uzoefu unaonyesha kwamba mara kwa mara wananchi wanapolalamika na kuona matatizo ya kijamii na kero zao hazitatuliwi mapema wanainung'unikia Serikali. Hata hivyo, hali hii husababishwa na baadhi ya watendaji ambao hawaoni na wala hawaelewi umuhimu wa kuweka kipaumbele katika utatuzi wa kero za wananchi kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuna haja sasa kwamba vyombo mbalimbali vinavyohusika na masuala ya aina hii hasa Polisi na Mahakama wajenge fikra mpya zinazoendana na kasi mpya ya kutocheleweshe maamuzi yanayohusu masuala yanayogusa wananchi wengi na yenye maslahi makubwa kwa Taifa. Natamani sana kama Majaji na Mahakimu nao wangesema watatoa haki kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utendaji Serikalini ni miongoni mwa jambo ambalo limezungumzwa kwa kina kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais. Tunapozungumzia utendaji Serikalini msisitizo ni uadilifu na uwajibikaji kwa Serikali na wananchi waliotuchagua. Hapa nitoe mfano. Hivi karibuni nilivyokuwa ziarani mkoani Shinyanga na Kilimanjaro nilitoa fursa kwa wananchi kueleza kero zao katika mikutano ya hadhara. Jambo moja linalojitokeza ni kwamba, kero zinazoelezwa na wananchi nyingi zingeweza kutatuliwa mapema iwapo viongozi katika ngazi mbalimbali wangefanya vikao vya mara kwa mara na wananchi bila kusubiri viongozi wa Kitaifa. Hali hii haionyeshi uwajibikaji kwa viongozi na watendaji wenye dhamana ya kuwatumikia wananchi. Kwa hiyo, natoa wito tena, kwa viongozi na watendaji katika ngazi mbalimbali kuwa karibu na wananchi, kufanya vikao na kusikiliza kero zao ili kuzitafutia ufumbuzi wa haraka.

Vile vile, upo udhaifu wa usimamizi kwa baadhi ya watendaji hasa katika ngazi ya Halmashauri. Kwa mfano, katika ziara hiyo hiyo Wilayani Same nilishangaa kupewa maelezo kuwa tangu mwezi Oktoba, 2005 hadi mwezi Februari, 2006 Wilaya haijaweza kusambaza tani 490 za mahindi za awamu ya kwanza katika vijiji vyote vilivyoathirika na njaa ingawa fedha za kusambaza walikwishapatiwa. Aidha, tani nyingine 549 za awamu ya pili zilikuwa bado hazijachukuliwa kutoka Hifadhi ya Chakula ya Taifa.

Naomba nitumie fursa hii kusisitiza kuwa katika hali ya janga la njaa tulilonalo, kwa sasa Serikali haitavumilia watendaji wanaotoa visingizio vya kushindwa kupeleka chakula cha msaada kwa wananchi walioathirika. Watendaji katika Serikali, katika ngazi zote, wanapaswa kuondokana na hulka ya utendaji wa kazi kwa mazoea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kuongeza mapato ya Serikali, nidhamu katika ukusanyaji mapato na udhibiti wa matumizi ndiyo msingi wa kujenga Taifa lenye uchumi endelevu katika utekelezaji wa mipango yake. Tusipojitahidi kukusanya mapato ya Serikali na wakati huo huo kuwa na nidhamu katika matumizi, ni dhahiri kwamba mipango yetu yote ya kiuchumi itaathirika. Kama alivyosema Mheshimiwa Rais, nidhamu katika kukusanya mapato na kuepuka matumizi mabaya ya kile kilichopatikana iwe ni sehemu ya uwajibikaji na utawala bora kwa viongozi na watendaji. Wananchi nao watusaidie.

Hivi sasa kwa mfano, ukienda katika maduka ya baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu kununua bidhaa mbalimbali utaulizwa kwanza kama unataka bidhaa hiyo kwa bei ya *VAT* au bila *VAT*. Mara nyingi wananchi wengi wanalazimika kukubali bei isiyo na *VAT* ambayo ni nafuu hivyo kuikosesha Serikali mapato. Haya ni baadhi ya maeneo ambayo Mheshimiwa Rais amewaagiza *TRA* na Hazina wayafanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Kilimo itaendelea kuwa mhimili wa uchumi wetu. Mheshimiwa Rais amesisitiza kwamba, wataalam wa kilimo watumike kuendeleza kilimo cha umwagiliaji maji na kutoa huduma za ugani. Serikali itashirikiana na sekta binafsi kuhimiza ubora wa mazao yetu na kutafuta masoko. Ili kuboresha ufugaji, Mheshimiwa Rais ameagiza tutoke katika utamaduni wa kuchunga na tufuge kisasa na kibiashara. Mheshimiwa Rais ameagiza mamlaka zote za mikoa kutenga maeneo maalum kwa ajili ya malisho ya mifugo. Kwa upande wa uvuvi alisisitiza kutumia raslimali zilizopo kwa maendeleo yetu.

Mheshimiwa Spika, sekta mojawapo inayochangia ukuaji wa haraka wa uchumi ni viwanda. Viwanda ndivyo vinaongeza thamani ya mazao ya kilimo na mifugo. Mheshimiwa Rais amezungumzia viwanda vikubwa, vya kati na viwanda vidogo kwamba vitasaidia kuongeza ubora na thamani ya mazao yetu ya kilimo na mifugo.

Aidha, amezungumzia umuhimu wa kuwasaidia wazalishaji wadogo wadogo kuwaongezea mitaji na kuongeza ubora wa mazao yao ili waweze kupata soko. Katika eneo hili, Mheshimiwa Rais ametoa changamoto kwa Serikali kuimarisha na kurahisisha upatikanaji wa huduma zitakazowezesha uanzishwaji na uendelezaji wa miradi ya

viwanda vya kati, vidogo na hasa vijijini ili kukuza uchumi, kuongeza ajira na kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amebainisha kuwa Awamu ya Nne ya Serikali yake itahimiza matumizi ya sayansi na teknolojia, pia itawekeza katika utafiti na kuimarisha Mfuko wa Taifa wa Sayansi na Teknolojia. Kuhusu Teknolojia ya Mawasiliano, Mheshimiwa Rais ameahidi kuongeza kasi ya kuandaa mazingira yatakayowezesha kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Nina hakika jitihada hizi zitatuwezesha kukabiliana na changamoto zinazojitokeza kwenye mazingira ya utandawazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchumi unaoshirikisha raia wengi, Mheshimiwa Rais ametoa tahadhari kutokana na tofauti kubwa inayojitokeza kati ya walionacho na wasionacho. Hata hivyo ameahidi kuwa Serikali itafanya mipango ya kuwawezesha wasionacho wajikwamue kutoka katika lindi la umaskini. Changamoto ni jinsi gani tutakavyowawezesha hao wasionacho ili nao waweze kushiriki kikamilifu katika kuchangia shughuli za kukuza uchumi wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais amebainisha hatua za kuchukua kuwawezesha wafanyabiashara na wawekezaji wadogo wadogo kushiriki katika uchumi wa kisasa. Ametoa changamoto kwa Watanzania wasomi mmoja mmoja au kwa vikundi vya ushirika wenye fani mbalimbali kushiriki katika uwekezaji na hivyo kujiajiri wenyewe kama mchango wao katika uchumi na katika sekta binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Utalii ni muhimu katika ukuzaji wa uchumi wetu. Ukweli unaojionyesha ni kwamba kama tukijikita katika Sekta hii tunaweza kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi katika nchi yetu. Tutumie raslimali zilizopo kuwavutia watalii na wawekezaji wengine kuingia katika sekta hii. Ni muhimu tujitangaze vizuri zaidi na tuongeze ubora wa huduma zetu na usalama kwa watalii wanaokuja nchini.

Mheshimiwa Spika, suala la elimu limezungumziwa na ukweli ni kwamba hakuna Taifa lililopata maendeleo bila kuendeleza elimu. Mheshimiwa Rais ametoa hatua ambazo Serikali itachukua kufikia malengo ya elimu katika Awamu ya Nne.

Kwa upande wa sekta za afya, maji na huduma nyingine za jamii, kusudio la Serikali ni kuondoa kero katika utoaji wa huduma hizo. Hivyo, Wizara husika zinapaswa kuandaa mikakati thabiti ya utekelezaji inayozingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, hifadhi ya mazingira ni eneo ambalo linahitaji nguvu za pamoja na za haraka katika kuepusha athari zinazoweza kutokea kama hatujali na kuzingatia kanuni zake. Hivi sasa nchi yetu imekumbwa na baa la njaa na ukame, baadhi ya maeneo nchini yana hali mbaya, tunahitaji kuhifadhi misitu, vyanzo vya maji na kupanda miti kwa wingi ili kuzuia nchi yetu kuwa jangwa. Hatutaoneana haya katika hili. Vyanzo vya maji ni lazima vilindwe kwa nguvu zetu zote. Ni muhimu sasa kuwa

na mipango shirikishi ya muda mrefu ya matumizi endelevu ya mabonde ya maji na utunzaji wa mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa michezo, burudani na utamaduni tumehimizwa kuendeleza sekta hizi katika ngazi zote. Vile vile, Mheshimiwa Rais amegusia umuhimu wa kushirikiana na kukuza lugha ya Kiswahili ambayo kwa sasa inatumika katika Umoja wa Afrika na inaendelea kupata umaarufu duniani.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuwa mfano wa utekelezaji wa suala hili pale alipohutubia mkutano wake wa kwanza wa Wakuu wa Nchi Barani Afrika kule Khartoum, Sudan kwa lugha ya Kiswahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la ujenzi na utunzaji wa barabara, limepewa umuhimu wa kipekee katika kuendeleza na kukuza uchumi wa Taifa letu. Aidha, suala la upatikanaji wa nishati limezungumzwa na Mheshimiwa Rais na amesisitiza na kuahidi kulipa kipaumbele suala la upatikanaji wa umeme nchini. Hayo yote tunatakiwa kuyawekea mkakati wa utekelezaji ili kuleta maendeleo endelevu kwa wananchi. Hakuna Taifa lolote duniani lililoweza kuendelea pasipokuwa na miundombinu bora ya kiuchumi. Miundombinu ya usafiri na usafirishaji, umeme na mawasiliano ya simu ni maeneo ambayo lazima tuweke macho yetu wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Rais, suala la Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa limezungumziwa. Aidha, Rais,ameahidi kwamba Serikali ya Awamu ya Nne, itatumia fursa zilizopo katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika *(SADC),* katika kuleta maendeleo ya kweli kwa Watanzania. Aidha, nchi yetu kwa kushirikiana na wenzetu wa nchi jirani zinazotuzunguka tutaendelea kushirikiana kwa kutumia fursa hii kuleta maendeleo na hivyo kujikwamua kutoka katika lindi la umaskini.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Rais, yeye binafsi pamoja na Marais Wastaafu, waliomtangulia kwa kuiwezesha Tanzania kushika kiti cha Urais cha Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, kuanzia tarehe 1 Januari, 2006. Kitendo hicho kimetupatika sifa kubwa kama nchi inayojali utu na kulinda amani duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuhitimisha kuwasilisha hoja ya kujadili hotuba ya Mheshimiwa Rais, napenda kusisitiza masuala yafuatayo ambayo Serikali itayashughulikia kwa umahiri na umakini mkubwa katika muda mfupi ujao ikiwa ni mwanzo wa kutekeleza ahadi za Mheshimiwa Rais.

Kwanza, kuwawezesha wanafunzi wengi waliofaulu mtihani wa darasa la saba kujiunga na elimu ya sekondari. Takwimu zinaonyesha kuwa katika Mikoa yote nchini, karibu asilimia 53.5 ya waliofaulu wamekosa nafasi za kujiunga na masomo ya sekondari. Nimeshatoa maelekezo kwa uongozi wa kila Mkoa, uhakikishe kuwa angalau asilimia 50 ya wanafunzi waliofaulu katika Mikoa yao wanawezeshwa kujiunga na

masomo ya sekondari. Nimetoa muda wa miezi mitatu ili kila Mkoa utoe taarifa ya hatua walizochukua na hali ikoje baada ya hatua hizo kuchukuliwa. *(Makofi)*

Pili, nchi yetu inayo rasilimali kubwa ya maji katika mito ambayo inaweza kutuwezesha kupanua kilimo cha umwagiliaji. Kama ilivyotamkwa katika Ilani ya Uchaguzi wa CCM, kutoka hekta 250,000 zinazolimwa hivi sasa hadi 2,500,000.

Mheshimiwa Spika, nimeielekeza Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, kuwa ni lazima tuwe na mkakati wa utekelezaji utakao ainisha hatua madhubuti za kutufikisha huko na ni lazima tuanze katika mwaka wa fedha 2006/2007. Lazima kilimo cha umwagiliaji kipate hadhi na mpango maalum wa kipaumbele. *(Makofi)*

Tatu, hifadhi ya mazingira haiwezi tena kuwa suala la maagizo au maelekezo. Lazima tuchukue hatua za dhati. Uharibifu na uchafuzi wa mazingira unaanza kutuletea maafa. Hali niliyoikuta Wilayani Same ambapo upepo wenye nguvu unasomba udongo wa juu na kupeperusha mbali ni moja ya matokeo ya athari za uharibifu wa mazingira. Ilifika mahali hata magari kwenda inakuwa taabu kwa sababu ya vumbi linalotoka. Ni wajibu wetu sote viongozi wa kuchaguliwa, wataalam na wananchi kuonyesha kwa vitendo kuwa maendeleo endelevu yanawezekana kwenye mazingira hayo. Tupige vita uchomaji misitu, ukataji wa misitu ovyo, kilimo na ufugaji kwenye vyanzo vya maji na kadhalika. Tutaweza kumsaidia Mheshimiwa Rais, katika *agenda* yake ya kuleta mabadiliko ya maisha kwa wananchi endapo tutajali hifadhi ya mazingira. Hatuwezi kusubiri tena.

Mheshimiwa Spika, nne, uwezo wa Serikali yoyote kutekeleza malengo yake unategemea pamoja na mambo mengine uwezo wa viongozi na wataalam wake kusimamia na kuratibu mipango na mikakati yenye lengo la kuboresha huduma zinazotolewa kwa wananchi. Mheshimiwa Rais, ametuonyesha njia kwa kauli na vitendo vyake. Hotuba yake imetupa dira, ziara za kukutana na viongozi na wataalam katika Wizara na Taasisi za Serikali zimewezesha kutoa changamoto na maelekezo ya ana kwa ana kwetu sote tunaomsaidia. Ari, nguvu na kasi yake ni kubwa. Lazima basi nasi tuonyeshe kwa vitendo kuwa tunaweza kumudu kasi na nguvu hiyo. Serikali kamwe haiwezi kuwavumilia viongozi na watendaji watakaokuwa legelege katika kutekeleza maagizo na maelekezo yanayotolewa mara kwa mara. Viongozi Mkoani na Wilayani watambue dhamana waliyobeba na wawajibike ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais Kikwete, utakubaliana nami ni kiongozi muungwana na anayependa kutekeleza yale yote aliyowaahidi Watanzania. Ni wajibu wetu kumpa ushirikiano wa hali ya juu. Wito wangu kwenu ni kuwa hotuba hii ichochee mjadala utakaoibua mawazo mapya na mikakati mipya ya kutuwezesha kubadilisha maisha ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, hoja hii ya Serikali haikupita kwenye Kamati yoyote. Lakini nimepeleka taarifa kwa Kiongozi wa Upinzani, kwamba pamoja na kuwa hatutakuwa na msemaji kutoka kwenye Kamati yoyote lakini ni vizuri kwa demokrasia ndani ya Bunge kwamba Upinzani upewe nafasi kutoa maoni kuhusu hoja hii iliyo mbele yetu. Kwa hiyo, nitafanya hivyo.Lakini kabla ya kufanya hivyo ya kumuita Kiongozi wa Upinzani, napenda tu nitangaze kwa ajili ya maandalizi, wachangajiaji wanakaribia 90 lakini tuna siku nne. Kwa hiyo, isitie shaka. Sasa kwa mpangilio tu ili Waheshimiwa wawepo na wajiandae nitaanza na Mheshimiwa Job Ndugai, atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Jenista Mhagama, baadaye Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mheshimiwa Phares Kabuye, ambaye naye atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Nyawazwa, halafu itamfikia Dr. Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Wilson Masilingi na Mheshimiwa Philemon Ndesamburo. Nadhani hapo tutakuwa tumefika saa inayotakiwa. Kwa hiyo, hao wajiandae. Sasa nitamuita Kiongozi wa Upinzani Bungeni. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI BUNGENI:** Mheshimiwa Spika, nami niungane na wenzangu kukupongeza wewe, kumpongeza Naibu Spika, kuwapongeza Mawaziri, Manaibu Waziri, kuwapongeza Wakuu wa Mikoa waliopewa kazi jana, lakini pia niwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Wawi kwa kunipa heshima hii ya kuwa Mbunge wa Jimbo lao. Nawaahidi kama kiliniagiza chama changu kwamba nisiwaangushe, sitawaangusha. *(Makofi)*

Niungane na Mheshimiwa Waziri Mkuu katika kuipongeza Hotuba ya Rais, aliyoitoa katika Bunge letu Tukufu, kwamba hotuba hiyo ilijaa matumaini iliyochambua kwa kiwango kikubwa matatizo na matakwa ya wananchi. Naamini inahitaji pongezi zetu wote. Rais alionyesha uwezo mkubwa katika kuwasilisha hotuba yake na ni matumaini yetu kuwa aliyoyaahidi atayatekeleza. Maana tatizo siyo kupanga wala kusema, tatizo ni kutembea kwenye mipango na maneno yenyewe. Unayosema umma wote wa Tanzania unangoja utekelezaji wa ahadi zilizotolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi nimefarijika sana na hotuba ya Rais na kwa kuwa namuelewa sana tokea mwaka 1978 naamini atatekeleza kwa dhati aliyoahidi. Sisi upinzani tunachohitaji ni maendeleo na hasa kumuondolea Mtanzania umaskini wa kipato, utawala unaoheshimu sheria na kutoa haki sawa kwa watu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya Rais, ametuasa sisi Wapinzani tujiangalie ni vipi tumeshindwa katika uchaguzi huu. Namshukuru sana Rais, kwa kusema hilo. Sisi hatuna ubishi na hilo ila tunaomba kulikumbusha Bunge lako Tukufu kwamba wakati nchi yetu inataka kuingia katika mfumo wa vyama vingi iliundwa Tume iliyoongozwa na Marehemu Jaji Francis Nyalali, pamoja na mambo mengine ilipendekezwa kufutwa kwa sheria 40 za ukandamizaji, kuwa na muda wa mpito ili kuweka mazingira mazuri ya uwiano wa ushindani wa kisiasa.

Aidha, walishauri mfumo wa Serikali Tatu, ili kuondoa manung'uniko katika Muungano wa kwamba Zanzibar wanaowakilishwa sana ndani ya Jamhuri ya Muungano kuliko wa Bara wanavyowakilishwa katika Serikali ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya Serikali iliyatupitilia mbali mapendekezo ya Jaji Nyalali na huyo kwetu sisi ndio mchawi mkubwa wa kwanza wa Kambi ya Upinzani kwa mazingira yaliyowekwa ya siasa hayakwenda kama vile Jaji Nyalali alivyopendekeza. Aidha, Tume ya Jaji Kisanga, nayo ilitoa mapendekezo kadhaa, lakini yote yaliachwa kwa hali inayoonekana kuandaa mazingira ambayo chama tawala kingepata mtihani mgumu katika uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huyu ndiye mchawi wetu wa kwanza kukataa kwa Serikali kutekeleza mapendekezo ya Tume hizo mbili. Pamoja na kasoro hizo vyama vya upinzani havikufanya vibaya sana katika uchaguzi. Kwani rasilimali chache walizokuwa nazo, Tume za Uchaguzi ambazo zimekuwa ni nyenzo muhimu katika kuendesha uchaguzi za vyama vingi nazo zimekuwa ndiyo mchawi wetu mkubwa maana haiwezekani matokeo yao ya Mikoa 21 yakapatikana kwa muda wa saa 48, lakini matokeo ya Mikoa mitano ya Zanzibar yakapatikana zaidi ya saa 48 na yakatangazwa mara mbili na mara zote mbili ni tofauti matokeo yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wachawi wetu tunawajua, ni wengi kwa mfano vyombo vya habari vinapoamua kukataa hata matangazo ya kulipiwa, vyombo vya dola kujihusisha na kuegemea upande mmoja wa Chama Tawala, kinyume na makubaliano ya muafaka baina ya CCM na *CUF,* wagombea wetu kutekwa nyara na kuteswa hadi kukaribia kufa, wengine kufunguliwa kesi za kubuni na kadhalika. Hao ndiyo wachawi wetu waliosababisha tushindwe kisayansi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna chama kinachoweza kushinda uchaguzi bila ya kuwa na fedha za kutosha vyama vyetu vilitegemea ruzuku ndogo na michango midogo sana kutoka kwa wanachama wetu ambao pia wachawi wetu huwaandama sana ili wasivisaidie vyama vyetu. Chama Tawala, kimeweza kujikusanyia mapato mengi kutoka vyanzo mbalimbali, marafiki na kadhalika wakati sisi vyama vya upinzani hatuna nyenzo za kufanyia kazi. Huyu ni mchawi wetu mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naona niwataje baadhi tu ya wachawi wetu ili tumsaidie Rais katika kutekeleza ahadi yake ya kuvisaidia vyama vya siasa nchini viweze kufanya shughuli zake bila ya bugudha na visiwe vinyonge katika shule zake. Sisi tutatoa ushirikiano wa hali ya juu katika kutekeleza azma hii nzuri ya Rais wetu kwani kama alivyosema Baba wa Taifa, Chama cha Siasa, kikikaa madarakani muda mrefu hujisahau. Hivyo ni vema kukawa na vyama vingine ili kukihamasisha kile chama kilichoko madarakani. Hivyo ni vema upinzani ukawa na nguvu ili chama kilichoko madarakani nacho kikaweza kutoa majibu sahihi kwa wananchi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunashauri kwanza, tunaomba uchaguzi wa Serikali za Mitaa, uwe chini ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi badala ya kuwa chini ya Waziri Mkuu hivi sasa.

Pili, Tume ya Taifa ya Uchaguzi, iundwe upya na uteuzi wa wajumbe wake waombe baada ya kutangazwa sifa za wagombea wenyewe, tatu, ujumbe wa Tume uchanganywe na vyama vingine hata kwa asilimia fulani  na nne, watendaji wa Tume waajiriwe kwa muda na wasiwe watendaji wa Serikali.

Tano, vyombo vya dola vikae chonjo katika masuala ya kisasa washughulikie usalama wa raia na mali zao.

Sita, kila chama kielezee chanzo cha mapato yake kwa kutoa ushahidi na vikaguliwe na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Wakati wa uchaguzi kila chama kionyeshe wazi kwa umma namna kitakavyopata fedha za uchaguzi, kitakavyotumia pamoja na wagombea wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Rais, anasema alipoingia tu ofisini tatizo la kwanza alilolikuta ni la njaa na leo hapa Mheshimiwa Waziri Mkuu naye ameligusia. Kambi ya Upinzani ina haya ya kusema:-

Mheshimiwa Spika, Taifa letu kwa mara nyingine tena limekabiliwa na balaa la njaa iliyosababishwa na ukame. Kambi Upinzani, kwanza inawapa pole wale wote ambao balaa hili limewaathiri na tunaungana na Serikali katika juhudi zake za kuwapatia chakula kwa bei nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani bado inaona upo udhaifu wa mipango yetu ya kuendeleza kilimo. Miaka ya 1980 na 1990 tulikuwa na Mikoa minne tukiita *big four,* ambayo kwa kawaida haikosi mvua hiyo. Ilikuwa Mikoa ya Rukwa, Ruvuma, Mbeya, Iringa na hatimaye Arusha. Wakati huo tatizo lilikuwa ni kusambaza chakula na siyo uhaba wa chakula. Leo baada ya miaka 42 ya Uhuru tatizo ni chakula na usambazaji wa chakula hii ni kasoro kubwa.

Mheshimiwa Spika, tatizo la njaa katika nchi yetu si kitu ambacho kimekuja ghafla tu, ila ni hali iliyokuwa inategemewa kulingana na historia ya miaka ya nyuma. Pamoja na tafiti na takwimu zilizokusanywa na Mashirika mbalimbali ya Kiserikali na yale yasiyokuwa ya Kiserikali. Kama tunakumbuka vizuri mwaka 2003 mwishoni, mwaka 2004 mwanzoni uhaba wa chakula uliathiri sana Mikoa ya Dodoma, Singida ambayo takribani watu 200,000 katika maeneo mbalimbali ya Mikoa hiyo walikumbwa na njaa.

Mheshimiwa Spika, katika takwimu zilizotolewa na Serikali Agosti, 2005 zinaonyesha kuwa watu 594,503 katika Wilaya 34 walikuwa wanakabiliwa na hali mbaya ya ukosefu wa chakula na bei ya mahindi karibu katika Mikoa hiyo, ilionyesha kupanda maradufu. Uhaba mkubwa wa waathirika wa balaa la njaa ni wale walioko katika Wilaya ya Ngorongoro, Arumeru Mkoa wa Arusha, vile vile Wilaya ya Meatu, Mkoa wa Shinyanga, Singida na hata hapa Dodoma. Aidha, baadhi ya Vijiji na Kata katika Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali halisi wa utendaji wa nchi yetu na uzoefu unaonyesha kuwa hata kama Serikali itapata chakula kingi cha misaada kutoka nje kama ambavyo inaonyesha kuwa Kampuni moja imeagiza tani 36,000 kutoka Marekani, tatizo kubwa ni jinsi gani chakula hicho kinasambazwa na kwa walengwa.

Tumeshuhudia hivi karibuni watu waliopewa dhamana hiyo ya kusambaza chakula hicho wameanza kufanya biashara na kuacha walengwa bila ya kuwa na msaada wowote. Tunamshukuru Rais wetu kwa kulitolea kauli hili. Tunaomba wanaohusika walisimamie kikamilifu ile kauli ya Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni vema tukarudia utaratibu wa zamani wa kuwa na Mikoa ambayo tuna hakika itapata chakula cha kutosha hivyo tuipatie pembejeo za kutosha na mikopo nafuu ili waendeleze kilimo. Hii itakuwa kama ndio Benki yetu ya chakula kama tulivyokuwa zamani *comrade* anakumbuka wakati huo.

Mheshimiwa Spika, naomba ninukuu maneno ya Mheshimiwa Rais katika hotuba yake ambayo alimnukuu Mwalimu Nyerere: "Mwalimu Nyerere hakurithi Taifa kwa wakoloni, alirithishwa mkusanyiko wa makabila na watu wa dini mbalimbali. Lakini kwa heshima na busara kubwa akatambua kuwa hata uchumi wa Tanzania ungekua kwa kiasi gani iwapo hakuna msingi imara na hisia za dhati za utaifa baada ya muda uchumi huo utakuwa hauna maana."

Mheshimiwa Spika, tunampongeza sana Rais kwa kuliona hili. Lakini kama kweli Zanzibar kungekuwa na viongozi wenye Utaifa kusingekuwa na mpasuko katika Unguja na Pemba kama Mheshimiwa Rais aliuainisha katika hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia kwa siku za karibuni bado Watanzania tunabaguana kwa misingi ya rangi zetu, dini zetu na maeneo tunayotoka pale unapokuwa uongozi wa Kitaifa. Hili ni jambo la aibu sana kwa nchi yetu kama Tanzania ambayo waasisi wake walijitahidi sana kutujengea umoja wa Kitaifa. Ndiyo leo tuna Muungano unaotimiza miaka 42 sasa.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Rais, ukurasa wa 18 anapozungumzia kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa mpasuko wa kisiasa na kihistoria kati ya Unguja na Pemba hasa uliozidishwa na matokeo ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005 tunahitaji masuala haya kujiuliza, je, ni historia ipi Mheshimiwa Rais, alitaka kuizungumzia ambayo yeye anaiona kwamba imeleta na inaendelea kuleta mpasuko huo wa kisiasa Zanzibar? Au ni ile historia ya baada ya Mapinduzi inayoendelea hadi leo katika kuwagawa Wazanzibar? Au ni ile historia ya upande mmoja wa kushika hatamu na kujiona peke yao ndiyo yenye haki ya kutawala Zanzibar na kufaidika matunda ya Serikali? Au historia inayosema tulipata nchi kwa mapanga na hatuko tayari kuitoa nchi hiyo tuliyoipata kwa kumwaga damu kwa vipande vya karatasi na maneno? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hizi kwa mawazo ndiyo historia ambazo Rais, anazotakiwa kuzifanyia kazi na siyo mpasuko wa kushinda au kushindwa kwa CCM au *CUF* Unguja au Pemba bali ni kama alivyosema yeye mwenyewe kuwa lazima aende ndani zaidi ya muafaka katika kutafuta ufumbuzi wa matatizo ya Zanzibar.

Sisi kwa tafsiri yetu ni kufanya mabadiliko ya Katiba yanayotambua umuhimu wa ushiriki katika uendeshaji wa nchi na makundi yote katika jamii kwa kutoa nafasi za uwiano. Hii nafikiri itakuwa ni *solution* ya kutusaidia kuondoka hapa tulipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunamuahidi Mheshimiwa Rais kwa hili na mengine yote tutampa ushirikiano wa hali ya juu ili taifa letu lisiendelee kuwa na mpasuko kwani hii ni aibu kubwa kwa taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amezungumzia rushwa, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa uzalendo na Utaifa wake uliokomaa pale alipoamua kuvalia njuga suala hili lilikuwemo ndani ya Ilani za Uchaguzi za Kambi za Upinzani la kupitia upya mikataba iliyosainiwa na Serikali, Mashirika ya Umma na Idara zinazojitegemea kwa nia ya kuongeza uwazi na uwajibikaji kwani mapapa wa rushwa wamelala katika upande huu.

Mheshimiwa Spika, tunaamini kuwa Bunge lako Tukufu litashirikishwa kikamilifu katika mchakato wa mikataba hiyo, ili wananchi wapate kuelewa kwa undani faida au hasara tuliyopata kutokana na mikataba hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Rais, vile vile aligusia suala la elimu, sisi tunaomba kutoa mapendekezo yafuatayo:-

Kwanza, Serikali ipitie upya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari *(MMES)* ambao haukidhi lengo la kila mtoto anayefaulu mtihani wa darasa la saba aweze kuendelea na Elimu ya Sekondari. Mpango huu urekebishwe kwa kuzingatia lengo hili na mkakati kabambe uandaliwe na kutekelezwa.

Pili, hatuna walimu wa kutosha katika shule nyingi za sekondari, upanuaji wa shule utahitaji kuongeza walimu. Pamoja na agizo la Waziri Mkuu, nafikiri hilo nalo lingeangaliwa kwa sababu kuwa na majengo ni jambo moja lakini unahitaji majengo, unahitaji walimu, unahitaji vifaa ili elimu iweze kutolewa pamoja na mpango wa kupanua vyuo vya elimu, unajua vijana wengi waliomaliza kidato cha sita na vyuo vikuu ambao hawana kazi. Vijana hao wanaweza kupewa kazi maalum za ualimu ili waweze kufundisha shule za sekondari. *(Makofi)*

Tatu, Serikali ifanye utafiti kuhusu uwezo wa shule za binafsi za sekondari zinazoweza kusaidia kupunguza tatizo. Serikali itoe motisha na kurahisisha taratibu za kusajili shule bila kuathiri viwango vya ubora wa elimu ili sekta binafsi iongeze uwekezaji katika elimu ya sekondari.

Nne, Serikali, iweke utaratibu wa kuwalipia ada wanafunzi waliofaulu lakini wazazi wao hawana uwezo wa kulipa ada waweze kusoma katika sekondari za binafsi. *(Makofi)*

Tano, ili kukwepa kukiuka sheria za fedha Serikali itayarishe Bajeti ndogo itakayohamisha fedha kutoka maeneo yasiyo muhimu na kupeleka katika sekta ya elimu ili vijana wetu waweze kuendelea na elimu ya sekondari.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inatahadharisha kuwa tatizo la vijana wetu kukosa elimu ya sekondari ni la muda mrefu. Tanzania ni miongoni mwa nchi za mwisho duniani kwa maendeleo ya elimu ya sekondari. Serikali isifanye kazi kwa kukurupuka bali ifanye utafiti wa kina irekebishe *MMES* na kupanga ratiba ya kudumu ya kila Mkoa, Wilaya na Kata kutekeleza mpango huo.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha na kukatisha tamaa kuwa katika kipindi cha miaka kumi iliyopita Serikali imetumia chini ya asilimia mbili ya Bajeti yake yote katika elimu ya sekondari. Kambi ya Upinzani, inaona ni muhimu kuongeza Bajeti ya Elimu kutoka asilimia 13 ya matumizi yote ya Serikali kama ilivyofafanuliwa katika sera za Kambi za Upinzani kwa kupunguza gharama za uendeshaji, matumizi ya anasa na misululu mikubwa ya misafala ya nje.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme, kwa kuzingatia Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha nyuma Serikali, imekuwa ikitoa ruzuku kwa shirika la umeme *(TANESCO)* na Kampuni ya *IPTL* ambayo inazalisha umeme na kuuza umeme huo kwa *TANESCO.* Sasa hivi tunaambiwa madeni yote ya *TANESCO* yasiyopungua bilioni 700 yanabebwa na Serikali lakini menejimenti inapewa *bonus* kwa utendaji wetu mzuri.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru Mheshimiwa Rais, katika ziara yake katika Wizara husika aligusia hilo la wananchi kutopata thamani halisi ya fedha zao na alibaini moja kwa moja kuwa lazima kuna matatizo fulani yanayosababishwa Watanzania kununua umeme kwa kiwango cha juu wakati Serikali inatoa ruzuku katika shirika hilo.

Mheshimiwa Spika, tunaamini kuwa sasa Serikali imejifunza kuwa uongozi wa Kampuni ikabidhiwe Watanzania na kupewa Mamlaka kamili wana uweze wa kufanya kazi vizuri zaidi kuliko Kampuni za kigeni. Ushahidi wa wazi ni *DAWASA* na sasa hivi *DAWASCO.* Ni vema Serikali ikaeleza ni lini Kampuni ya kigeni *Net Group Solution* itaondoka na kukabidhiwa Watanzania kuendesha *TANESCO. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ufumbuzi wa kudumu wa umeme ni kuondoa ukiritimba wa *TANESCO* yaruhusiwe makampuni mengine yauze umeme, pili, matumizi ya gesi na mkaa wa mawe uwe lengo kuu la umeme wa uhakika. Aidha, Serikali isiwe na miradi mingi midogo midogo ambayo gharama za uendeshaji itakuwa kubwa mno. Sasa tumeambiwa kuna miradi kama 5, 6 ya umeme, mimi nafikiri tuki-*concentrate* kwenye miradi miwili mikubwa ya gesi na mkaa wa mawe tunaweza tukatatua tatizo hilo.

Tatu, Serikali itueleze hatua inayochukua kupungua ughali wa umeme ili wananchi wapunguze kutumia mkaa ambao kupatikana kwake ni kifo cha miti, yaani huwezi kupata mkaa kama mti haujakatwa na hivyo kusababishwa na jangwa.

Mheshimiwa Spika, ujambazi, kumekuwapo na matukio ya ujambazi wa kupora na kutumia silaha katika kipindi cha miezi ya hivi karibuni kwa nguvu sana. Watanzania wengi wamelalamikia sana hatua zinazochukuliwa na Jeshi la Polisi, kuwa siyo makini katika kufanya kazi taarifa ya uhalifu zinapotolewa na raia wema. Tunaamini kabisa yapo mambo mengi yanayosababisha Jeshi la Polisi kutofanya kazi zake vizuri. Lakini la muhimu sana ni kutokupenda kushirikiana na wananchi kwa sababu wanazozielewa wao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kwa uzoefu ni kwamba wananchi wako tayari kulisaidia Jeshi la Polisi kutoa taarifa na vyombo vyote vya ulinzi na usalama, tatizo ni kwamba wanapotoa zile taarifa ni vipi wao wanaweza kupata taarifa kwamba jambo lao limeshughulikiwa. Hilo la la kwanza.

Lakini la pili ni pale ambapo zile taarifa zikishafanyiwa kazi yule mtoa habari hadhuriki na wale ambao aliwatolea habari.

La tatu ni kwamba vyombo hivi vya ulinzi vikikaa muda mrefu mahali pamoja na ndiyo maana mwalimu alikuwa na utaratibu kila baada ya miaka mitatu, minne, unasikia amestaafisha maafisa kwa manufaa ya umma. Ni kwa sababu ukishakaa mahali muda mrefu unazoeleka unaweza kununuliwa kwa njia rahisi sana. Hiyo ndiyo *experience* ambayo tumeiona.

Sasa leo unakuta Mkuu wa Jeshi, kila wakati yuko kwenye *television, radio* anazungumzia ujambazi. Mimi sikumkuta Liani, wala Mahundi hata siku moja akienda kwenye *television* na redio alikuwa anafanya kazi yake kama *professional. (Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Kulikuwa hakuna *Television.*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI BUNGENI:** Hata kwenye redio walikuwa hawaendi. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, nafikiri nasema sasa mpaka watu wana- *renew contract* nafikiri si jambo zuri sana halisaidii sana.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo, ningependa kabisa kwamba wale Askari ambao wamekaa muda mrefu ama wa-*rotate* au waondoshwe, wabadilishwe waletwe wengine hilo linasaidia vile vile katika kufanya kazi nzuri ya polisi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo katika suala la ulinzi ni suala zima la upelelezi wa kesi ambalo Waziri Mkuu, ameligusia ni muhimu sana likafuatiliwa kwa sababu kama kesi zinachelewa wahalifu wanapewa dhamana wanarudi tena kwenye gereza na kadhalika yako mambo mengi tukipata wakati tutakaa na Waziri nitamsaidia kumpa ushauri.

Mheshimiwa Spika, naomba kumalizia kwa kusema kwamba tatizo la mikopo na madeni ya nchi ni tatizo ambalo hivi sasa linahitaji kusimamiwa vizuri. Serikali yetu

bado inaendelea kukopa pamoja na kwamba ina uwezo wa kulipa lakini gharama za uendeshaji wa Serikali zimepanuka zaidi, usafirishaji wa bidhaa zetu kwenda nje ni mdogo sana, urali wetu wa kibiashara na nchi jirani unazidi kuwa mbaya zaidi. Tunahitaji kukaa kitako kuangalia namna gani tutaweza ku-*manage* matumizi na mapato yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mwongozo wa Spika, Kanuni ya 55(3) kuna jambo ambalo limetokea sasa nilitaka mwongozo wako.

Nimeona Mawaziri walipokuwa wanatoa hoja zao na Waziri Mkuu, baadhi ya Wabunge ambao siyo Mawaziri wamesimama, je, hawa ambao hawakusimama si utovu wa nidhamu? *(Kicheko)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa William Shellukindo.

Napenda nikumbushe kwamba si sahihi kwa wale ambao si Mawaziri kuunga mkono hoja za Serikali kwa maana ya kusimama kuziunga mkono. Wanaweza kuziunga mkono kwa kuchangia lakini siyo kusimama. Wanaosimama inaitwa ku-*second the motion* sasa anaye- *second* ni *member* wa Serikali. Ahsante sana Mheshimiwa William Shellukindo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, niendelee sasa ni mchango wa jumla, napenda nikumbushe tu ni dakika 15 kwa kila mchangiaji, lakini kengele italia katika dakika ya 10 kumkumbusha tu ili umaliziaji wa hoja uwe mzuri na ikilia kengele ya pili ni lazima mchangiaji akae, asiseme anamalizia au kuna sentensi haijaisha, unakaa hapo hapo ndio utaratibu.

Kwa hiyo, kengele ya kwanza ni tahadhari ili dakika tano ziwe za umaliziaji mzuri. Sasa nitawaita wachangiaji nitaanza na Mheshimiwa Job Ndugai na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, ajiandae.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwanza kwa heshima kubwa sana uliyonipatia ya mimi kuwa Mbunge wa kwanza kujadili hotuba ya Mheshimiwa Rais, nakushukuru sana. Lakini nianze kwa kuwashukuru wananchi wa Kongwa kwa kunichagua na kunirudisha hapa kwa mara ya pili kwa kura nyingi sana zaidi ya asilimia 90, ahadi yangu kwao ni kwamba nikiwa hapa kama alivyoshauri Mheshimiwa Rais nikiingia kwenye Bunge hili, nikitoka kwenye Bunge hili, nikijadili mambo kama ninavyofanya sasa nitakumbuka sana heshima kubwa ambayo wananchi hao wa Kongwa wamenipa na nitawatumikia kwa uaminifu mkubwa hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo kwanza nitoe pongezi kubwa kwa Mheshimiwa Rais kwa kuchaguliwa na nchi nzima kwa kishindo na sisi wa Kongwa tumempa asilimia 94 ni moja ya Majimbo yenye wapiga kura wengi sana ya vijijini,

tumempatia kura karibu 84,000 kwa Jimbo la Kongwa peke yake na kwa asilimia 94. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuna imani kubwa sana kwake na Serikali yake, tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ushindi wa kishindo aliopata Jimboni kwake Monduli na zaidi kwa nafasi hii aliyopata ya Uwaziri Mkuu, sisi wa Kongwa tunakuombea kwa Mwenyezi Mungu kwamba kazi yako iwe nzuri na tuna matumaini makubwa nawe. Niwapongeze Wabunge wote kwa kuchaguliwa kwenu, niwapongeze sana Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri, niwakumbushe tu kwamba nyie siyo tu wenzetu bali ni miongoni mwetu kwa hiyo, ni zaidi ya wenzetu, tunawaahidi kabisa kuwapa ushirikiano mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunakupongeza sana na Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo matumaini kabisa kwamba kazi yetu itaenda vizuri, mtaliongoza Bunge hili kwa hekima na busara kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wako watu wamewahi kusema kwa Kiingereza wanasema *Executives of all types are known to hide behind the fallacy of Secretaries and assistants*. Kawaida ya wakubwa wengi wawe wa mashirika au Serikali kupenda kujificha nyuma ya wasaidizi wao, makatibu wao, masekretari wao kuwapata inakuwa ni vigumu sana wana watu wako kule mbele mpaka umalize huo mchanganuo umkute unakuwa umefanya kazi kubwa sana, hii ni kawaida sehemu nyingi.

Mheshimiwa Spika, lakini Rais wetu ameonyesha mfano ambao mimi sijawahi kuuona mahali pengine. Jana alikuwa Kariakoo sokoni nilipokuwa nikitazama kwenye *television* sikuamini, anapita Kariakoo sokoni anazungumza na wafanyabiashara wa kawaida, wanunuzi wa kawaida sokoni, mimi sijui kama kuna Rais mwingine nyie mmewahi kumuona yuko sokoni tena soko lenyewe aina ya Kariakoo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, tunapata funzo gani pale kwamba viongozi tusijifiche nyuma ya hawa masekretari na makatibu na nini, tutoke twende kwa watu kama Rais wetu anavyoonyesha mfano. Rais gani hapa Mashariki mwa Afrika iwe Kenya, Uganda, Somalia, Ethiopia, Zambia, Zimbabwe? Rais gani anaweza kutoka kwenda mtaani acha habari ya sokoni kutembea kwenye mtaa? *Impossible*. Safari moja mwaka juzi nilipata bahati ya kwenda Zimbabwe dereva akawa ananirudisha *airport* nikawa naongea naye michapo tu kidogo, jamani habari za hapa anasema hapa hali mbaya sana mimi nikikutana na bwana mkubwa tuko mtaani nitamuua, dereva anasema, nikikutana na bwana mkubwa sihitaji mtu mwingine mimi nitamuua. Hasira iko kwa watu wa kawaida mmoja mmoja. Lakini Rais wetu anafika mahali pa kwenda sokoni na anashangiliwa na soko zima na nyie mnawajua watu wa sokoni kule wauzaji na wabeba mizigo wanafananaje. Hata baadhi ya Wabunge tunaweza tusiwe na ushujaa huo wa kufika sokoni Kariakoo, anatoka ndio *point* ninayoizungumzia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningependa kutumia fursa hii kuwaomba viongozi mnaomsaidia Rais mtoke muende kwa watu, Mheshimiwa Waziri Mkuu juzi ametoka ameenda kuangalia matatizo ya njaa, sasa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya

watakaoteuliwa na viongozi wengine wote funzo la kwanza ni kutoka kwenda kwa watu kuona matatizo halisi ili kuyapatia ufumbuzi halisi, tusijifungie nyuma ya masekretari, nyuma ya makatibu na kuweka ukiritimba kuweza kupatikana tutoke twende hadi kwenye maeneo. Rais ametoka amekuja kwenye Wizara zetu moja moja kwani asingeweza kuwaita Ikulu mmoja mmoja lakini ametoka amekuja kwenye Wizara moja, moja maana yake nini? Maana yake na nyie mtoke muende sasa ndio maana yake na ndio funzo kubwa tunalipata.

Mheshimiwa Spika, la pili katika hili mabadiliko ya maendeleo ya kuipanga Serikali ya Awamu ya Nne vizuri na kwa kweli yanaungwa mkono na wananchi wengi tunasubiri ngazi ya Wilaya na kuendelea na kuendelea. Ushauri wangu ni kwamba sasa huku chini ndio muhimu zaidi isije ikaishia kwenye Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya hapa twende mpaka watendaji wa vijiji, watendaji wa kata kule ndio tatizo kubwa kabisa ukibadilisha huku juu ukaacha hawa wakurugenzi wa maendeleo, ukaacha wote hawa hivyo hivyo walivyo hivi sasa hakuna tutakachopata. Mabadiliko haya yaendelee mpaka Serikali ya Awamu ya Nne ijipange vizuri yaende mpaka chini kabisa kwa Mtendaji wa Kijiji.

Mheshimiwa Spika, tukifanya hivyo tutakuwa tumeweka utaratibu ambao ni mzuri zaidi kwa ajili ya mafanikio mazuri zaidi na maendeleo kwa kila Mtanzania kama tunavyodhamiria.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mbunge wa Kongwa kama nilivyojitambulisha mwanzo, kwa kweli kuna hili baa kubwa sana la njaa ambalo linatokea katika nchi yetu na katika nchi jirani. Sisi kule Kongwa tuna soko la Kimataifa la Kibaigwa na kwa kiwango kikubwa ndio tunalisha Dar es Salaam mahindi ya *grade* ya kwanza kabisa tunatoa sisi yenye bei nzuri pale Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mwaka huu hali ni mbaya sana na nilikuwa nawauliza wazee wa miaka mingi kidogo hawakumbuki mwaka unaofanana na huu, hali ni mbaya mpaka sasa hivi mvua haijanyesha inayoeleweka, mahindi hayajaota na sisi Kongwa mwisho wa kupanda mahindi huwa ni kwenye tarehe 20 Januari. Sasa tunayo Februari sehemu kubwa ya Wilaya nzima hata kuota mahindi hayajaota na tarehe za kupanda mahindi zimeshapita kwa hiyo ni mwaka wa ajabu sana ni mwaka mbaya sana.

Katika mgao uliopita wa awamu ya kwanza Kongwa haikupata mgao wowote wa chakula cha njaa, tungeomba sana Serikali katika awamu hii ya pili inayokuja na sisi watukumbuke kwa sababu hali siyo nzuri Kongwa na Mpwapwa. Tunaomba sana takwimu zinazokuja Serikalini ziwe ni za hakika zinazotoa picha ya hali halisi ya matatizo yaliyoko kule vijiji mwaka huu ni wa kipekee sana tusipokuwa makini basi yanaweza yakatoa ambayo hatuyaombei hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, ningeomba sana utaratibu wa takwimu zinazoenda Ofisi ya Waziri Mkuu ziwe ni takwimu za kweli ziisaidie Ofisi ya Waziri Mkuu kujiandaa vizuri kwa ajili ya kukabili baa hili, zikija takwimu ambazo zinaficha ficha mambo zitaifanya Ofisi ya Waziri Mkuu isiweze kuwa na takwimu halisi za kuweza kufanya maandalizi

halisi kwa ajili ya kukabiliana na balaa hili kubwa ambalo tunalipata la hali mbaya sana ya hewa. Pia tunapenda sana kwa mwaka huu hizi takwimu zinapotoka Wilayani basi kila *DC* ampe nakala Mbunge wake au Wabunge wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hizi takwimu zimekuwa siri, Wabunge hawajui tushiriki wote hii hali iliyoko huko inataka tushiriki wote haitaki kikundi fulani cha watu wawe wao ndio wanajua peke yao hapana tushiriki wote ili likiharibika basi sote tuwajibike, tusinyoosheane tu vidole, hapana tuwajibike sisi sote katika jambo hili la njaa na tunajua Serikali yetu ni makini na inachukua hatua za hakika katika suala hili la njaa.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu inayo mipango mizuri na mingi tumeirithi kwa Serikali ya Awamu ya Tatu iwe ni ya kielimu, tumepiga hatua, iwe ni ya kiafya tumepiga hatua, iwe ni ya barabara tumepiga hatua, katika sekta nyingi tumepiga hatua nzuri katika awamu ya tatu na ninaamini sekta hizo zitaendeleza vizuri zaidi katika awamu ya nne tunayoianza. Lakini liko eneo moja ambalo naweza kusema mpaka sasa bado halijafanyiwa kazi vizuri na Mheshimiwa Waziri Mkuu amelieleza hapa na Mheshimiwa Rais alilieleza katika hotuba yake, suala la hifadhi ya mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na mimi nimepata heshima ya kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Mazingira ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inateketea ukitoka Dar es Salaam mpaka Dodoma mpaka Mwanza huko barabarani tu ukiangalia kushoto na kulia jinsi uharibifu wa mazingira unavyotokea huwezi kuamini. Miti inakatwa ovyo kila mahali, moto wakati wa kiangazi kila mahali, kilimo kisichokuwa endelevu kila mahali mtu anaamua anahamia mahali popote pale anaanzisha makazi katikati ya misitu anaanza tu anakata miti ana-*settle* pale hakuna anayemuuliza. Liko tatizo kubwa sana la makazi ya watu, liko tatizo kubwa sana la kuhamahama kwa mifugo na Mheshimiwa Rais alilieleza katika hotuba yake.

Ningependa kuomba sana awamu hii ya Serikali ilitazame kwa kipekee suala la hifadhi ya mazingira, tulipitisha sheria hapa mwaka 2004 ya kusaidia mambo haya, lakini mambo haya hayaendi kwa sheria tu, kama juzi tulisikia sijui kama ni kweli maana baadhi ya vyombo vya habari wamekuwa waongo sana, sijui kama ni kweli tulisikia kwama imepigwa marufuku mkaa.

Mheshimiwa Spika, sasa haya mambo ya mazingira huwezi kwenda kwa marufuku marufuku, lazima u-*balance* maana umeme hakuna ukisema na marufuku mkaa sasa itakuwaje? Kwa hiyo lazima una-*balance* hapa unatoa *incentive* hapa unafanya hivi, hapa unafanya hivi ili mambo yaweze kwenda kwa wakati mmoja, huwezi kusema tu kuanzia leo ni marufuku mbao, hapana lazima watu wapate vitanda, lazima watu wapate viti vya kukalia na ni mbao kwa hiyo, lazima unakwenda kwa ku-*balance*. Lakini ninasema habari ya hifadhi ya mazingira ipewe kipaumbele chake na ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kumteuwa Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, kuwa Waziri katika Wizara hii tutampa ushirikiano mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba Kamati yako hii ipewe fursa ya kutosha ya kuweza kuisaidia Serikali katika *aspect* hii ya hifadhi ya mazingira. Tutakubaliana katika mambo mengine tunaenda vizuri, katika suala la hifadhi ya Mazingira bado kabisa tuko nyuma tunahitaji kuchukua hatua kamilifu ili tuweze kuhakikisha kwamba mazingira yetu yanalindwa na yanahifadhiwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa fursa hii napenda kumalizia kwa kupongeza sana hotuba ya Mheshimiwa Rais na naomba niseme nashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, nikupongeze sana kwa kuchaguliwa kuwa Spika wetu kwa umahiri wako tayari na nina hakika tutakuwa na muda mzuri kwa kipindi chote cha miaka mitano inayokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze na niwashukuru sana wananchi wa Karatu ambao ndio wameniwezesha nisimame hapa saa hizi kwanza kwa kunichagua lakini ya pili kwa kuifanya CCM kuwa Chama cha Upinzani kwa mara ya pili Wilayani Karatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza pia hivyo hivyo kwa kule Bariadi na ninampongeza na ndugu yangu hapa, huu ni utani ndugu zangu wasikasirike kwa sababu siasa ndivyo ilivyo, kama mnavyotunyanyasa hapa na sisi kule Wilayani tunawanyanyasa kule Wilayani. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba niwapongeze kuanzia Mheshimiwa Rais, Waziri Mkuu, Mawaziri na wale wote ambao wamepata nafasi mbalimbali mpaka kwa Wenyeviti wa Kamati mbalimbali kwa ajili ya muda naomba niishie hapo.

Mheshimiwa Spika, naomba baada ya kusema hilo naomba nimpongeze Rais kwa namna ya pekee kwa ubunifu ambao ameuanza, sehemu amesema mwenzangu sihitaji kurudia lakini kwa kweli kwanza lugha aliyokuja nayo si lugha ya ubabe, ni lugha iliyo karibu na watu na sisi sote tumefarijika kwa lugha hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ya pili ni namna ya kufanya kazi yake na hilo pia nimuunganishe na Waziri Mkuu wake nadhani wameanza kwa kasi mpya, nguvu mpya kwa jinsi wanavyoshughulikia kero za wananchi lakini naomba wakati huo huo nitoe tahadhari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unapogusa maslahi ya mtu daima kuna tatizo niwaambie tu kwamba wana kazi nzito kwa sababu nina hakika wanagusa maslahi ya watu, wasifikiri watakuwa na marafiki, watakuwa wanatengeneza maadui. Kwa hiyo, mikakati yao tunaomba kuwahakikishia kwamba sisi kama CHADEMA naomba nitamke kwamba tutaungana nanyi tunapofanya maslahi ya wananchi na tutapambana na yoyote anayehujumu jitihada za aina hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme mambo mawili madogo kwa haraka sana halafu niende kwenye kilichonifanya nisimame. La kwanza ni suala la chakula, suala la chakula kama alivyosema mwenzangu ni tatizo kubwa katika Wilaya yangu ya Karatu, naomba nishukuru Serikali kwamba tayari wameshatupelekea awamu ya kwanza tani karibu 300 na kitu na juzi wametupelekea tani 360 lakini naomba niseme Karatu tuna tatizo kubwa sana, si sasa nadhani tutakuwa na tatizo mpaka mwaka kesho kwa sababu sisi kama hatujapanda mpaka sasa hivi maana yake hatuna uwezekano wa kuvuna hata Julai na Julai tusipovuna hatutavuna mpaka mwaka kesho.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nadhani Serikali iangalie kwa makini hilo watu wa Karatu kwa kawaida hawaambiwi kulima, Mheshimiwa Waziri Mkuu anajua wanalima hata shamba lako wanaweza kuliingilia wakaenda kulilima kama huangalii sasa tatizo si kazi tatizo ni ukame na hili hatuna namna ya kufanya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu watu wako juzi walikuwa Karatu nawashukuru sana kwa kazi waliyofanya, naamini tutafanya kazi nzuri kuwasaidia wananchi wetu. Lakini nitoe tahadhari kwamba chakula kinapopelekwa mara ya mwisho nina taarifa kuna watu hasa wagawaji wanajiwekea wao badala ya kuwajali wananchi.

Naomba hilo likemewe na kwa kuwa Wabunge si wajumbe katika Kamati husika naomba taarifa zetu tunapotoa mzipokee.

Mheshimiwa Spika, la mwisho katika haya ya jumla naomba niseme tu kuhusu ujambazi, nadhani Bunge kama Bunge linatakiwa kukemea na kulaani kwa ukali wote matukio yote ya ujambazi yanayofanyika katika nchi yetu. Maisha ya wananchi yanapotea, mali zinaharibika lakini pia tuna wakati huo huo kero mbalimbali na malalamiko yanayotolewa dhidi ya jeshi la polisi. Kuna askari wetu wazuri sana wanaofanya kazi nadhani tuwapongeze na waendelee na moyo huo kufanya kazi yao, lakini kuna matatizo ya nyenzo ambazo pia zinakosekana nadhani Serikali iangalie kuwapatia polisi nyenzo na motisha zinazostahili. Askari wengi wanafanyakazi katika mazingira magumu sana, mishahara midogo sana, posho ndogo sana, vishawishi vingi sana na ndio maana mara nyingine inawezekana hali inakuwa ni ngumu. Lakini pia inatutia sisi wananchi wasiwasi kwamba silaha nyingi zinazotumika ni silaha ambazo vinginevyo hazina maelezo isipokuwa labda zimetoka kwenye vyombo vyetu vya dola, hili Serikali ni lazima iangalie.

Mheshimiwa Spika, hapa hapa ndani ya Bunge hili miaka kama miwili iliyopita hoja ilitolewa kwamba jeshi letu linahitaji kuwa *overhaul,* linahitaji kufanyiwa kazi upya sina neno la *overhaul,* likaleta utata mkubwa sana kukawa na malumbano kati yetu na polisi na leo tumerudi pale pale ninatoa wito tena jeshi letu linahitaji kuwa *overhauled* matatizo haya yote tuyaangalie kwa upya lakini kauli pia mara nyingine zinazotolewa na viongozi wetu wa vyombo vya ulinzi na usalama hasa polisi hazitusaidii. Nadhani wale wanaokaa sehemu na kufanya jeshi kuwa mali yao sasa ni wakati wa kuwashughulika wako viongozi wa polisi wamejifanya kwamba jeshi la polisi ni la kwao na hata

ukiwapelekea taarifa hawashughulikii zili taarifa na ushahidi ni kituo cha juzi kule buguruni ambako maaskari hawako kituoni saa sita usiku nadhani huu ni ushahidi wa wazi kabisa kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, nirudi sasa kwenye hoja ambayo imenifanya nisimame na kutoa mchango wangu kwa hotuba ya Mheshimiwa Rais. Natumia hotuba ya Rais ukurusa wa 12, 13 bahati mbaya mimi nina kitabu cha kiingereza tu cha Kiswahili sijui kilinipita wapi lakini ninatumia ukurasa wa 12, 13 na nitaenda mbele mpaka kwenye sehemu *Good Governors* mpaka ukurasa wa 22.

Mheshimiwa Spika, kwanza Mheshimiwa Rais ametuwekea mwelekeo mzuri sana katika masula yote ya utawala bora na mwelekeo wa nini kitafanywa na Serikali yake. Kimsingi anayosema Mheshimiwa Rais yanaendana kabisa na matamko mazito yaliyoko ndani ya Katiba yetu na hasa Ibara ya 30 ya katiba, nimeletewa ya Kiswahili nashukuru sana naona wamenipenda hawa sina hakika kama kurasa zinaendana kwa kuwa nimejitaharisha nitajaribu kufanya *reference* kwa yote.

Mheshimiwa Spika, katika katiba yetu haki za binadamu zimewekwa katika nafasi ya kwanza na utawala bora unaendana kimsingi na haki na uhuru wa raia ni wazi kabisa kwamba hakuna uhuru usio na mipaka wala hakuna haki isiyo na mipaka na tunasema haki ya mtu mmoja inaanza pale ya mwenzake inapoishia, nadhani hii ni misingi ya kawaida tu ya kujua haki ya mtu mmoja inaanza wapi na haki ya mtu mwingine inaanzia wapi.

Sasa kwa nini nasema haya? Nasema kwa sababu katika sehemu kubwa sana ya Wilaya yangu hasa maeneo ya Oldeani kule tuna tatizo kubwa sana kwanza mazingira ya Oldeani ni mazingira ya wafanyakazi katika mashamba ya mkataba na katika mashamba haya wananchi wengi walifika kule miaka ya 1950 wakienda kama wafanyakazi wa kuchuma kahawa au vibarua kwenye mashamba ya kahawa wameoa pale, wamezaa, watoto wao wameoa tena wakazaa na hata wajukuu nafikiri nao wamezaa tena pale. Hawa wako wenye mashamba ya mikataba na mashamba ya mikataba kwa kawaida mtu ana-*title* kwa hiyo, ana haki na lile shamba lakini wananchi wakapewa maeneo wakaambiwa lima, wakaambiwa jenga nyumba watajenga.

Mheshimiwa Spika, kumetokea wimbi sasa katika kipindi cha kama miaka miwili ya watu kuondolewa bila utaratibu, mtu aliyejenga kwa miaka yote amefungua shamba amefyeka mpaka likawa shamba leo, kwa ghafla anaambiwa ondoka kesho hutakiwi, ni suala ambalo hata kama mtu ana haki yake, hata kama ana *title* si rahisi mwadamu kuwa *treated* kama kuku. Hili tumelipeleka kwa vyombo vya Serikali, Mkuu wa Wilaya anafahamu, Mkuu wa Mkoa anafahamu, polisi wanafahamu lakini kinachotokea ni kwamba haki za wale watu zimefunikwa. Sisi hatukatai wale watu kuondolewa, hatukatai wale watu kupewa *notice* lakini nadhani utaratibu wa nchi hii pia unajulikana, mwadamu unampa utaratibu, unamwambia ondoka baada ya muda fulani ujiandae uende ukajenge nyumba yako, nyumba ya binadamu haiwezi kuwa kiota cha ndege ukajenge kwa nusu saa.

Mheshimiwa Spika, ninasema hivi kwa sababu sasa hivi ninapoongea nina watu 164 kwenye shamba moja la Edelewesi wako *lockup* na suala ni zito zaidi kwa sababu ukienda polisi wanaingilia kwa namna ambayo inatia wasiwasi labda kwamba kuna rushwa ndani. Mahakama inaingilia kwa namna ambayo kunatia wasiwasi, hakimu amekwenda *site* yeye mwenyewe bila kuagizwa na *section* yoyote ya mahakama ameagiza watu wakamatwe na huyo huyo ndio ameweka watu *lockup* hapa kunaanza kuwa na wasiwasi hakimu wa Oldeani na kuna hakimu mwingine anaitwa Shayo pale Karatu na Msajili wa Mahakama Arusha anajua, Jaji Mfawidhi Arusha anajua, *DC* ambaye ni Mwenyekiti wa Mahakama ya Mwanzo anajua. Lakini huyu ameitwa mpaka kwa Jaji kwa taarifa niliyonayo Mfawidhi lakini anarudi anatamba hata kwenye mabaa kwamba hakuna kitu kitakachonitokea hawawezi kunifanya chochote, taarifa hizi tunaleta, naomba zichukuliwe kama taarifa za kufanyia kazi Serikali kama ilivyo makini nina hakika itazichukua na itazifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, nina malalamiko pia kwamba hata mara nyingine Makatibu Tarafa wanaingilia, ninalalamikiwa Katibu Tarafa mmoja na ninaomba nimtaje kwa jina kwa sababu taarifa hii nimeletewe anaitwa bwana Ole Korosoi, anaenda kwenye mashamba, anawaomba fedha kwa ajili ya kusomesha watoto wake au shida binafsi, akikataliwa anaanza mbinu za kwenda kuchochea mgogoro kati ya tajiri na wafanyakazi wake, hili nalisema kwa sababu linaathiri haki za wananchi. Mheshimiwa Rais ameweka misingi mizuri, iwapo watendaji wetu iwe Mahakama, iwe polisi, iwe watendaji wa Serikali hawatamsaidia Mheshimiwa Rais mbinu zote tunazozungumzia za Mheshimiwa Rais kwa kweli zitakuwa ni maneno kama tulivyozoea huko nyuma.

Mheshimiwa Spika, ni ombi langu, ni ombi la wananchi wa Karatu kwamba tutasikilizwa hatua za haraka zitachukuliwa na Wizara zinazohusika na labda kwa kuwa kuna idara zinazohusika nilitupe kwa Waziri Mkuu kwa sababu ndio kiongozi wa yote hayo. Wananchi wamenipa majina zaidi 200 wameniomba niandae hoja kwa utaratibu tuliofundishwa kwamba tunaweza kuleta hoja maalum kama wananchi wamesaini, sidhani kama kuna haraka ya kufikia hatua hiyo, nina majina nitamkabidhi baadaye Waziri Mkuu nimweleze kitu gani wananchi wanataka. Lakini iwapo itafikia kwamba hakuna kilichofanyika basi nitapeleka hatua hiyo, kwa nini wananchi wanafukuzwa kwa utaratibu huo? Imetokana nadhani kwa tafsiri yangu sina hakika huko nyuma mwaka 2000 Mheshimiwa Rais alifuta hatimiliki ya mashamba mawili. Inaelekea hawa watu ambao wamehoji maeneo makubwa ambayo hayajaendelezwa kwa muda mrefu na wananchi hawana maeneo ya kuishi wameona kwamba Rais yuko kwenye hatua ya kufuta na mengineyo kwa sababu watu wa ardhi walipotembelea mwaka 2000 wali-*identify* heka zaidi ya 10,000 ambazo hazitumiki iko kwenye maeneo ambayo hawawezi kutumia kwa malengo yaliyoko kwenye hatimiliki, wanaona kwamba sasa haya maeneo yatanyang'anywa kwa hiyo wanaamua kuwaondoa wananchi kwa nguvu.

Mheshimiwa Spika, hii ndiyo tafsiri ya haraka tuliyonayo na watu wa ardhi nadhani wakati ule Mheshimiwa Waziri Gideon Cheyo alipokuwepo watu wake walifanyia kazi. Tunamshukuru mashamba mawili yameondolewa hatimiliki yanakabidhiwa sasa kwa wananchi kwa utaratibu kwa sababu Karatu kuna tatizo la ardhi. Lakini hawa wanapofikia hatua hii kwa kuzuia jitihada za Serikali kwanza nadhani ni

kinyume cha utaratibu kwa sababu Serikali imeshapita maeneo hayo sasa wanawaondoa eti kwa sababu wanataka kupanda miti. Nadhani ni kinyume cha utaratibu na ku-*frustrate* jitihada za Serikali katika kuhudumia wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu alitazame, alifanyie kazi, *details* zaidi nitampatia na kabla ya jioni leo nitakuwa nimempelekea *details* ili aweze kuunganisha Wizara zake zinazohusika. Hawa walionyimwa hata *bail* sisi tunaendelea kuzifuatilia ni suala la mahakama, hatutaki kufanya Serikali iingilie, lakini nataka kutamka kwamba hata polisi wameingia kwenye mtego kwa mfano *remove order* imeandikwa Alhamisi iliyopita, kwa kawaida *remove order* inaandikwa kwa siku ile na walikuwa tayari kwenda kuwatoa. Lakini bahati mbaya yule aliyekwenda kuchukua *remove order* kwa kuwa hajui hata kiingereza imeandikwa tarehe ya siku tano mbele, ni utaratibu wa aina yake na ni wa ajabu sana. Watu wanafuatilia kumbe kuna hujuma lakini baadaye tulipochunguza tukakuta hawa watu walitakiwa wakae ndani zaidi ya siku 14 kwa agizo la hakimu mwenyewe. Kwa hiyo, ili kuweza kuunganisha hivyo wameandikiwa *remove order* ya siku tano mbele zaidi na hapo katikati kuna *weekend* vile vile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilidhani kwamba haya mambo yote yanatakiwa kufanyiwa utafiti wa kina Serikali ifanye uchunguzi, mimi Mbunge kazi yangu ni kuwa sauti ya wananchi nimefikisha Serikalini na nadhani Serikali itafanyia kazi kwa sababu Serikali hii naamini ni Serikali sikivu, ni Serikali inayofuatilia haki za wananchi na ni Serikali ambayo italinda haki za watu wote bila kujali nani mkubwa na nani mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, na mimi nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ya hotuba ya Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nami pia ni mara yangu ya kwanza kuchangia hoja hapa ndani Bungeni, naomba niwashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Peramiho kwa kunirudisha hapa Bungeni kwa sura mpya ya Mbunge wa Jimbo la Peramiho.

Ninawashukuru sana na kwa kweli wamenipa ushindi wa kishindo wa asilimia 93, ninawahidi kwamba nitashirikiana vizuri na Serikali hii ya Awamu ya Nne katika kuyafanya yale ambayo tumeyabaini wote kwa pamoja kama ni mahitaji muhimu ya Jimbo hilo la Peramiho Wilaya na Mkoa na hatimaye nchi nzima ya Tanzania, ninaomba niwashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, lakini niendelee kumpongeze sana Rais wetu kwa jinsi alivyoanza utaratibu wake wa kutenda kazi kwa kweli umekuwa ni utaratibu wa mfano na si yeye tu kama walivyosema wenzangu hata mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Peramiho nimpongeze sana pia Mheshimiwa Waziri wetu Mkuu ndugu yetu Edward

Lowassa, kwa jinsi alivyoanza kufanya kazi na hasa katika suala hili la njaa lakini tunaomba tumwambie Mheshimiwa Edward Lowassa, pamoja na tatizo hili la njaa yako mengine ambayo tutayaomba pia aje kuyaangalia kwa karibu kama alivyolifanyia hili ili aweze kuendelea kuonyesha hiyo njia iliyo bora ya kutenda kazi katika Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu hawa mimi naweza kuwafananisha wanafanya kazi kama vile bata aliavyo vifaranga vyake, huwezi kumkuta bata amemtanguliza kifaranga mdogo kuliko wote ndio aonyeshe njia ya kupita, mara zote bata anatangulia yeye na hivyo basi msululu mzima utafuata kwa mtindo ambao umeuonyesha, ni muafaka na njia ambayo itawafikisha wote mahali ambapo ni salama na ndivyo Serikali yetu ilivyoanza kufanya kazi. Kwa hiyo, kwa ujumbe huo ninaomba sana Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri na wengi wote watakaochaguliwa kwenye nafasi mbalimbali wazingatie kuonyesha mifano iliyobora na jamii nzima ya Watanzania ifuate ili tuweze kufika mahali ambapo ni salama, kwa ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya naomba hilo lizingatiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda mimi niseme kwamba hotuba ya Mheshimiwa Rais kwa namna nyingine sisi tungeweza kusema kwa kweli imejitosheleza lakini tungependa kuchukua nafasi hii mimi nafikiri kwanza niseme kwamba ninapochangia hotuba ya Mheshimiwa Rais ninaanza kwa kuiunga mkono na halafu niseme ili iweze kuwa hotuba tekelezaji ama itakayoweza kutekelezwa basi katika maeneo fulani fulani hatuna budi kuchangia na hivyo basi kuifanya hotuba iweze kutekelezeka ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli wenzangu wameanza na *agenda* ya njaa, njaa inayoikabili nchi yetu kwa sasa hivi, sasa mimi naomba niitazame *agenda* hiyo kwa namna tofauti kidogo Jimbo la Peramiho, Songea Vijijini, sisi mvua kule tunamshukuru Mungu zinanyesha, lakini tunapozungumzia suala la kugawa chakula cha njaa sasa hivi bado hatuangalii je, tukishamaliza hiki ambacho tunacho sasa hivi tukakigawa, mwaka huu mwisho na mwaka kesho kwa msimu wa mvua unaoendelea mbele, hali itakuwaje, hivyo mimi nilikuwa nadhani tunaposhughulikia dharura ya ugawaji wa chakula tuyaangalie pia maeneo ambayo yana mvua tukaona Serikali inafanya nini kusudi maeneo yale yazalishe ziada kwa ajili tahadhari ya chakula katika siku zijazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya yanatakiwa kwenda yote sambamba tunapogawa tujenge tahadhari ya siku za mbele, je, tukishamaliza kugawa hiki tulichonacho kuanzia mwaka huu mwezi wa nane, wa tisa na kuendelea msimu wa mavumo na mwakani kabla mvua hazijanyesha tutagawa nini kama hatuchukui tahadhari ya kuzalisha zaidi sasa hivi.

Naomba tuangalie tunawaangaliaje wakulima wa Jimbo la Peramiho wasaidie Taifa kuzalisha hiyo ziada ili waweze kuilisha nchi, pale ambapo itatakiwa tena chakula kingine kiweze kuongezeka kusaidia. Lakini liko suala moja mimi nalishangaa, tunagawa mahindi kama chakula ili kuondoa njaa, lakini tuna watoto wadogo ambao hawali mahindi hayo, ugali, hakuna anayekumbuka hilo. Kuna watoto wako kwenye hatari ya njaa lakini wanahitaji maziwa na surplus ya vitamini mbadala ili na wenyewe waweze

kuondokana na hii njaa ukizungumzia suala la ugali unazungumzia wale wanaoweza kukata matonge, wale wasioweza kukata matonge inakuwaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naomba Serikali ione pia kama kuna uwezekano wa kutengeneza utaratibu wa kugawa maziwa kwa watoto. Asilimia 50 ya watoto chini ya umri wa mwaka mmoja katika nchi yetu wana uzito pungufu ambao unatakiwa uongezewe ziada ili waweze ku-*survive* kwa utaratibu mzuri. Kwa hiyo, nafikiri hilo nalo lizingatiwe.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Rais yako mambo ambayo ameyataja, mimi naweza kusema kama ni amri kumi za utendaji wa kazi katika Serikali yake. Amri yake ya tatu ama muongozo wake wa tatu umezungumzia sana suala la umaskini, malazi na kadhalika.

Mimi naunga mkono kwamba ni hoja ya msingi lakini ninafikiri tunao mpango katika nchi yetu wa kupambana na umaskini na hasa kupambana umaskini wa hali na kipato na waathirika wakubwa wa eneo hilo ni wananchi wanaokaa maeneo ya vijijini na hata wale wananchi wangu wa Jimbo la Peramiho huko Muhukulu na maeneo mengine ya Songea Vijijini kwa kuwa Jimbo langu liko huko Songea vijijini.

Mheshimiwa Spika, lakini bado wananchi hao wana tatizo kubwa la pembejeo zana za kulimia mpaka sasa bado wako katika jembe la mkono, mpaka sasa hivi bado shughuli ya kilimo cha umwagiliaji kule ambako sisi wenzenu tunawaambia kwamba mvua zetu ni za uhakika, halijatiliwa umaanani wa kiasi cha kutosha. Mimi nilikuwa naomba tufanye hivi kwenye Bajeti inayokuja ili hizi amri kumi basi za Mheshimiwa Rais zitekelezeke, naomba zitengwe fedha maalum kwa ajili ya kubadilisha utaratibu wa jembe la mkono kuingia kwenye jembe la kukokotwa na ng’ombe ama majembe ya trekta na yapelekwe basi katika maeneo yanayozalisha chakula kwa wingi katika nchi yetu ya Tanzania. Lakini niseme kwamba pamoja na hayo Wizara inayoshughulika na masoko ione kwamba inakazi ngumu ya kuangalia upya suala zima la masoko ya bidhaa zetu za mazao katika nchi yetu ya Tanzania. Kwa hiyo, huo uwe ni mkakati wa makusudi.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba hiyo Mheshimiwa Rais pia amezungumzia sana suala la miundombinu na nashukuru Waziri aliyepewa dhamana hiyo sasa hivi ni Mheshimiwa Basil Mramba, anakumbuka wakati wa bajeti mwaka jana, tumegombana sana hapa ndani kuhusu *unit bridge* namba mbili ya kuvukia nchi ya Msumbiji ambayo iko katika Jimbo langu kwenye kijiji cha Muhukulu. Ninashukuru Serikali imeshatoa fedha kwa ajili ya barabara na tayari tulishaahidiwa kwamba tutahamishiwa daraja kutoka barabara ya Kibiti - Lindi ambayo inatengenezwa sasa hivi kwa kiwango cha lami, basi daraja lile lingeletwa kule katika kivuko hicho cha Mto Ruvuma ili basi na Mkoa wetu wa Ruvuma na Jimbo la Peramiho lifunguliwe mawasiliano na nchi ya Msumbiji. Naomba sana Mheshimiwa Basil Mramba, alisisitize hilo na alikumbuke vizuri katika meza yake ili liweze kutekelezeka na wananchi wale wa Mkoa wa Ruvuma na hususan Jimbo la Peramiho tuweze kuongeza mapato kwa kutumia mawasiliano hayo mapya.

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Rais amezungumzia utawala bora, hapo mimi naangalia utawala bora katika hali ifuatayo:-

Mheshimiwa Spika, sasa hivi fedha nyingi za Serikali zinapelekwa katika Halmashauri zetu, lakini nimegundua yako matatizo, tunapopitisha Bajeti ya Serikali na kila Halmashauri ikijua kwamba kiasi fulani cha fedha kimekuwa *allocated* kwa ajili ya shughuli mbalimbali kwenye Halmashauri husika, fedha hizo zinachelewa kufika wananchi wanaanzisha shughuli za maendeleo kwa kujitolea kufyatua matofali na shughuli nyingine mbalimbali. Lakini Serikali inachelewa kuteletea fedha hizo matokeo yake nguvu za nchi zinapotea bure, majengo yanabomoka matofali yale ambayo sisi tunatengeneza kwa kutumia udongo yanamong'onyoka na mvua na hivyo kurudisha hizo juhudi nyuma badala ya kupiga hatua ya kwenda mbele, naomba sana Serikali sasa hivi izingatie suala zima la kuhakikisha fedha zilizotengwa katika bajeti zinafika katika maeneo kwa wakati muafaka, ili kuweza kuondokana na tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile suala zima la kuangalia matumizi ya fedha hizo, mara nyingi Mkaguzi Mkuu wa Serikali amekuwa akitoa hapa taarifa ya ubadhirifu wa fedha katika maeneo mbalimbali, lakini hakuna hatua inayochukuliwa, mimi nafikiri kwamba ni wakati muafaka wa kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Rais wetu amezungumzia mahitaji ya makundi maalum, lipo kundi la vijana, vijana ndio wanaoishi katika vijiwe na mimi nashukuru, niwashukuru sana Wabunge wenzangu kwa kunichagua kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo Jamii. Wizara inayoshughulikia masuala ya kazi na ajira na vijana iko katika Kamati yangu, ninaomba tutengeneze mkakati maalumu wa kubadilisha vikundi na vijiwe vya vijana katika maeneo mbalimbali kuwa vikundi vya kiuchumi vitakavyowaletea uwezo wa kujitegemea na kuwaongezea ajira. Hilo ni eneo lingine ambalo kwa kweli linatakiwa liaangaliwe sana na mimi niseme kwamba upo uwezekano wa mitaji kupitia vyama vya akiba na mikopo.

Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itaona vyama hivi vya akiba na mikopo kama chombo muhimu cha kuwakomboa wananchi kwenye suala la mitaji na kuwaletea maendeleo ya haraka. Naomba suala la vyama vya akiba na mikopo lipewe kipaumbele na vyama hivyo viongezewe mitaji na hivyo ndivyo vinavyowafikia wananchi wengi na hata katika maeneo yale yasiyofikika ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa ambazo mimi ninazo, mimi ni Balozi Kiongozi wa kwanza wa Vyama vya Akiba na Mikopo katika nchi yetu ya Tanzania lakini taarifa tulizonazo sasa hivi katika mpango wa vyama vya Akiba na Mikopo nchi yetu ya Tanzania ni ya mwisho katika Bara la Afrika, lakini mimi naamini vyama vya akiba na mikopo vinaweza kuleta ukombozi mkubwa sana na hasa katika suala la kuongeza mitaji na uwezeshaji wa jamii katika ajira na pia katika kujifanyia kazi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, niendelee kusema kwamba mpango wa elimu ya sekondari ni mpango muafaka lakini ninaomba Serikali iangalie upya namna ya utoaji wa ruzuku za ujenzi wa sekondari zetu. Utaratibu wa kupitia shule jirani, kuna maeneo mengine hakuna shule jirani na maeneo yanayojengwa shule sasa hivi kwa hiyo imekuwa ni kazi ngumu, shule hizo mpya zinapojengwa tusubiri fedha mpaka shule jirani iliyoko kilometa 100

ipate fedha ndio ipeleke huko kwenye shule mpya sijui kwa nini tusizitumie Halmshauri zetu katika kutekeleza mpango huu kama ilivyotekelezeka mipango mingine.

Mheshimiwa Spika, nafikiri hilo litaweza kutusaidia sana. Naunga mkono hoja ya mazingira, ni muhimu sana tuhifadhi mazingira yetu na ninaamini ndugu yangu Mheshimiwa Job Ndugai kwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo atatusaidia sana na Waheshimiwa Wabunge kuleta mkakati wa kuhifadhi mazingira katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa mazingira yanaharibika lakini mimi nadhani tuendelee tu kufikiri hivi mbadala wa kutumia nishati ya mkaa inaweza kuwa ni nini, tunawataalam wanaweza wakatufundisha basi kutumia gesi ili kutengeneza umeme wa matumizi ya nyumbani badala ya kuendelea kutegemea matumizi ya mkaa kama chombo pekee cha kuongeza nishati katika matumizi yetu ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, mimi ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais, ninaomba niitakie Serikali yetu ya Awamu ya Nne utekelezaji bora na tunaahidi kwamba tutaipa ushirikiano wa kutosha kabisa ili kweli wananchi matarajio haya waliyonayo kwenye Serikali yao yaweze kutekelezeka na yaweze kutimia, kwa kila mtanzania inawezekana na tunaahidi sisi Wabunge tutashirikiana na wapiga kura wetu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa kupata nafasi ili na mimi niweze kuongea machache kuhusiana na hotuba ya Rais wetu ambayo kwa kweli tunapakapaka tu mafuta yenyewe inajitosheleza tu. *(Makofi)*

Lakini kabla sijasema nalotaka kusema naomba niwashukuru wapiga kura Biharamulo ambao wameniwezesha kurudi tena katika nyumba hii Tukufu. Kwa kweli ilikuwa kazi, mimi sikutarajia, walikuwepo wenzangu walioweza kutoa takrima na usafiri mzuri lakini wakaamua kunichagua mtu anayetembea kwa mguu na kwa baiskeli, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Pia naomba niwashukuru wapigakura wa Bunge hili ambalo wamenipandishia *CV* kwa kunichagua kuwa Mbunge wa kuwakilisha Watanzania kwenye Bunge la Afrika, asanteni sana, sina cha kuwalipa lakini nitawaheshimu.

Naomba sasa na mimi nichangie kidogo kwa kumpongeza Mheshimiwa wetu Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kupata urais kwa kura nyingi ukisema kishindo ni kero, nasema kwa ushindi mkubwa. Lakini pia naweza nikampa pole kwa kukubali kujitishwa mzigo huu ambao mimi nauona ni mkubwa sana, kwa nini nampa pole, kwa kweli kuwa kiongozi mkubwa sana ni kazi kubwa na hasa kwa ninavyomfahamu Mheshimiwa Kikwete, anakubali kwamba lazima atumikie Watanzania kuliko kutumikiwa. Naamini kazi ya Serikali mara nyingi Serikali nyingi za Kiafrika hazijifahamu kwamba ni Serikali na hazijifahamu kwamba ni Serikali na kujua kwamba zinawadhifa mkubwa sana na wajibu kwa wananchi huko nyuma nimeshuhudia Serikali inayoweza ikajitoa kwa wajibu

na kusema kwamba watu wote ni Serikali. Mnamwambia nani mnadai nanyi nyote ni Serikali hakuna nchi ambayo kila mtu anaweza akawa Serikali, hiyo itakuwa ni nchi ya ajabu. Wagiriki walisema kwamba Serikali ni kundi la wananchi waliochaguliwa kwa ajili ya kutawala nchi hiyo, sasa Kabuye na wewe unajiita Serikali, umechaguliwa kwa makusudi hayo? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali lazima ijijue kwamba ni Serikali na imechaguliwa kwa ajili ya kutawala pamoja na kuleta maisha kwa watawaliwa. Kwa kufanya hivyo Serikali nyingi zinawatwisha mizigo watawaliwa kwamba kila kitu wafanye, mimi nikiwa Uingereza kwenye Chuo cha *Oxford,* mimi huwa ni mzungumzaji, vijana walishupaa wakasema tumechoka na ninyi Waafrika mnasema kwamba kutoendelea kwenu kunatokana na sisi kuwakandamiza ninyi hamjui uchawi wa maendeleo yenu. Waafrika tumeumbwa wote tunatokana na Adam na Eva wote tumekuwa duniani pamoja, inakuwaje sisi tunaendelea na ninyi mnabaki hivyo kwa hiyo, uchawi mnao ninyi wenyewe mnasingizia uchawi wakasema kama ni utumwa nchi zote zilienda utumwani lakini yalipokwisha tume-*take off* kama nikutawaliwa Waingereza wakasema tumetawaliwa na Mrumi miaka mitano yalipokwisha tume-*take off* lakini ninyi mnakalia kulilia mambo yalikwisha, sasa mna miaka arobaini na zaidi ya kujitawala, mmefanya nini, mtakalia kutafuta wachawi. *(Makofi)*

Mimi nikajua kwamba ni kweli lazima watutafute wachawi, lakini mwingine akasema kwamba kuongoza watu wakaendelea ni nia na wala sio mifumo ya utawala. Sisi Waingereza tunaendelea pamoja na kuwa kwamba tuko kwenye mfumo wa ufalme ambao watu wengi hawaupendi, sasa nikajua inawezekana nchi yetu haina nia ya kuendeleza watu, na watu wa Afrika wale wafalme wa zamani walizoea kutumikiwa kuliko kutumikia.

Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa ambao mmepewa madaraka sasa hivi, mlijue kwamba mnawajibu wa kutumikia watu na msisubiri kutumikiwa na watu kwa kiwango kidogo sana ndipo tutakapoweza kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali katika kutumikia watu kwanza inawaheshimu na inawapenda na hili ndilo tokeo la kuheshimu haki za binadamu. Je, hali ikoje katika nchi yetu kwa haki za binadamu, ni kweli inawezekana hizi mahakama tunazotengeneza tukaingia wenyewe haiwezekani katika nchi inayoheshimu haki za binadamu mtu akauawa na akachomwa moto kwa kisingizio kwamba ni watu wenye hasira, haiwezekani, halipo duniani. Binadamu anauwawa haki ya binadamu ya msingi ya kwanza ni uhai, uhai wa binadamu ndio msingi wa kwanza wa binadamu lakini uhai wa Watanzania unaondolewa hivi hivi ni wananchi wenye hasira. Unasema unatunza haki za binadamu! Haki ya binadamu ya kwanza ni haki ya kuishi sasa umemuondolea kuishi kwake na bado unamzalilisha utu wake kwa kumuweka moto kama yule anayebabua panya, haya yatatuletea matatizo. Nchi inanyamaza kwani hawa watu wenye hasira ni Mungu, hawawezi wakatafutwa, hilo kwanza tukilimaliza tutakuwa tumejiweka mahali pazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haki ya binadamu ni kitu cha msingi, uhai na utu wa binadamu, tusipofanya hivyo basi tutakuwa hatufanyi kitu kingine lakini vile vile naomba niseme ukishajua kwamba binadamu anastahili kuishi na anastahili heshima basi Serikali yake tukufu ambayo amejiwekea lazima imsaidie kuweza kuishi na ili kuweza kuishi binadamu lazima ajue anapambanaje na mazingira ili aweze kuishi. Kitu cha kumsaidia kupambana na mazingira binadamu ni elimu, elimu iwe ni elimu ya kutosha binadamu kuweza kujua mazingira yake na jinsi ya kupambana nayo ili aweze kuishi na kuendeleza kizazi chake.

Je, sasa elimu tunayopewa Watanzania inakidhi haja hiyo, mbona karibu asilimia kubwa ya Watanzania wamekwenda shule ya msingi, Rwanda na Burundi elimu yao ya msingi inaishia darasa la sita, sisi mpaka darasa la saba, lakini je, hawa watu waliopata hii elimu kweli wamepata wazo la kupambana na mazingira ili waweze kuishi vizuri, mbona umaskini umekithiri? Tujiulize sasa hii elimu tunayowapa watu wetu inatosha? Tunawaandaa kupambana na mazingira ili waweze kuishi na kuendeleza kizazi, tukitoka hapo ndipo tunakwenda kusema kwamba hii elimu, elimu ya msingi haitoshi, ni mjinga ukijenga, unatengeneza msingi halafu unasema mke wangu tuingie kukaa kwenye nyumba, haijaisha huo ni msingi kama kuna mnyama mtaliwa. Sasa Watanzania walio wengi wameishia kwenye elimu ya msingi, ni msingi lazima tuweke matofali kwenye msingi ili Mtanzania aweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni aibu watoto wamejitahidi, wameshinda halafu asilimia 50 wote wanaambiwa rudi nyumbani waishie msingi tu hawawezi kupambana na mazingira na ndio matatizo yanayofanya umaskini ukithiri, hawana uwezo mtu wa darasa la saba ana uwezo wa kujiondolea umaskini kwa asilimia saba na ndio tulionao asilimia saba ndio anayoiweza mtu wa darasa la saba tunasema hao ndio watu tumewapa elimu sisi Afrika tunaongoza, tunaongoza haya sasa wimbi limekuja la sekondari ni kweli kabisa tumeshagundua kwamba msingi si nyumba lazima tuongeze matofali ambayo ni elimu ya sekondari. Hebu sasa tuiangalie nayo yenyewe ikoje ni elimu, ni jina, wengine wanasema ni sekondari za siasa au Kabuye nimejenga sekondari tano kwenye Jimbo langu lakini hizo sekondari zina walimu, sekondari zina maabara, sekondari zina vifaa, majengo yanatosha itakuwa vile vile haya angalau wa *form four* aliyesoma vizuri anaweza akajiondolea umaskini kwa asilimia 25 lakini kama amesoma vibaya si ajabu akajiondolea sawa sawa na asilimia saba kama wa darasa wa saba, ndicho tunachokifanya.

Mheshimiwa Spika, walimu hawapo, vifaa havipo mimi Mkenya mmoja Franc Solekapalo, yeye ni Spika wa Bunge la Kenya nilikuwa naye Uingereza, juzi ananiambia ninyi *you don't have form four, you only have four years* mnachukua watoto, unawalunda pale miaka minne, ni *form four* ya wapi? Hawana elimu ya *form four* na anasema tungelikuwa na mtihani kama ule mlioufanya wakina Kabuye wa *Cambridge* angalau ukawa *East Africa,* Tanzania mngeshika mkia, *is true* sekondari Rais ameamrisha angalau asilimia 50 waingie *form four* lakini walimu unao asilimia 50 ya kuweka pale wakawe pale *four years* halafu unasema *form four* ndio ile ile ya kushindwa kujiondolea umaskini.

Mheshimiwa Spika, naomba sana hili mliangalie hivi kama walimu hawatoshi hivi Kenya ni *English speaker,* Uganda ni *English speaker,* kwa nini katika hali hii tunapokuwa tunaandaa watu wetu tusiombe walimu wakaja kutufundishia wako walimu Kenya na Uganda wakawa wanatushikiashikia *secondary school* zetu na sisi tukawa tunajiandaa, tukishakuwa tayari tunawaambia mkataba umekwisha muende, kuliko kujenga sekondari ya mwalimu mmoja kwa nini tusifanye hivyo?

Mheshimiwa Spika, wako wenzetu mbona wakati tunajitawala tulikuwa hatuna mahakimu si tulileta Wanaigeria, tulipopata mahakimu wetu tuliwaambia ndugu zetu, tunawashukuru sana nenda, kwa nini tusifanye hivyo kuliko kuharibu watoto wetu, kuwaendeleza, mnampotezea muda afadhali apande mgomba kwa hiyo miaka minne kuliko kumweka pale anatoka hata kazi hamna hakuna analoliweza, hawezi akajiajiri haya ni matatizo makubwa sana. *(Makofi)*

Ndugu zangu nawaombeni sana Serikali yetu tukufu sasa iwe na mahali pa kuanzia hivi kweli miaka arobaini hata maji Watanzania hatujapata maji, tunakula matope, hatuna kipaumbele tuanze na hili, hata maji ukienda Biharamulo vijiji vingi havina maji, wanakwenda kilometa sita wanakula tope. Mimi ninapokwenda kwenye kampeni, nakwenda na maji haya ya chupa, lakini unajua maudhui ya watu tunaogombea, usionyeshe kwamba wewe huwezi kunywa maji yao, unaficha ufanya kama unayekwenda pembeni unakwenda kunywa maji yao sasa wakikupa maji unasema sisi wala ndizi huwa hatunywi maji sana, umekwepa kunywa balaa. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, ndugu zangu tuwe na kipaumbele tuseme sasa hili tumelimaliza angalau tunaanza hili, tukifanya hivyo ndugu zangu Waheshimiwa ambao mmejipa huo mzigo ndio maana nikasema Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na timu yake pamoja na kuwapongeza nawapa pole ni kazi kubwa sana, msifurahie kukalia viti vya mbele. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Yesu Kristo, Mitume walimwambia kwamba tunashukuru bwana mizimu inakimbia na kila kitu, lakini akawaambia hilo halitoshi mjisifu wakati mtakapokuta majina yenu Mbinguni yameandikwa na ninyi Waheshimiwa msifurahie viti vya mbele, mfurahi wakati Watanzania watakapokuwa wametokana na huu umaskini.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge kabla sijasitisha shughuli zetu za asubuhi hii nina matangazo machache tu.

Kambi ya Upinzani baadhi yao wameleta maoni kwamba jinsi tulivyopanga ukaaji wao inawazuia kushauriana chama kwa chama, yaani watu wa chama kimoja mathalani CHADEMA wanashindwa kuwasiliana vizuri na kwa karibu kwa sababu wamepangwa mbalimbali. Kwa hiyo, nimemuomba Katibu akae nao ili waelewane watakalolikubali basi Spika ndio ataamua liwe hivyo.

Tangazo la pili nawafahamisha Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim na Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe kwamba maswali yao ambayo hayakujibiwa leo tutayapanga katika orodha ya shughuli za kesho, hii pia ni taarifa kwa Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria.

La tatu saa 11.00 jioni katika uchangiaji nitaanza na Mheshimiwa Esther Nyawazwa, atafuatiwa na Dr. Harrison Mwakyembe ambaye atafuatiwa na Mheshimiwa John Cheyo na baadaye Mheshimiwa Lucy Mayenga, wajiandae kwa sababu hao ndio tutaanza nao kwenye mjadala saa 11.00 jioni.

Sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru sana ili na mimi nipate nafasi ya kuchangia hotuba ya Rais wetu aliyoitoa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu sana kwa kutuwezesha sisi Wabunge tulioingia toka mmwaka 2000 na kuingia tena kwenye Bunge hili mara ya pili kwa kutuwezesha kurudi tena mara ya pili, Mwenyezi Mungu tunaomba tena atuzidishie uhai wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili naomba niwashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Mwanza baada ya Mwenyezi Mungu, kuwapa uwezo wa kunipa kura nyingi na kunirudisha tena Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue sasa nafasi hii kumpongeza Rais wetu wa Chama cha Mapinduzi, Mawaziri wa Chama cha Mapinduzi, Manaibu Waziri na leo hatimaye Wakuu wa Mikoa wameteuliwa tena na Rais wetu mpendwa basi nawatakia kila la kheri kwa kazi yao nzuri hii ya Ari Mpya, Kasi Mpya na Nguvu Mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina imani kubwa sana na Mheshimiwa Rais kwa uteuzi wa viongozi waliopewa, wananchi wote wanawaangalia na sisi Wabunge tunawaangalia viongozi walioteuliwa na Rais wetu. Nina imani kubwa watatekeleza maendeleo ya wananchi na ndicho wanachotaka wananchi.

Mheshimiwa Spika, ili nisisahau kabisa naunga mkono hii hotuba ya Rais kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii kuvipongeza vyombo vya Ulinzi, vyombo hivi vya Ulinzi na Usalama vimetusaidia sana katika hali ya amani na utulivu tulipokuwa katika mchakato wote wa Uchaguzi Mkuu ambao ulipangwa, ukapanguliwa na ukapangwa, ukafanyika.

Kwa hiyo, naomba sana ingawa sasa kuna wimbi la majambazi kazi hii ni kubwa sana kwao, naomba basi kwani ni kazi ngumu tuzidi kuwaombea maana kazi yao hii ngumu wanapambana na watu wasiowajua, wanapambana na watu wenye silaha na wanapambana na watu ambao hawajui ni lini watafanya hicho kitu, niwaombe tu kwamba hawa walioko chini ya Usalama wa Raia wajipe moyo na Mungu atawasaidia na sisi wote tutawaombea.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Rais wetu imegusa maeneo mengi na hasa nyeti ya wananchi kwa matarajio yao ambao sasa kwa awamu hii ya nne ambayo inaendeleza ambayo yamefanywa kwa awamu zote nne ya kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, nitaomba basi ili niungane na Rais wetu kwa kutoa dira ya kitabu chake cha hotuba ndani ya Bunge hili kwa wananchi ili kama utekelezaji ufanyike wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi iliyotolewa mwaka 2005 mwezi Oktoba itekelezeke, nitaomba wapinzani wakubali matokeo.

Mheshimiwa Spika, tusitafute mchawi, mchawi ni maendeleo ya wananchi ndiyo wanachohitaji siyo kutafuta nani amesababisha nani ashinde au Chama hiki kishike madaraka. Wananchi wanachokihitaji sasa hivi ni maendeleo yao hivyo nitaomba sana, ninaomba nitoe ombi kubwa sana kwa wenzetu wapinzani. Huu uhuru wa kisiasa na uhuru wa vyombo vya habari visifanye sasa wananchi ambao wanasubiri maendeleo sisi Wabunge tuwasimamie maendeleo yao wabaki kusoma magazeti ya kurumbana kati ya Serikali, Wabunge na wananchi. Nitaomba basi katika kutoa uhasama huu ambao unaendelea kwa kipindi kirefu basi huu uhuru wa vyombo vya habari pamoja na uhuru wa kisiasa tuuweke pembeni tuangalie maendeleo ya wananchi yanakuwaje.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Rais wetu katika ukurasa wa 47 amezungumzia masuala ya viwanda vidogo vidogo, sana nitazungumzia vijana na wanawake.

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kuwafikia hao walengwa ambao wengi ni wanawake na vijana ndiyo wenye imani kwa mikopo kwenye mabenki au kwenye *NGOs* ambazo zinawapa mikopo nitaomba basi Serikali yetu ya Awamu ya Nne iangalie na hao wanawake wana matumaini makubwa sana na vijana kwamba watafanyiwa nini na katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi imeainisha kabisa kwamba kutakuwa na mkakati maalum wa kuangalia uwezeshwaji wa wanawake na vijana katika uzalishaji na kuboresha mikopo ya riba nafuu.

Mheshimiwa Spika, nitaomba basi Serikali yetu ya Awamu ya Nne ije na mpango wa kudumu wa kuwafanyia nini vijana, kuwafanyia nini wanawake katika kuwaletea mipango ya muda mrefu na siyo ya muda mfupi ambao utawawezesha wawe na matumani kidogo. Tunawapa mikopo ya nafuu kwa kiwango gani na tuwatafutie masoko unapowapa elimu halafu wanazalisha kwa wingi basi nafikiri Serikali yetu ije na mipango na mikakati ya kuhakikisha hao watu watakapozalisha watakapopata elimu ambayo watakuwa wameeleweshwa watapata wapi masoko ya kuuza bidhaa zao.

Mheshimiwa Spika, ili wananchi washiriki katika kukuza uchumi wa Taifa letu, nitaomba sana washirikishwe wao wenyewe kama mwananchi utamtenga pembeni ukawa wewe ndiye unaongoza tu sijui kama kutakuwa na mafanikio yoyote basi naomba Serikali yetu ya Awamu ya Nne katika ukurasa wa 47 kwa sababu Rais wetu ameelezea tumewashirikisha vipi katika Sekta za Utalii, katika Hifadhi za Mazingira ambayo ni kero zaidi ambayo inawagusa zaidi wananchi waliopo huko vijijini.

Mheshimiwa Spika, lakini tutawashirikisha vipi katika kupata ajira, nashukuru Serikali yetu ya Awamu ya Nne inaeleza wazi ajira siyo ya mezani ofisini ni ajira ambayo kila mtu ana mikono miwili, ana macho miwili, ana masikio mawili atajiajiri yeye mwenyewe kwa kusaidiwa na Serikali yake ya Awamu ya Nne ili kuhakikisha kwamba na yeye anashiriki katika kukuza uchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nasisitiza tu kwamba washirikishwe wananchi wenyewe katika kuhakikisha kwamba ajira watakazozipata basi watakuwa wamepewa elimu ya kutosha, watakuwa wameelekezwa jinsi ya kufanya na maafisa wetu ambao wanashiriki na kuelimisha wananchi basi wafike katika maeneo ya wananchi walioko huko vijijini.

Mheshimiwa Spika, naomba tena na mimi niungane na Rais wetu katika ukurasa wa 54 katika hotuba ya Rais wetu, nimempongeza sana Rais wangu kwa sababu ameonyesha dhahiri, ni wangu kwa sababu mimi ni Mbunge wa Chama cha Mapinduzi ni wangu ni wa Serikali yangu nampongeza sana alivyozungumza suala la kuzungumza kiswahili na ameonyesha mfano juzi alipokuwa Khartoum, Sudan alizungumza kiswahili. Kwa hiyo nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuonyesha mfano. Nitaomba sasa na wataalam wetu wanapoanza kuandaa Miswada, wanapoandaa Mikataba au Maazimio yoyote hata uanzishaji wa shule za sekondari za *academic* basi ziitwe kwa majina ya kiswahili ili tuwe na kumbukumbu nzuri kwa Watanzania kama kweli tunataka kumuenzi Rais wetu wa Chama cha Mapinduzi kwamba ameenzi kiswahili basi na sisi tukitumie kiswahili kama ndiyo lugha yetu ambayo tunashawishi na nchi nyingine za Afrika zitumie lugha hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru sana ndugu zetu wa Mamlaka ya Mapato. Nchi hii inawachukulia *TRA* kwamba ni Zakayo, kila mtu aliyesoma katika Biblia Zakayo anamjua ni nani, Zakayo alikuwa mtoza ushuru kwa hiyo, niwaombe sana ndugu zetu wa *TRA* tunawategemea sana katika Taifa letu katika kutukusanyia mapato na ninyi ndiyo mmetuonyesha dira nzuri ya kuhakikisha kwamba tunakusanya mapato yetu wenyewe na tunaweza kuendeleza miundombinu yetu.

Mheshimiwa Spika, basi naomba tu Mungu atawasamehe kwa makosa ya kukusanya mapato mnavyokimbizana na wakwepaji lakini tunawapa nguvu kwamba ninyi mtaweza kutunusuru katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, lakini itasikitisha unaona wenzetu Mamlaka ya Mapato inajitahidi kukusanya mapato kutoka kwenye nyenzo mbalimbali, unakuta watu wengine wanatumia matumizi mabaya sana, nitatoa mfano Mheshimiwa Rais bahati nzuri ametoa

mfano wa masurufu inakuwaje mtu anapewa masurufu anakaa mwezi mmoja amekwenda safari amerudi kutoka safari anashindwa ku-*retire* masurufu kwa sababu gani.

Kwa hiyo, nitaomba katika ukaguzi wa mahesabu yote tuangalie basi hata hayo masurufu wenzetu tunawapa nguvu za kukusanya mapato lakini watu wengine wanataka kutumia fedha za nchi hii kwa kuchengachenga hiyo itatufikisha mahali ambapo inakatisha tamaa kwa wenzetu wa Mamlaka ya Mapato. Nitaomba basi hao wakaguzi wanapokagua mahesabu ya wenzetu basi waangalie na hawa hilo ni fungu moja ambalo nimeliangalia kwa sababu masurufu ni wewe umepewa hela umetumia mafuta urudishe risiti za mafuta. Sasa mwenzio atakuwa anakusanya pesa halafu wewe unazitumia bila utaratibu wa kimahesabu.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa nimelenga kwa hayo machache ambayo Rais wetu ametupa mwongozo mzuri wa kufanyia kazi kwa kufuata Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana na ninaunga mkono tena kwa asilimia mia kwa mia hii hotuba ya Rais wetu. Ahsante sana.*(Makofi)*

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuwashukuru wapiga kura wote wa Kyela kwa kuniunga mkono bila kigugumizi toka mwanzo wa mchakato wa uchaguzi hadi mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naelewa ni kitu gani kilichokuwa kinawasukuma namna hiyo. Ni kiu ya maendeleo. Na mimi kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa wapiga kura wao sitawaangusha.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa niaba ya wapiga kura hao wa Kyela nikupongeze wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Naibu Spika kwa ushindi mkubwa mlioupata katika Majimbo yenu ya Uchaguzi na vile vile ndani ya Bunge hili na kuweza kuliongoza kwa kipindi cha miaka mitano ijayo hadi mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, naomba vile vile nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na vile vile Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Aman Abeid Karume, kwa ushindi mkubwa walioupata katika Uchaguzi Mkuu uliopita.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, nawapongeza Wabunge wote walioteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Wabunge, kuwa ma-*regional commissioner,* kuwa Mawaziri, Naibu Mawaziri ambao watamsaidia Mheshimiwa Rais katika kuendesha Serikali ya Awamu ya Nne ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Lakini pongezi maalumu zimuendee Mheshimiwa Edward Lowassa, Mbunge wa Monduli kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri Mkuu wa Tanzania na uteuzi wake kuungwa mkono kwa kishindo na Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waswahili wanasema nyota njema huonekana toka asubuhi, kwa sisi baadhi yetu ambao tulipata bahati ya kwenda shule na Mheshimiwa Waziri Mkuu bado tuna kumbukumbu za nyota ya uongozi iking'ara kwa Mheshimiwa Edward Lowassa tangu enzi hizo. Tunachomtakia ni kumwombea neema, kumwombea baraka na afya njema aweze kuzimudu kazi zake nzito kwa ufanisi mwema. Ahsante.

Mheshimiwa Spika, sijawasahau Wabunge wenzangu wote tuliomo humu. Tupongezane jamani kwa kupata ridhaa ya wananchi katika Majimbo yetu na vile vile akina mama wa Viti Maalumu hasa CCM, wao mchakato wao ni mgumu kweli kweli. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na muda kuwa mfupi nitagusia masuala mawili au matatu katika hotuba muhimu ya Mheshimiwa Rais.

La kwanza, ni suala la mpasuko wa kisiasa uliopo kati ya Unguja na Pemba, mpasuko ambao Mheshimiwa Rais ameuongelea kwa hisia kali na vile vile kwa ujasiri mkubwa.

Mheshimiwa Spika, mimi naona hatuna budi kumpa moyo Mheshimiwa Rais kuhusu suala hili linaloitia dosari Tanzania ili tupate ufumbuzi wa kudumu. Mimi naona Mheshimiwa Rais kutokana na hotuba yake tayari ameonyesha utashi wa hali ya juu wa kisiasa na vile vile ari inayostahili ambayo nina uhakika itatufikisha katika kutatua tatizo hili. Pengine wamwangushe viongozi wa kisiasa ambao wanaweka mbele maslahi yao ya kibinafsi na vile vile wanaweka pembeni maslahi ya Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, naongea kutokana na uzoefu wangu kama Mjumbe wa Kamati ya Tume ya Rais ya Muafaka. Wenzangu wengine wawili wa *CUF* wako humu humu ndani. Tukiweka siasa pembeni, nataka kuthibitisha hapa mbele yenu kwamba muafaka kati ya CCM na *CUF* tumeutekeleza kwa kiasi kikubwa. Lakini yale machache ambayo hatukuweza kuyatekeleza ndiyo ambayo yanaendeleza huo mpasuko.

Mheshimiwa Spika, tulikwama suala la pesa kuwafidia wale walioathirika na ghasia za vurugu za kisiasa za Zanzibar na yote ni kwa sababu wafadhili walijitokeza mwanzoni kwamba wangetoa hiyo fidia lakini ulipofika muda wa fidia wakaingia mitini na mzee mzima Jumuiya ya Madola. Mimi naelewa kwa nini walifanya hivyo. Walifanya hivyo kwa sababu hawakuamini kwamba sisi Waafrika tena Watanzania tungeweza tukafikia muafaka unaotekelezeka sisi wenyewe. Ndiyo maana wakaanza kujitolea ahadi hovyo. Tukakubaliana, tukafika mpaka kulipa na fidia. Kuwaambia, wakaingia mitini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa ari yake mpya ya kutatua tatizo hili, kwamba gharama hizo za fidia ambazo wahisani wamezikwepa tuzibebe sisi wenyewe Watanzania. Tuzilipe kwani uzoefu umetuonyesha

kwamba gharama za kuepusha shari daima ni nafuu kuliko gharama za kuzima shari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili ni kwamba mbali na kubeba gharama hizo nilikuwa namwomba Mheshimiwa Rais amalizie pale ambapo sisi tulishindwa kupamalizia napo ni kuunda Kamati ya Pamoja ya Ushirikiano ya Vyama inaitwa *Inter Party Committee* ambayo vyama vyote badala ya CCM na *CUF* peke yao vitahusishwa na ningeomba hiyo Kamati ipewe kazi mbili za mwanzo kumalizia yale ambayo hatukuyamalizia sisi hasa ya fidia na pili kuhakikisha kwamba mfumo tuliourithi wa uchaguzi Zanzibar kutoka Uingereza wa *the winner takes all* au mfumo wa *First Past the Post,* tuuache sasa, hautusaidii. Unaleta ushindani usio na maana, ushindani wa kufa na kupona. Tu-*adopt* mfumo wa *proportional representation* utatuokoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niliongelee kwa haraka suala la pili ambalo Mheshimiwa Rais aliliongelea. Mheshimiwa Rais alilinganisha nishati na chembe za damu mwilini. Mimi nadhani alipatia kwani bila nishati ya uhakika hatuna maendeleo ya uhakika. Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 inaeleza kwamba kufikia mwaka 2025 Tanzania itakuwa *a semi industrialized developed country* yaani nchi ya kati ya maendeleo iliyoendelea ya viwanda.

Mimi nimeziangalia nchi ambazo tayari zimeshafikia hatua hiyo. Lakini katika nchi hizo utaona kwamba kigezo kikubwa kilichowafanya wafike hapo na kubakia hapo ni matumizi ya nishati ya uhakika. Sasa leo hii sisi Watanzania *per capita consuption* ya nishati ni *watt 24* lakini wenzetu waliofikia huko *per capita consuption* ya *watt 388.* Kwa hiyo, ina maana mwaka 2025 itabidi kila Mtanzania hapa atumie angalau wastani wa umeme wa *watt 388* na kufikia mwaka 2025 wataalamu wanatuambia idadi ya watu hapa Tanzania itafikia pengine milioni zaidi ya 50. Kwa hiyo, tutahitaji umeme zaidi kwa wanaojua hesabu *megawatt 20,000.*

Mheshimiwa Spika, sisi nafikiri hatujafikia hata *megawatt* elfu moja. Swali kubwa ni je, tutapata wapi vyanzo vya uhakika vya nishati? Mimi nafikiri picha ya dunia inajieleza yenyewe kwamba 76% ya nishati duniani inatokana na gesi, mafuta na vile vile makaa ya mawe. Hii *hydro* tunayoitumia sana na kuwa tegemezi hapa Tanzania ni 5% mpaka 6% tu dunia nzima. Kwa hiyo, naungana kabisa na Mheshimiwa Rais anaposema sasa tuangalie upande wa makaa ya mawe Mchuchuma na sehemu nyingine.

Mheshimiwa Spika, Mungu ametupa makaa ya mawe siyo Mchuchuma tu, yapo vile vile Liganga anakotoka Profesa Mwalyosi na huko Kiwira. Makaa yapo tu juu juu yanalilia kuvunwa, hebu tuyavune sasa tuwe na uhakika wa nishati ya uhakika. Tuna *deposit* alisema Waziri juzi za makaa ya mawe ya zaidi ya tani bilioni 1.2.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa neno fupi sana, vyombo vya habari ni viungo muhimu sana kati yetu na wananchi. Nasema hivyo kwa sababu vyombo vya habari vinatafuta, vinakusanya na kusambaza taarifa na taarifa siyo tu ni mali, vile vile ni nguvu ya pekee. Lakini vyombo vya habari vikiwa mikononi mwa watu ambao hawana uadilifu, watu ambao hawaijui taaluma yenyewe ilivyo, ni sawa na kumpa kichaa panga.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naeleza haya kwa vile mimi siyo tu mwanasheria vile vile ni mwandishi wa habari kitaaluma. Yanayotokea hapa yananiuma kweli kweli hasa ya upotoshaji wa habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu Rais wa awamu iliyopita alinipa kazi ya kusimamia ukuaji wa hii taaluma kwa kuwasomesha vijana. Nilikuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo cha Uandishi wa Habari, Chuo ambacho tumekilea kufikia mwaka 2003 tukakifanya kuwa Taasisi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ili waandishi wetu wasipate tu *Certificate* na *Diploma* bali wapate pia *Ph.D.* kipo pale.

Mheshimiwa Spika, lakini leo naumia moyo kwa nini? Wabunge wako kwenye semina, waandishi wa habari wenzangu wanautangazia umma kwamba ndiyo Wabunge wako kule wanatunga sheria kwa kupitia semina. Unapotoa *interpretation* kwamba wanafikia maamuzi ina maana tunatunga sheria hata kupitia semina! Mbunge mmoja tu kati ya Wabunge 324 anasema haoni sababu Mbunge hapigiwi saluti, kesho yake waandishi wa habari wenzangu wanatoa *bold headlines;* "Wabunge sasa walilia kupigiwa saluti." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mbunge mmoja tu anasema yeye angetamani kipindi cha rais kiwe miaka saba. Hata Wabunge iwe miaka saba. Hajaungwa mkono na mtu mwingine, lakini kesho taarifa kubwa magazetini zinasema kwamba, "Wabunge sasa wanataka kujiendeleza kwenye nafasi zao wanataka sasa miaka saba." Nchi nzima inatuona watu wa ajabu.

Mheshimiwa Spika, nilitaka tu niseme kwamba huu si uandishi wa habari ila ni uhandisi wa habari, tunapika habari na wanaofanya haya ni waandishi wachache tu wanawaharibia jina waandishi wazuri wengi ambao nimekwenda nao shule ni waandishi wazuri sana. Wakati wa semina Wabunge watatu waadilifu kweli tena tunaowaamini sana walikuwa wanajenga hoja kwamba Mbunge akiwa kwenye jimbo lake huyo Mbunge kila msiba lazima achangie. Mtoto yeyote ambaye suruali imechanika au kaptula ya shule hatatoka kijiji cha mbali basi anakuja kwa Mbunge. Mgonjwa yeyote itabidi apelekwe kwa Mbunge kwani gari la Mbunge ndiyo *ambulance.* Hakuna anayechangia mafuta, kila huduma ya maendeleo Mbunge lazima achangie. Walikuwa wanahoji, sasa jamani na mshahara wa shilingi milioni 1.2 yote haya Mbunge anabeba. *(Makofi)*

Kwa nini tusiige utaratibu wa wenzetu wa Kenya na Uganda ambao wana kitu kinaitwa *Constituency Development Fund?* Sasa pengine alikuwa nadhani ni Mheshimiwa William Shellukindo aliongea kwa kiingereza hawakuelewa sasa ikawa hawa Wabunge wanataka mshahara zaidi, tumepakwa matope nchi nzima. Tatizo ni nini? Unawa-*quote* Wabunge *out of context.* Kwa mwandishi wa habari, *this is a crime.* *(Makofi)*

Tatizo ni nini? Tatizo linaweza kweli kuwa ni la kisiasa lakini vile vile linaweza kuwa ni la kibiashara. Unajua unapoandika *sensational news* ndiyo watu wanakimbilia kununua magazeti kuna ushindani sasa hivi lakini mimi naliona tatizo letu kubwa kwa

vyombo vyetu vya habari sasa hivi ni *UPE, UPE* kirefu chake ni Uandishi Pasipo Elimu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Rais wa Uganda Yoweri Museveni alilaaniwa na dunia nzima alipoamua na kusema sasa nimechoka na upotoshaji. Hakuna kuandika habari bila *Degree* ya Chuo Kikuu cha Makerere. Watu wakasema huyu ni dikteta. Sasa tusifikishwe hapo. Ninachosema tu, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge tunao wajibu wa kuwasaidia waandishi wa habari wapate elimu zaidi.

Naomba pengine kuanzia Bajeti ya mwaka 2006/2007 Waziri anayehusika aweke angalau *scholarship* kama 20 kila mwaka, hata 10 kwa ajili ya waandishi wetu wakasome Chuo Kikuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tusipofanya hivyo hawa jamaa wataendelea kutu *quote out of context* mpaka dunia nzima itatuona sisi watu wa ajabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa sababu muda umekwisha kwa kusema naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ikiwa ni mara yangu ya kwanza kuzungumza katika Bunge lako Tukufu napenda kuchukua fursa hii kukupongeza kwa nafasi uliyoipata lakini kadhalika napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa nafasi hiyo aliyoipata kwa ushindi wa kishindo kwa kukubaliwa kwa kweli kwa asilimia kubwa na Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kadhalika napenda pia kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliopita katika Majimbo yao pamoja na wale wa Viti Maalum kwa kuchaguliwa katika Mikoa yao lakini vile vile ningependa kuchukua fursa hii kuwashukuru Jumuiya ya Vijana ambao kwa kweli wao ndiyo walioweza kunisaidia mpaka kufika hapa nilipo na hasa kwa nafasi ya pekee maadamu Mwenyekiti wangu yumo humu humu Mheshimiwa Dr. Emmanuel Nchimbi, Naibu Waziri wa Habari, basi na yeye apate hongera hizi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikua nataka kuzungumzia suala la usalama katika mabenki. Kwanza kabisa ninaipongeza hotuba ya Rais kwani ilikuwa ni hotuba nzuri iliyojitosheleza. Katika hotuba yake Mheshimiwa Rais ameonyesha kusikitishwa kwake na hali halisi iliyopo hivi sasa ya vitendo vya kihalifu katika mabenki yetu na taasisi za fedha.

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho kimenisukuma leo hii kutoa mchango wangu ni kujiuliza hivi ni kwa nini hivi vitendo vya kihalifu vinaendelea katika mabenki yetu?

Mheshimiwa Spika, lakini katika kuangalia hili napenda kuzungumzia suala hili la kuibuka ghafla kwa huu uhalifu wa kutumia silaha katika taasisi za fedha. Hapo zamani katika miaka ya nyuma uhalifu katika taasisi za fedha walikuwa wanawatumia wafanyakazi au watumishi katika sehemu mbalimbali ili kuweza kupata hizo fedha

ambazo walikuwa wanazitaka, lakini sasa hivi uhalifu huu umeingia katika sura mpya ya kutumia silaha baada ya kuingia mtandao mpya wa sayansi na teknoloji kwa hiyo, imekuwa ni vigumu wao kuweza kuingia katika hizi taasisi za fedha kwa hiyo, wameamua kuingia na utaratibu mpya wa kutumia silaha kwa sababu wanajua wakichukua bastola wakiingia pale wakiwatishia watu laleni chini watalala na ataweza kufanya uhalifu huo.

Mheshimiwa Spika, lakini katika Tanzania kuna mabenki mengi, kuna taasisi nyingi za fedha mimi ambacho najiuliza ni kwa nini basi imetokea kwamba wizi huu umekuwa unatokea katika benki moja zaidi ya mara mbili au tatu. Nikitolea mfano katika benki ya *NBC* ndiyo benki inayoongoza kuweza kufanyiwa uhalifu yaani kwa maana kwamba majambazi kuingia na kuvamia na kuiba.

Tatizo la kuiba linaweza likatokea sehemu nyingine yoyote, lakini kwa nini katika Benki hii inatokea mara tatu? Kwa kweli kama tatizo linatokea mara moja unaweza ukasema ni bahati mbaya, likitokea mara ya pili sijui utatoa maelezo gani. Lakini zaidi ya mara mbili kwa kweli inabidi iangaliwe upya, kwa sababu biashara yoyote kama mtu anaweza akaamua kuifanya, anaamua kufanya biashara kubwa kulingana na uwezo alionao. Kama mtu ameamua kufanya biashara kubwa ya kufungua kitu kikubwa kama Benki ambacho kinaingiza fedha zetu nyingi za walipa kodi, fedha za wananchi kama hana uwezo wa kuweza kusimamia hali halisi ya ulinzi na usalama wa mali pamoja na maisha ya wale wafanyakazi kwa kweli hastahili.

Mheshimiwa Spika, vile vile pia hili suala naliangalia katika sura nyingine. Hakuna biashara kubwa ambayo mtu ataingia kuifanya kama atakuwa hana Bima. Sasa Mheshimiwa Waziri wa Fedha anaweza kuangalia upya kwamba inawezekana basi hii Benki au hizi Taasisi sasa hivi umefumka huu mtindo mpya kwamba labda watu baada ya kuibiwa au kufanyiwa uhalifu kuna kitu wanachonufaika nacho ndani yake. Kwa sababu wananchi wanajiuliza maswali mengi kwamba inakuwaje hiki kitu kinatokea hapo tu bila majibu. Kwa taarifa nilizonazo ni kwamba katika hiyo Benki wamekuwa hawataki ulinzi wa Polisi kwamba wanasema Polisi wakiingia pale wakiwa wameshika bunduki watawatisha wananchi. Hii kwa kweli inakuwa sio sababu ya msingi kwa sababu hivi vitu pale kuna maisha ya watu maana achilia mbali hizo fedha lakini kuna maisha ya watu. Watu wanaweza wakaathirika, wakauawa na kufanyiwa vitendo vingine vibaya lakini hii Benki nashindwa kuielewa kwa nini wanakuwa wanaona kwamba kuweka hao Polisi itachukuliwa kama ni kuwatisha wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika sababu ambazo zimekuwa zikielezewa kuhusu huu uhalifu katika hizi taasisi za fedha ni kwamba wafanyakazi wamekuwa wakishirikiana na majambazi. Hili ningependa liangaliwe upya kwa sababu sasa hivi ukizungumzia hili suala la wafanyakazi hawa inabidi ufanyiwe utaratibu ili waweze kuandaliwa upya kwamba waliingia ingia vipi. Kwa sababu hivi sasa hapa Tanzania umeibuka kama ni mtindo au ni tabia kwamba sasa hivi ukienda kuomba kazi sehemu nyingine yoyote kama huna refa wewe huwezi kupata. Kuna vijana wengi sana ambao wanamaliza vyuo wana uwezo mkubwa sana wa kuweza kufanya hizo kazi lakini hawakubaliwi kwenda kufanya hizo kazi kama mtu hana refa. Sasa kwa mtu mwingine ambaye amefaulu vizuri ana

uwezo mkubwa sana wa kuweza kufanya kazi anaambiwa kwamba lazima upate refa. Matokeo yake tumejikuta katika sehemu nyingi kwamba mtu anaingiza watu ambao anawajua aidha, ndugu yake au jamaa au mtoto wa rafiki na kadhalika. Hiyo inakuwa haina tatizo sana ni tatizo kwa upande mwingine inaweza ikawa pia sio tatizo kwa sababu tunaambiwa inabidi tugawane kidogo tulichonacho kwamba hizo nafasi za kazi zilizopo ni hizo hizo. Kama ni Mabenki ni hayo hayo, kama ni nchi ni hiyo hiyo moja kwa hiyo huwezi kusema ni mtoto wa fulani basi aruhusiwe kufanya kazi sehemu fulani. Lakini kwa kweli hii inatakiwa uiangalie kwamba wale watu wanaoingizwa katika hizo sehemu ni watu wa namna gani. Kwa sababu hatma yake inakuwa kwamba katika hizo sehemu wafanyakazi kwa sababu wameingia kwa njia ya kujuana na njia ya kuweza kufahamiana na watu kwa njia ya kinyemela, njia ya mlango wa nyuma kwa sababu tu ameingizwa na mtu fulani hata kama akifanya kitendo cha uhalifu pale kuna uwezekano mkubwa sana wa yeye kutoweza kuchukuliwa hatua kama za kufukuzwa au hatua nyingine zozote kwa sababu tu aliingia kwa kupitia mgongo wa mtu fulani.

Mheshimiwa Spika, naomba katika hizi taasisi za fedha wakati wanafanya aidha, kama ni ukaguzi au ni uangalizi upya wa hizi taasisi za fedha katika kuangalia zile sababu zinazopelekea haya matatizo kuweza kuendeleza basi waweze pia tuliangalie hili suala la wafanyakazi ambao sio waaminifu. Kwa sababu katika kila Benki unaambiwa kwamba wafanyakazi wawili watatu wamechukuliwa wanahojiwa. Lakini hii tabia itaendelea mpaka lini.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuzungumzia Benki Kuu yetu *BOT*. *BOT* katika suala hili hawana budi kuwa na majibu ya kuweza kuwajibu wananchi. Kwa sababu Benki Kuu ndiyo inayotoa leseni katika Mabenki yetu na taasisi zote za fedha hapa nchini. Sasa endapo vitendo kama hivi vinaendelea na kitu kikubwa zaidi ambacho kwa kweli kinaudhi na kinauma ni kwamba taasisi kwa mfano kama hizi *Bureau de Change* zikifunguliwa katika mazingira ambayo hayaridhishi. Tutaendelea kuwalaumu Polisi kwamba wanachelewa kufika kwenye matukio, Polisi sijui wanafanya hivi lakini *BOT* hawajafanya upembuzi yakinifu kuweza kuangalia hizi *Bureau dE Change* ambazo watu wanakwenda wanatoka shilingi milioni kumi anapata leseni zinafunguliwa wapi. Kwa sababu hivi sasa katika jiji la Dar es Salaam imeibuka kwamba mtu akiwa na fedha shilingi milioni kumi au kumi na tano na kadhalika anakwenda anafungua *Bureau de Change.* Lakini hizi *Bureau de Change* zimeenea mpaka Kariakoo uchochoroni huko. Ukiangalia hakuna *CTTV Cameras,* hakuna *alarm* hakuna mifumo yoyote ya kiusalama ambayo unaweza kusema kwamba hii mifumo itasaidia. Matokeo yake watu wamekuwa wamekufa kila siku katika hayo maeneo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda kwanza hii Benki Kuu iweze kuangalia upya hili suala la utoaji wa leseni za kufungua biashara ya hizi *Bureau de Change.* Kwa sababu mtu akiwa na fedha leo mimi Lucy Mayenga, nimekaa hapa nimepata fedha zangu za gari nimeamua sinunui gari, gari yangu niliyonayo inanitosha nakwenda kufungua *Bureau de Change* nikifungua *Bureau de Change* nikimaliza unamweka mtu hapo nikimaliza akija anauawa unasema mambo mengine yanaendelea, aidha tena jamani basi ndiyo naenda kwenye Bima nakwenda kurudishiwa fedha yangu. Kwa hiyo hiki kitu inawezekana hakiwaumi watu kwa sababu wanaodhurika sio wao yeye amefungua ofisi amecha pale wanaohusika na kuumia ni wafanyakazi. Napenda kuchangia katika hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia suala lingine ambalo napenda kulichangia ni kuhusu suala la Polisi. Kwa kweli Polisi wamekuwa wanalaumiwa kila kukicha kwamba Polisi hawafanyi kazi inavyopaswa. Lawama zimekuwa ni nyingi sana, lakini mimi katika utaratibu mzima wa utendaji kazi wa Polisi ningependa kuchangia mambo yafuatayo.

Mheshimiwa Spika, kwanza ninaunga mkono suala la ubadilishaji wa muundo wa Jeshi la Polisi. Lakini vile vile lawama nyingi zisiendelee kumiminiwa Polisi wakaendelea kulaumiwa tu bila ya kujiuliza kwamba hawa Polisi wanalaumiwa lakini wanalaumiwa sababu nyingine zinazofanya washindwe kufanya kazi ni zipi. Kwa sababu mimi nakumbuka kuna Meya mmoja katika jimbo la New York anaitwa Juliana, mama mmoja yuko *strong* sana. Yeye alikuwa anawalaumu sana Polisi kila kukicha Polisi hawafanyi kazi vitendo vya kihalifu vinaongezeka. Lakini baadaye watu wakamwambia hebu kaa na hawa Polisi uwaulize tatizo lao ni nini.

Baada ya kukaa na wale Polisi, Polisi wakamwambia sisi hatuna magari, hatuna vitendea kazi, hatuna silaha na kadhalika tunahitaji vitu kama hivyo ili tuweze kufanya kazi vizuri. Wakakaa naye wakapewa vitendea kazi, magari na vitu vingine vyote muhimu ambavyo vinatakiwa katika kufanya kazi bora. Wakapewa hivyo vifaa wakafanya kazi baada ya hapo akawauliza tatizo sasa ni nini. Ina maana hapa tatizo labda ni la mtu binafsi aidha watu wamekaa muda mrefu wanatakiwa wahamishwe.

Mheshimiwa Spika, mimi naishauri Serikali kwamba suala la Polisi liweze kuangaliwa kwa maana ya kwamba Waheshimiwa Wabunge tuunge mkono Bajeti ya Wizara ya Usalama wa Raia iwe ni kubwa zaidi ili Polisi waweze kupata vitendea kazi wanavyovitaka maana na wao pia ni binadamu. Wanaposema kwamba tunashindwa kufika sehemu fulani kwa sababu hatuna gari ni kitu cha msingi ni hoja ya msingi na ni sababu nzito ya msingi.

Naomba Polisi wapewe vitendea kazi ili waweze kufanya kazi zao vizuri na lawama zipungue kwa sababu na wao pia ni binadamu hata kwa mtu ambaye anajitolea kwa kiasi kikubwa kufanya kazi anaweza akavunjika moyo kwa sababu anaona mimi nafanya kazi lakini kila siku nalaumiwa tu basi na mimi bora nikae hivi hivi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote kabisa nataka kutumia nafasi hii kuwashukuru sana wapiga kura wa Bariadi Mashariki kwa kunirudisha hapa Bungeni.

Mimi nilikuwa sishindani na Chama cha Mapinduzi nilikuwa nashindana na kijana wangu ambao wapiga kura walinisaidia kumpa adhabu inayostahili. Kwa hiyo, nawashukuru sana. (*Makofi)*

Kwa msingi huo huo nataka kutumia nafasi hii najua tayari nimekwisha kupongeza wewe Mheshimiwa Spika, lakini nataka kukuhakikishia kwamba maoni ya Chama chetu tunapozungumzia juu ya Bunge tunaliangalia Bunge kama taasisi. Sisi wote ni wana wa Bunge hili na kwa hiyo yale yaliyosemwa na Mheshimiwa Ndugu yangu nyuma yangu hapa na sisi kama upande wa *UDP* tunasema tutalitetea Bunge hili ili liendelee kuwa na hadhi yake na lionekane kweli ni Bunge la watu ambao nawawakilisha wananchi wa Tanzania na bila kujali chama. Linapokuwa Bunge ni Bunge.

Pia nataka kutumia nafasi hii tayari nimeshampongeza ndugu yangu rafiki yangu Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa kuchaguliwa kuwa Waziri Mkuu natumaini yale niliyosema yameshatosha kwa sasa hivi nataka kukupongeza pia kwa kuja Bariadi kuangalia habari ya njaa.

Mheshimiwa Spika, labda katika mchango wangu ningeanza na jambo la njaa. Pamoja kuna pongezi zingine ambazo nimeshazitoa ndiyo maana nimeacha mambo ya pongezi kwa sababu Waheshimiwa Wabunge nilishawapongeza nilipozungumza mara ya kwanza labda niongeze tu kwamba wakati ule Mawaziri walikuwa bado hawajachaguliwa na Manaibu Waziri na wenyewe nawapongeza najua mbele yenu kuna kazi kubwa ya kufanya na kama Rais alivyosema tutawachangamsha. Natumaini mtachukulia kwamba tunapofanya hivyo tunafanya shughuli yetu ambayo ni kuonyesha upande mwingine wa shilingi. *(Makofi)*

Pia nataka kuwapongeza Wenyeviti wenzangu wote ambao tumechaguliwa kuingia katika safu ya uongozi. Mimi nawashukuru sana wanakamati ya *PAC* kunichagua kuwa Mwenyekiti wa *PAC,* ahsanteni sana na wananchi wanaweza kutegemea kitu ambacho tutakachoomba sisi. Wazungu wanasema *is value for our taxes* yaani tunataka tu thamani ya kodi yetu. Hatuna ugomvi na mtu tukipata thamani ya kodi yetu naona mambo yatakwenda sawa.

Kwa kuwa muda hautoshi ni afadhali niendelee na shughuli ambayo nataka kuifanya. Kwanza kabisa nilitaka kuzungumza jambo la njaa. Nazungumza jambo hili la njaa zaidi na mimi ningependa kuona hili jambo la njaa lichukuliwe kwa uzito unaostahili. Njaa inayozungumzwa sio njaa ya mwezi mmoja. Njaa tunayoizungumza ni njaa ya mwaka huu na njaa ya mwaka unaokuja. Hili nasema kwa sababu leo hii nilipopiga simu kwa Katibu wangu anayeshughulikia na mambo ya Bunge kule Bariadi takwimu hata za kilimo tu zinanitia wasi wasi sana ni jinsi gani hata Bariadi tu peke yake tutaweza kuishi. Wananchi wa Bariadi wameitikia kilimo, wamelima vizuri karibu ekari 16,000. Lakini mpaka hivi sasa imeota ni asilimia 17 tu kama vile hekta 2,801. Kwa hali hiyo tutaishi vipi? Sio hivyo tu.

Ukiangalia kama tuna njaa tulikuwa tunakimbilia pamba. Wananchi hawana matatizo ya kulima wamelima vizuri sana hekta zaidi ya 7,000, lakini pamba ambayo mpaka sasa imeota ni asilimia 25 tu. Kwa hiyo, hata kimbilio letu kwa pamba hakuna. Tungeweza tukakimbilia kwa mifugo lakini mifugo yenyewe leo pale Bariadi tuna mnada ukiangalia maksai ambaye alikuwa anachukua laki mbili na nusu leo kwa sababu

amekonda leo anauzwa kwa shilingi 35,000 ambayo ni sawa sawa na gunia moja la mahindi. Kwa hiyo, hata kimbilio ya Benki yetu kama mifugo Benki yetu nayo imekauka. Mvua katika siku 120 ambayo ndio msimu wa kulima mvua imenyesha kwa siku 12 tu. Inanyesha leo inaacha wiki mbili au mwezi mmoja kwa hiyo chochote kile kilichopo kinakauka, bado nafikiri tutaishi vipi. Kweli Waziri Mkuu amekwenda Bariadi ameahidi tani 2280 lakini ambazo tulizoomba ni tani 2280 tumepewa tani 838 na ameniambia kwa kuninong'oneza hapa kwamba ameongeza hajasema kiasi gani lakini hata hivyo hicho chakula kiko Shinyanga hakijafika Bariadi. Tatizo ni kubwa na ningependa Bunge hili lingeweka jambo hili la njaa *at least* kwa kikao hiki mbele kabisa. Kwa sababu hii ni Bariadi lakini nafahamu Magu ni hivyo hivyo, Kwimba ni hivyo, hivyo, Meatu hali ni mbaya zaidi na sehemu yote ambayo ninayoifahamu mimi.

Kwa hiyo, matumaini yangu baada ya kikao cha kuzungumza hotuba ya Rais tuje Wabunge na azimio lililo mahsusi kabisa ambalo inalieleza Serikali hatua ambazo tungependa sisi Wabunge lichukue ili kuweza kunusuru kwa mpango wa sasa hivi wa muda ambao ni mfupi na kwa marefu zaidi. Lakini kwa sasa hivi tunagawiwa mgao ambao unasema tu kwamba kilo 12 kwa yule ambaye asiyejiweza kwa shilingi 50 kwa kilo. Sijui sisi tuna wakazi wa Bariadi laki sita na hamsini, sasa sijui kama kwa utaratibu huu inawezekana kweli maana yake ukifanya mahesabu Bariadi inahitaji chakula karibu tani 15,000 na hiyo ni kwa mwezi sijui tutafika wapi? Kwa hiyo, nalisema hili kuonyesha kuwa Bunge hili ni Bunge la watu maskini. Ni Bunge la wakulima, ni Bunge la watu walio na wananchi kama walioko Bariadi ni lazima tutoke na jambo kabisa muhimu zito la kuhakikisha kwamba sisi tunawajali wananchi wetu na tunawajali labda hata zaidi ya mafao ambayo watu wanaandika katika magazeti. Bunge hili ni Bunge la watu maskini tunataka Serikali ichukue kweli jambo hili la njaa katika stahili ya kwake.

Mheshimiwa Spika, kwa maoni yetu pawe na chakula cha aina mbili. Hatuwezi kukataa chakula cha shilingi 50 kwa wale wasiojiweza kabisa lakini mimi naona njia endelevu tutafute chakula popote kilipo na Serikali iwe *facilitator* au iweze ikasaidia hicho chakula kifike kwa njia ya wafanyabiashara na wafanyabiashara washindane sio kwa ughali lakini kwa unafuu wa kuuza hicho chakula. Tukifanya hivyo chakula kitakuwa kingi na wananchi watajitahidi kupata mahali popote fedha kidogo ya kuweza kununulia, lakini tatizo ni kubwa. Kwa wananchi wa Bariadi mimi kama Mbunge nitajitahidi kwa kila njia kuhakikisha kwamba nashirikiana Serikali kuhakikisha kuwa kwamba makali ya njaa haya hayaendelei kuwa mabaya kama vile yalivyo kwa hivi sasa. Hilo ni la kwanza.La pili nataka kujikita zaidi katika hotuba ya Rais. Mimi kwanza nikiwa kama Kiongozi wa Chama cha Siasa ilinivutia sana nilipoona kauli mpya ambayo alioleta Rais ya kutaka ushirikiano wa dhati kabisa na viongozi wa Vyama vya Siasa ili kuhakikisha kwamba kweli tunajenga mfumo wa vyama vingi ulio endelevu na unaosaidia Watanzania wote. Mimi naona hili nataka kuliunga mkono na nitakuwa tayari kabisa na tumeona tayari kuna mambo ambayo yameshafanyika kwa mfano kuwepo kwa Waziri anayeshughulikia mambo ya siasa. Kwa hiyo, ni matumaini yetu kwamba yule Waziri anayeshughulikia mambo ya siasa basi atengeneze mazingira yaliyo mazuri ili kuhakikisha kwamba kweli azma aliyotangaza hapa Rais ya kuweza kuweka mazingira mazuri kudumisha utamaduni na vyama vingi kweli iweze ukafika. Lakini kuna mambo ambayo yanawezwa kufanywa kwa mara moja. Jambo la kwanza kuna haja sasa hivi

kuangalia upya jambo la takrima. Haiwezekani kabisa kwa hali ambayo tumekuwa nayo mtu mwingine anakuwa na fedha ambayo yuko tayari kumnunua mtu yoyote yule ambayo yuko ndani ya siasa. Bariadi tumeona Madiwani wengine wananunuliwa kwa shilingi kumi, kumi na tano milioni na mtu unajiuliza fedha hizi zinaokotwa wapi. Kama kuna shamba la fedha la namna hiyo basi wote tuelezwe ili tuweze tukaenda kuokota. Sasa hivi tumefika mahali na mimi Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi nawapongeza sana kwa kushinda na kwa kweli ni wengi na ni Wabunge wazuri wengi tu madigrii kibao na Madaktari lakini nawapa pole sana kwa sababu utaratibu wa kuwa Mbunge wa Chama cha Mapinduzi ni mgumu kweli kweli na kwa kile siwaonei wivu. Mimi naona tumefika mahali sasa ambapo huwezi ukawa na haki ya kuweza kumwakilisha mtu yoyote bila ya kuwa na mfuko, bila ya kuwa na fedha. *No money, no right to represent anybody*. Hali ya namna hii haiwezi ikaachiwa ikaendelea tu bila ya kuweza kuwa *checked. (Makofi)*

Mimi ni matumaini yangu katika Bunge hili nitaangalia mambo matatu ambayo mimi naona ni ya lazima. Kwanza Bunge lingependa liangalie zaidi wakulima. Mimi kila siku nitalikumbusha Bunge hili juu ya wakulima wa pamba. Haiwezekani wakulima wa pamba wakaendelea kuwa wao ndio wanafidia *industry* yote ya pamba kwa hali mbovu ya michango mbalimbali pamoja na bei ambazo zilizopo. Pia natumaini katika uhai wa Bunge hili tutaangalia zaidi watoto wetu. Haiwezekani kweli tukaendelea na utaratibu ambapo tuna watoto milioni 7.5 wakiwa katika *Primary School* na 500,000 tu ndio wako katika *Secondary School*. Kama kweli tunataka kuwa Taifa ambalo litaendeshwa kwa njia ya Sayansi na Teknolojia hali hii ni hali ambayo haiwezi ikaruhusiwa kuendelea. Pia ningependa jambo hili la ari, kasi mpya na nguvu mpya zaidi kwa mambo ambayo yanayohusu mazingira ni vizuri ingekuwepo lakini tuangalie. Mambo yanasema usifanye hivi kesho, usikate mti kesho bila kujua utapikia kitu gani ni lazima liangaliwe. Kinachotuangamiza watu wengi bila hata kupata hifadhi nzuri ya mazingira. Mimi kwa wale watu ambao ni watu wa kasi, nguvu, ari nina *suggestion* moja kuwa kwamba tufikirie juu ya ku-*stop, think and act*. Mimi naona hii itatusaidia sana na hii Kambi ya Upinzani tutawasaidia tu-*stop, think and act correctly.*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, na mimi niungane na wasemaji waliopita awali ya yote nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wa Mkoa wa Iringa kwa kuniwezesha kuingia katika Bunge lako Tukufu. Sambamba na hilo nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukipatia Chama Tawala kura nyingi za kishindo na kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge kuingia katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, takwimu zangu zinaniambia tunao wanachama waliojiandikisha wa Chama Tawala milioni 7, lakini kura zilizopatikana ni milioni 9. Hii peke yake inaonyesha imani kubwa waliyonayo wananchi wetu na imani hiyo inatakiwa tuiweke katika vitendo.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake nzuri ambayo imetupa maono ya kule tunakokwenda na tulikotoka. Kabla sijaanza kuchangia niseme kwanza kwamba ninaunga mkono hoja. Ninaomba nianze kwa kuchangia suala la kilimo na kimsingi nitazungumzia kuhusu kilimo cha chakula. Kule kwetu Iringa tunasema siasa ni kilimo. Asilimia 70 ya wananchi wetu wanaishi vijijini na kwa kweli tegemeo lao kubwa ni kilimo. Kilimo nitakachopenda kukizungumzia leo ni kilimo cha mahindi. Watu wetu wengi sana wanategemea kilimo hiki hasa mikoa ya Iringa, Mbeya, Rukwa na Ruvuma kwa kweli kilimo cha mahindi ndio zao la chakula na wakati mwingine ndio zao la biashara. Watu wetu wanafanya kazi sana na kwa kujitolea. Wakati wa kilimo ukiitisha mikutano katika mikoa hiyo niliyoitaja hutapata watu kwa sababu asubuhi saa 12.00 tayari wako mashambani tena wanakwenda bila hata kushurutishwa na utawakuta saa 12.00 jioni ndio wanarudi kule kwetu kuna vitu wanaita migoe. Watu hawa wanafanya kazi sana pamoja na kufanya kazi hizi sana maisha yao bado hayabadiliki kila iitwapo leo.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba kama tulivyosema katika ilani yetu na kama alivyosema Mheshimiwa Rais kwamba kilimo sasa kitakuwa ni kilimo cha *modernization*. Imefika wakati sasa wa kuhama kutoka kwenye kilimo cha jembe la mkono na kwenda kwenye kilimo kinachotumia pembejeo maalum kama pembejeo au matrekta. Zao hili pamoja ni kwamba tegemeo kubwa sana la nchi yetu bado bei yake ni ndogo. Inafika wakati watu wanaogopa kuwekeza kwenye mahindi kwa sababu wakati wa mavuno gunia la mahindi unaambiwa ni shilingi 5,000 kilo 100, mkulima huyu amehangaika palizi mbili, kupata mbolea na kadhalika. Kwa hiyo hata kile kiwango ambacho ametumia huyu mkulima wakati mwingine bado kinakuwa hakirudi anakuwa anajitoa sana. Nilidhani wakati umefika wa kuangalia hawa wakulima. Ni kweli tuna ruzuku upande wa mbolea na pembejeo lakini nadhani ipo haja ya kuliangalia sana.Nilikuwa najaribu kutafakari. Mara nyingi nasikia kuna Bodi mbalimbali, Bodi ya Kahawa, Bodi ya Pareto, Bodi ya Tumbaku lakini sijasikia Bodi ya Mahindi. Nadhani ipo haja sasa zao hili likaundiwa vyombo maalum ili kuweza kusaidia wakulima na uwezekano wa zao hili kupatikana kwa urahisi zaidi. Sambamba na hilo nilipenda nitoe mchango wangu mwingine na hasa ukizingatia mwaka huu tuna hali ya njaa lakini haitahatarisha kama tulivyoambiwa na hilo natumaini sana, nilidhani ipo haja ya kuwekeza katika kilimo cha umwagiliaji. Kilimo cha Umwagiliaji lazima tukiangalie sana tusitegemee mvua. Lakini sambamba na hilo basi tuangalie yale maeneo ambayo yanapata mvua za kutosha mwaka huu tunafanya nini ili mwakani suala la njaa lipungue. Basi tuwezeshe mikoa hii na wilaya hizi kuzalisha zaidi mwaka huu.

Pia nilidhani wakati umefika sasa wa kuwa na Kamati za Kilimo na Chakula katika kila kijiji. Kwa sababu kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa namba 7 na 8 ya mwaka 1982 kila kijiji kina uwezo wa kuunda Kamati zake. Zipo Kamati za Kudumu lakini Kamati zingine inategemeana na hali halisi ya kijiji. Kama ni kijiji kinachoshughulikia masuala ya uvuvi na kadhalika basi wanaweza wakaunda Kamati za Muundo huo. Kwa hiyo kila kijiji nadhani ni vyema kikawa na hizi Kamati za Kilimo na Chakula ili waweze kuweka takwimu vizuri kwamba kila eneo limepata kiasi gani na usambazaji wake unakuwa ni kiasi gani. Kwa sababu mara nyingi watu wetu

wanazalisha lakini wakati wa mavuno yamkini inatokea watu wanauza mazao yote na kusahau kutunza mengine hasa utashangaa Wilaya ambazo zimepata chakula kwa wingi leo hii wanaomba msaada wa chakula.

Kwa hiyo, huo ndio mchango wangu sambamba na hilo nichukue nafasi hii kuishukuru sana Serikali iliyopita na hii ya awamu ya nne kwa kuzingatia makundi maalum. Serikali yetu kwa kupitia Wizara yake imefanya vizuri sana kwa upande wa wanawake na kuwawezesha wanawake. Vile vile Serikali imefanya vizuri sana kwa upande wa watoto na vijana. Sasa nilidhani wakati umefika wa kuangalia kundi la wazee, walemavu na yatima.

Mheshimiwa Spika, hii nadhani ni changamoto siwezi nikatoa mikakati hapa lakini nilikua naomba nitumie nafasi hii kuzungumzia kwamba Wizara itupie macho jinsi ya kuwaangalia wazee wetu, walemavu wetu na yatima.

Mara nyingi watu ambao ni walemavu wakiwa wanaomba kazi sehemu utakuta mtu anaambiwa njoo nafasi ipo, lakini wakati mwingine akitokea pale katika ile sehemu ambayo ameomba kazi kwa kuwa ni mlemavu anaambiwa nenda nitakuita siku nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ningeomba sana suala la walemavu tuzidi kuliangalia nadhani *NGO'S* na mashirika ambayo yasiyo ya kidini yamefanya vizuri sana. Zaidi ya hapo ningeomba pia kuchangia suala la michezo, kwa sababu michezo ni afya lakini vile vile huongeza ajira

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ningeomba Wizara ijaribu kuangalia suala la kuinua michezo.

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie tena kuunga mkono hoja na kwa hayo machache nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

## HOJA YA KUTENGUE KANUNI YA BUNGE YA 21 (4)

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge kuna mambo hapa ambayo inabidi tuyaamue, moja ni kwamba nimepokea taarifa kutoka Serikalini, Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwamba ingefaa tupate *briefing* saa 1:30 jioni hii. Kwa kuwa jambo hili ni muhimu na wakati huohuo tunabanwa na Kanuni ya 21(4) ambayo hairuhusu kuahirisha shughuli kabla ya saa mbili kasoro robo inaruhusu kuendeleza hizi shughuli sio kuzifupisha.

Kutokana na umuhimu wa jambo lenyewe natoa idhini Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu aweze kutoa hoja tutengue Kanuni kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 124 ili 21(4) tuitengue kwa madhumuni ya jioni hii na tuweze kumaliza shughuli za Bunge saa 1:25 jioni hiyo itatuwezesha kupata *briefing* muhimu sana sana ya Serikali saa 1:30.

Kama naafikiwa hilo basi nitamwomba Mwanasheria Mkuu aweze kutoa hoja ya kutengua kanuni ya 21(4) ili Bunge liweze kuzingatia mambo mengine kwa kuahirishwa kabla ya muda wake.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwa Niaba ya Waziri Mkuu, naomba kutoa hoja kwamba Kanuni ya Bunge ya 21 (4) itenguliwe kwa kufuata Kanuni ya Bunge ya 124 (1).

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. ZAKIA H. MEGHJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwa)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya kutengua Kanuni ya 21 (4) ilipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono, hoja yenyewe ni yakutengua Kanuni ya 21 (4) inayotulazimisha kuendelea na shughuli rasmi za Bunge hadi saa mbili kasoro robo. Hoja ya kutengua imetolewa na kuungwa mkono. Kwa hiyo, Kanuni Namba 21(4) imetenguliwa. Kwa hiyo Mheshimiwa Spika atasitisha shughuli za Bunge saa 1:25.

Tangazo la pili, nimepokea maombi kutoka kwa waheshimiwa Wabunge ambao ni wachangiaji 115. Katibu amefanya hesabu na pia kuachia ule muda wa Mheshimiwa Waziri Mkuu kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, inaelekea kama muda wa kuchangia utakuwa ni dakika 15, basi hadi Ijumaa jioni watakaoweza kuchangia ni Waheshimiwa 76. Kwa hiyo, kiasi cha Waheshimiwa 39 hawataweza kuchangia. Sasa natoa ushauri tu kama tutaendelea hivyo basi tutawataarifu wale 39 ili waweze kuchangia kwa maandishi. Watakaopenda wachangie kwa kifupi kwa maandishi ili kumpa nafasi Mheshimiwa Waziri Mkuu kujibu hoja.

Kwa kuwa tutawafahamisha kesho asubuhi wale, ambao dhahiri hawatafikiwa wachangie kwa maandishi masuala yao basi Mheshimiwa Waziri Mkuu atafikishiwa hayo kwa utaratibu wa kawaida ili siku ya Ijumaa wakati anajibu hoja basi yale yaliyofikishwa kwa maandishi yataweza pia kupatiwa majibu.

Nieleze tu kwa utaratibu huo, bado katika *Hansard* ya Bunge waliochangia kwa maandishi pia kwenye *Hansard* inakuwepo. Kwa hiyo, kutakuwa na rekodi ya nini walichangia. Tunasikitika kwa hilo.

Mwisho ninaomba kuasa kwamba Waheshimiwa Wabunge mnauliza maswali marefu sana kwa Mawaziri, na mfano wa swali moja la kesho ambalo wala siwezi kutaja ni la Mheshimiwa nani, swali peke yake ni ukurasa mmoja. Swali la kesho moja hilo. Sasa kwa kuokoa muda nawasihi sana Waheshimiwa Wabunge tulenge katika jambo,

mara nyingine tunawalaumu Waheshimiwa Mawaziri kwamba wanazunguka sana katika sana katika kujibu ni kwa sababu swali la mzunguko linakaribisha jibu la mzunguko. Aidha kwa Waheshimiwa Mawaziri leo kulikuwa na jibu moja refu sana, nilikuwa napima hapa karibu dakika saba bado linajibiwa tu.

Sasa naomba pia Waheshimiwa Mawaziri wajitahidi kujibu kwa kulenga kwa kifupi tu na nilitoa tahadhari zamani Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu majibu ambayo hayajibu lile swali la Mbunge. Leo lilikuwepo moja, bado nasubira, bado Spika naona tulee hii hali kidogo ili tuzoee. Kwa sababu ni *give and take*. Lakini baada ya muda itakuwa vigumu kwa Spika kuacha kuigonga kidogo Serikali kama jibu lenyewe linaoneka kama kukwepa swali halisi la Mheshimiwa Mbunge. (*Makofi*)

Baada ya muda nitanong'onezana na Mheshimiwa Waziri Mkuu ili aelewe hiki ninachosema kinahusu swali lipi na jibu lipi.

Tunaendelea, Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, atafuatiwa na Mheshimiwa Wilson Masilingi.

**MHE. HASSAN RAJAB KHATIB:** Mheshimiwa Spika, na mimi nichukue nafasi hii kukupongeza sana kwa kupata kura nyingi sana ndani ya Bunge hili kuwa Spika wetu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hongera sana. (*Makofi*)

Lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Anne Makinda, kwa kuwa Naibu Spika nae kwa kupata kura nyingi sana. Lakini pia nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri Mkuu kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kupata kura nyingi sana ya imani ndani ya Bunge hili. Haijapata kutokea. kwa hivyo hongera sana. *(M akofi)*

Waheshimiwa Wabunge kwa wakati huo wa mfumo wa chama kimoja Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, wakatio huo hiyo ndiyo tulikuwa tunaiita *pressure group* wakati Serikali ikitaka kufanya mambo, Wabunge ambao wanataka kufanya mambo basi inapitia mikondo hiyo. Kwa hiyo, ninaamini kwamba shughuli zao zitakuwa ni zile zile za *pressure group*. Kwa hivyo ahsante sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nisiwe mwizi wa fadhira, nichukue nafasi hii niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Amani, kwa kunipa nafasi hii kwa kipindi cha nne kurudi tena Bungeni hapa na kama si wao mimi naamini nisingesimama hapa.

Lakini na mimi nawaambia kwamba imani yao walionipa wananchi wa Jimbo la Amani nitajitahidi kuwa nao pamoja na tutakwenda sambamba kuhakikisha kwamba Jimbo la Amani linapata maendeleo ya kutosha sana na msimamo ule ule kama alivyosema Mheshimiwa Spika, kwamba utakuwa wa *standard* na *speed*. Kwa hivyo huo ni mwendo ambao tutakaokwenda nao katika Jimbo letu la Amani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa hayo mafupi mimi niseme tu kwamba Hotuba ya Mheshimiwa Rais, hii ni dira tosha kabisa ya kusimamia maendeleo ndani ya nchi hii. Lakini mimi nitaanzia kwa amani na utulivu.

Mheshimiwa Spika, amani na utulivu ndani ya nchi hii, hii ni sera ya Chama cha Mapinduzi na Tanzania imepata sifa kubwa ulimwenguni kwa sera hii ya amani na utulivu. Waheshimiwa tumebahatika nchi yetu ya Tanzania imezungukwa na nchi nane, lakini nchi hizo zote nane kurupushani yoyote inayotokea katika nchi zao mafichoni kwao ni Tanzania na hawawezi kujificha Tanzania tu lakini wanafuata ile ile amani na utulivu.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi ningeishauri Serikali mtu anayechezea amani na utulivu ndani ya nchi hii kusiwe na mjadala, msemaji wa Mheshimiwa Waziri kwamba, kusiwe na msalie Mtume, Waziri alikuwa anazungumza sana kule wakati alipokuwa anazungumza kule Arusha au Moshi kule. Sasa mimi ningelishauri, kwamba, amani na utulivu ndani ya nchi hii ni sera ambayo inayoweza kuwalinda wananchi wake bila ya matatizo yoyote.

Mheshimiwa Spika hivi sasa yanajitokeza mambo ya maajabu sana. Sasa unajitokeza ujambazi wa hali ya juu, Kisiwa cha Zanzibar hivi sasa. Zanzibar ilikuwa unalala milango yote wazi, ndiyo. (*Kicheko*)

Narudia, Zanzibar ilikuwa unalala milango yote wazi, yote hakuna matatizo hakuna kurupushani unalala mustarehe kabisa. Lakini hivi sasa Zanzibar imekuwa na matatizo makubwa sana ya ujambazi watu sasa hivi wanakuja kwa Boti asubuhi wanatokea wapi haijulikani. Lakini wanakuja asubuhi wanafanya vurugu wanafanya huduma wanafanya ujambazi halafu wanarudi kwenye Boti wanarudi wanakokwenda. Sasa mimi nafikiri jambo la busara Serikali hii iliangalie kwa undani sana.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa hali yetu hii ya amani, kuna watu wachache wanataka kuiondosha hali hii ya amani kabisa. Amani hii ndiyo inayotuletea watalii ambao ndiyo wanaotupatia fedha ndani ya nchi hii kwa wingi, lakini sasa wakisikia taarifa kama hizi basi naamini kwamba wenzetu watakuwa moyo wao unapungua na watalii kuja watapungua. Sasa nasema Serikali suala hili ilivalie njuga, kuhakikisha amani na utulivu na purukushani ambayo inajitokeza hivi sasa inadhibitiwa kwa nguvu zote na mimi ningeliomba Watanzania, kwa sababu hawa wanaofanya vitendo hivi vyote wamo ndani ya miongoni mwetu, ndugu zetu, marafiki zetu, kaka zetu, wapenzi wetu na tunawaelewa.

Lakini sasa tusikubaliane nao kabisa kutuletea kutuharibia nchi yetu kwa manufaa yao. Ningeliomba tena Serikali na Watanzania wote kwa ujumla, hili tulivalie njuga sote. Tuwe kwa pamoja sote tuhakikishe amani yetu na utulivu tunaulinda kwa nguvu zetu zote ndani ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili nilikuwa nataka kuzungumza hifadhi ya mazingira. Bahati nzuri na mimi nimekuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Hifadhi

ya Maliasili na Mazingira. Hivi sasa watu hawakujali sana hii hifadhi ya mazingira na mimi nasema hii hifadhi ya mazingira hivi sasa tunazungumza habari ya ukame, huu ukame unatokana na uharibifu wa mazingira na ningeliwaomba sana sasa, hata hizi dira za mvua sasa hivi zimeharibika. Sasa ningeliomba sana hawa watu wa hali ya hewa wakaanza sasa kufanya *research*. Kwa sababu sasa hivi hali ya mazingira ya mvua na hali ya miongo imepitwa na wakati. Sasa kutokana na uharibifu mkubwa wa mazingira Tanzania sasa hivi iko katika hali ngumu sana sana kutokana na hali ya uharibifu wa mazingira.

Sasa mimi ningeliomba sana, watu wa hali ya hewa wakafanya *research* kabisa kutizama upya hali ya miongo ya mvua hivi sasa, hilo la kwanza. Pia wangekuwa wanasaidia hasa wakulima katika maeneo mbalimbali katika nchi hii. Lakini ningeliomba Serikali kwamba mazingira yawe yanapata *lesson* maalum hasa shuleni. Shuleni kukawa kuna *syllabus* maalum ya mazingira, ni vizuri kabisa kila mwananchi ajue umuhimu wa hifadhi ya mazingira. (*Makofi*)

Hivi sasa miti inakatwa hovya kabisa, magogo yanakatwa hovyo kabisa, watu wanatia moto bila mpangilio, sasa hii ni tatizo kubwa na tena isitoshe hivi sasa viwanda hivi vinavyochimbachimba dhahabu nayo ni moja katika kuchangia katika uharibifu mkubwa wa mazingira. Viwanda vikubwa vikubwa vinavyochimba dhahabu wanachimba dhahabu halafu wanaacha mashimo imekuwa matatizo makubwa.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi ninafikiri hawa viwanda na wao wanaochimba dhahabu basi nao wapewe mashariti. Moja baada ya kuchimba dhahabu basi waweke mazingira mazuri haidhuru wafukie mashimo yale au wapande miti mule waongeze nini.. Hiyo itakuwa ni jambo la busara kabisa lakini kwamba wao wanachimba wanachukuwa wanachokitaka halafu wanatuachia mashimo, inakuwa ni kitu kidogo kinamatatizo makubwa.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Mazingira imeweka sheria na utaratibu mzuri sana na imeweka kwamba siku hizi kuna utaratibu hata haya magari makubwa yanayokwenda kuchukua abiria utaona mtu anakula ndizi anatupa barabarani anakunywa maji mule ndani anatupa chupa barabarani, sasa unafikiri ule si utaratibu mzuri, nafikiri tuwe na utaratibu na sisi ndani ya nchi hii kuhakikisha kwamba hifadhi zetu za mazingira zinakuwa ni nzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, la tatu ambalo litakuwa ni la mwisho, maana naona kengele ya kwanza imeshapigwa, nazungumzia ajira. Ajira kwa vijana ni kitu muhimu sana na Mheshimiwa Rais katika hotuba yake aliizungumzia sana hili suala la ajira hasa ya viwandani, ajira binafsi na ajira nyingine.

Mheshimiwa Spika tatizo kubwa ndani ya nchi yetu ni vijana wengi wamekosa ajira na tatizo hili kubwa ndani ya nchi yetu hatujaweka utaratibu hasa wa kuwasaidia vijana hasa kujiajiri wao wenyewe. Sasa mimi ningeliomba kabisa kwamba vijana wakati wanapokaa pamoja kuunda ushirika wao, wawe wanajua wapi pa kwenda. Sasa hivi vijana wote wanaunda ushirika wanakaa pamoja lakini hawajui wanakwenda wapi

wala hakuna mtu anayewasaidia, lakini tunasema tu kaeni pamoja, kaeni kina mama, kaeni pamoja, lakini wanakwenda wapi, hakuna? (*Makofi*)

Sasa nafikiri Serikali ibadilike, Serikali ibadilike iweke utaratibu mzuri wa ajira ya kujiajiri wenyewe. Kwa sababu lazima tuzungumze kweli kwamba Serikali haiwezi kuwa na ajira kwamba wote wanaomaliza shule kwamba wanapata kazi Serikalini si sahihi hiyo ulimwengu mzima nafikiri hakuna. Lakini Serikali iweke utaratibu mzuri wa wananchi, vijana wetu kina mama kukaa pamoja na kutafuta njia ya miradi yao lakini wajue wanakwenda wapi. Lakini sasa hizi hata wakikaa, wakakaa pamoja wakafanya ushirika wao lakini wapi pa kwenda kupeleka matatizo yao, hakuna. Sasa mimi ningelishauri sana suala la ajira ya vijana ambao tunao wengi na uwezo huo hapa Tanzania nafikiri upo, tunao kabisa uwezo huo tukijipanga uwezo huo upo tunao ni utaratibu tu. Tufuate utaratibu tu, Naibu Waziri wa Ajira yupo ananiangalia vizuri tu hapa, na huo ni wajibu wako Mheshimiwa Waziri.

Lazima tuweke utaratibu mzuri unaofaa, kwa sababu vijana ndiyo nguvu kazi, mimi ningelishauri kitu kimoja, hivi sasa Tanzania inaleta sana mitumba ya magari, utasikia kuna *Mark II, Benz*, sijui nini, mitumba tu ya magari. Mimi ningelishauri Serikali sasa ilete mitumba ya matrekta. Sasa hivi iko haja kabisa Serikali wale ambao wenye uwezo wapewe nafasi ya kuleta mitumba ya matrekta ndani ya nchi hii. (*Makofi*)

Tuachane na mambo ya vijembe vya mkono, kwa sababu trekta mpya ni sawa lakini sasa ni bei kubwa. Ssasa unafikiri watu hawataki gari mpya, lakini kila mtu na uwezo wake. Yule ana uwezo wa kupata gari mpya acha anunue, yule ambaye hana uwezo wa gari mpya atanunua mitumba, ndiyo ulimwengu unavyokwenda kila mtu ana nafasi yake. Sasa mimi naishauri Serikali wale wenye uwezo uwaruhusu walete mitumba ya matrekta, *fugerson, ford* wazilete hapa na maplau yao na ma-*disc* yao ma-*planter,* ni vizuri kabisa ili kuongeza kasi ya kilimo na kuongeza ajira kwa vijana wetu.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache sitaki kengele ya pili inigongee kabla sijamaliza naunga mkono kabisa hoja ya Mheshimiwa Rais ahsante sana.(*Makofi*)

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda nikushukuru kwa dhati kabisa kwa kunipatia fursa ya kuchangia hoja iliyoko mbele yetu iliyowasilishwa na Waziri Mkuu, Hotuba ya Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete.

Kabla siajendelea naomba nianze na shukrani, napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kushiriki Uchaguzi Mkuu uliopita nikaweza kupata ushindi wa kishindo wa kwangu na chama changu Chama cha Mapinduzi. Kura 76,801,sawa na asilimia 91 ni dhamana kubwa kutoka kwa wananchi wa Jimbo la Muleba Kusini baada ya kuwatumikia miaka kumi nawashukuru wananchi. Naomba Serikali mnisaidie, ninaomba Waheshimiwa Wabunge, mnisaidie ni kazi ngumu. (*Makofi*)

Pia nashukuru sana kwa sababu hata Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete alipata kura nyingi sana katika Jimbo la Muleba Kusini na katika Tanzania nzima. Asilimia 88 ni ushindi wa kishindo hauhitaji mjadala uchaguzi umekwisha. Uchaguzi ulikuwa huru na wa haki, na nadhani swali lililoulizwa asubuhi hatutapata jingine la namna hiyo. Sasa nitoe pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Rais na Makamu wa Rais kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi. Ninampongeze Mheshimiwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Aman Abeid Karume kwa kushinda kwa kishindo. Ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuchaguliwa Monduli na akathibitishwa baada ya kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kwa kura nyingi na Bunge letu Tukufu kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hongera Mheshimiwa Edward Lowassa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakupongeza na wewe umepata ushindi wa kishindo na Naibu Spika ushindi wa kishindo. Wote ni vishindo vishindo, vishindo, lakini lazima niwapongeze. Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, mmeteuliwa mkapewa dhamana kubwa ya heshima nawapongezeni sana tena asana. Waheshimiwa Wabunge wote, nawapongeza kwa ushindi katika katika Majimbo na wengine kwa kuteuliwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Wabunge. Nawapongeza Wenyeviti wa Kamati za Bunge za kudumu na Makamu wao na nawapongeza Wakuu wa Mikoa wote walioteuliwa kushiriki kumsaidia Mheshimiwa Rais wa awamu ya nne kutekeleza majukumu ya utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa hari mpya, kasi mpya na nguvu mpya. Pongezi za pekee ni kwa wale Wabunge walioteuliwa kuwa Wakuu wa Mikoa maana yake uteuzi wao ni wa jana tu bado ni moto moto, hongera sana.

Sasa naingia kwenye hoja, Hotuba ya Mheshimiwa Raisi ni nzuri sana tena sana, na nimevutiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyoiwasilisha vizuri pia, naunga mkono malengo yote ya Mheshimiwa Rais na mbinu anazokusudia kuzitumia katika kuliongoza Taifa letu kwa miaka mitano. Ninapenda kuchukua nafasi hii kumhakikishia kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Muleba Kusini na kwa niaba yangu binafsi ushirikiano wa dhati na wa hali ya juu sana.

Mheshimiwa Rais ameweza kufafanua Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa lugha nyepesi, hata Wapinzani sasa wanaunga mkono hotuba ya Rais, na kwa hiyo wanaunga mkono Ilani ya Chama cha Mapinduzi, na hii ni ishara nzuri sana. Mimi nimevutiwa na hotuba ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani na walio changia baada yake, sasa tunaanza vizuri, tunaangalia *issues*, mambo ya msingi katika kuendeleza Taifa letu kuwaletea wananchi maendeleo kushinda vita dhidi ya umaskini. Mimi nimevutiwa na mambo mengi, lakini muda hautoshi nitasema machache, la kwanza ni kwa jinsi ambavyo Rais wetu amedhamilia kushughulikia masuala ya Muungano.

Muungano wa Tanzania kama alivyoeleza Mheshimiwa Rais ni sahihi unampasuko, na mipasuko ikitokea kabla yake kuna mitikisiko au matetemeko. Sasa matetemeko mara nyingi hata haya ya Dunia haya ya sekunde nane mfululizo wanasema mnaweza mkaisha naomba yasije hapa. Hapa lilijaribu tu sekunde mbili ilikuwa hatari lakini nasikia kulikwa kuna vipasuko humu ma-*engineer* wanasema.

Sasa ni rahisi kuweka mpasuko lakini kuuziba mpasuko sio kazi nyepesi. Mheshimiwa Rais wa awamu ya tatu Benjamin Mkapa amejitahidi kadri ya uwezo wake kwa kushirikiana na viongozi wenzake ndani ya chama na Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kutetea umuhimu wa Muungano na kuwezesha Muungano, akaukabidhi kwa Mheshimiwa Rais Kikwete ukiwepo na Mheshimiwa Kikwete amesema ameupokea na mpasuko anaomba Mwenyezi Mungu kipindi chake kikikoma ajitahidi kuacha bila mpasuko.

Naungana na mapendekezo ya Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe kama sehemu moja wapo ya mkakati. Lakini zaidi napendekeza mjadala ndani ya Bunge uanze mapema kwa sababu Mheshimiwa Rais ameahidi atawezesha Mjadala wenye lengo la kushughulikia mpasuko wa Muungano. Bunge likae pamoja na Baraza la Wawakilishi, kikao cha pamoja. Tujifungie mahali tena haraka sana ikiwezekana kuanzia mwezi kesho. Tujifungie mahali bila Waandishi wa Habari, bila waandishi wa habari, tuwaite wote wanaojua lolote juu ya Muungano, tuwaite wote wenye kero juu ya Muungano. Wapinzani wajiandae kuleta hoja, tutakomesha huo mpasuo kwa sababu tutapasua jipu lililokuwa limebaki. Mimi kuna ninayoyajua juu ya Muungano, lakini najua kidogo sana. Wengi wetu humu ndani mnajua kuliko mimi, sana.

Kwa hiyo tukikaa tukaambizana uso kwa uso tutajua nani mwenye tatizo kwenye Muungano huu, maana huu Muungano si wa Kisiasa huu. Huu Muungano kwa maelezo tuliyopata kwa Waasisi ni wa damu. Mimi nimebahatika na nyie mmebahatika kumsikiliza Baba wa Taifa, mimi maneno ya mwisho aliyoniambia Baba wa Taifa na sijawahi kusema hadharani kama wosia wake alisema; wewe kama Waziri kazi yako nakuomba umsaidie Rais kuhakikisha Muungano hauvunjiki. Nimetoka kwenye Baraza la Mawaziri, Mawaziri wapo. Mheshimiwa Marmo rafiki yangu saidia Mheshimiwa Rais Muungano usife. Mheshimiwa Makamu wa Rais siwezi kumwagiza wala siwezi kumpa maelekezo hata Waziri Mkuu siyo *size* yangu.

Mheshimiwa Spika, nasisitiza hili la Muungano kwa dakika kumi kwa sababu utekelezaji wa yote ambayo Mheshimiwa Rais amesema kwenye hotuba yanatekelezwa kwa malengo ya nchi nzima, siyo kwa Bara tu. Tumalize hilo ili tuweze kwenda kwa *speed*, hiyo ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya kama tunavyosoma katika hotuba humu ndani. Mimi nimesikia hotuba za leo nikasema hivi kweli kuna mpasuko! Mambo machache mengine yanahitaji kufafanuliwa au kuelezwa tu yamefanyika lini. Mfano sheria 40 za Tume ya Nyalali zingine tulishafuta,. Kama imebaki nadhani mbili au moja ambayo ina utata, sisi Serikalini tunasema si utata. Wanasema Tume ya Kisanga, ya Kisanga yapi! Tumeenda kwa wananchi, wananchi wakatuambia fanya hivi. Sasa haya ni mambo kuelezana, tukapasua majibu, tukasonga mbele.

Mheshimiwa Spika, sasa, nimevutiwa pia na hotuba ya Rais alipozungumzia kwamba ataendeleza Utawala wa Sheria na wa haki. Ndio kuondoa visiki kwenye uwanja wa siasa na maendeleo. Kazana na Utawala bora tutasaidiana.

Mheshimiwa Rais amezungumzia kuwezesha Watanzania, waweze na wenyewe kunufaika na fursa za rasilimali na mali zote za nchi. Mkazo, Elimu, mkazo Afya na kukuza uchumi. Vipaumbele vya Serikali tutavipata kwenye hotuba zenu za Bajeti. Ni mapema mno, maana hii ni hotuba ya Rais, najua Waheshimiwa Mawaziri mtakuja na mikakati na mapendekezo ya Bajeti tuwape fedha kutekeleza ilani. Mimi nitawapa ushirikiano mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie na njaa. Nakushukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, hukuja Mleba Kusini kwa sababu muda ulikuwa hautoshi ulienda kwenye *sampling* Shinyanga, Kilimanjaro. Naomba uje na Muleba Kusini, kuna njaa. Halafu hii njaa, ukiangalia Dodoma, mimi nimekaa Dodoma hapa, kuna njaa Dodoma na Singida kuliko ya Muleba. Lakini njaa tusiipime kwa wingi wa wenye njaa. Njaa ikishagusa hata mtu mmoja, ni njaa kali kwa sababu hakuna anayekula kwa niaba ya mwenzake. Kwa hiyo, tupeleke chakula kwa wananchi kwa mtindo wa dharura na ndivyo mlivyoanza Serikali imevutiwa. Sasa na tumia Jeshi, ndio mapendekezo yangu. Tumia Jeshi la wananchi na Jeshi la Kujenga Taifa wasambae. Baa ka njaa ni kama mafuriko. Ng'ombe anauzwa shilingi 2000 Manyoni siyo jambo dogo. Kwa hiyo, hamna maji, kama hamna maji ukipeleka mahindi hata wakisaga hawatapika. Tathmini isiwe ya mahindi tu, na ya maji. Pia naomba tafadhali sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, msisitizo wangu: Muungano tukae mapema, Rais atuwezeshe tukae hata wiki tatu tutoke na mapendekezo ya kuishauri Serikali namna ya kutatua mpasuko. Atuwezeshe, vichwa vyetu vinafanya kazi. Tu-*brainstorm* kwa siri, vikao vya siri, tupate nyaraka zote. La pili, njaa, twende kwa *speed* kutumia Jeshi la wananchi na Jeshi la Kujenga Taifa na kuhusu Usalama wa Raia najua mikakati inaendelea tusiseme hapo. Polisi tuwasaidie wasije wakaogopa. Sasa hivi nadhani Polisi wanaogopa badala ya majambazi kuogopa. Msiwatishe Polisi hawa majambazi hayana nguvu ni mabenki tu na wasingekuwepo vyombo vya habari msingejua. Kwani yanayotokea Muleba mnayaona! Wanatekwa watu Muleba kila mara, magazeti hayafiki. Ukerewe kule kwa Mheshimiwa Dr. Mongella, kila usiku, lakini vyombo vya habari vimekaa Dar es Salaam na kuibiwa Benki.

Sasa nashauri msiwatangaze majambazi kwenye vyombo vya habari. Vyombo vya habari acha sasa kwanza tupambane na majambazi. Unajua watalii watatukimbia kwa kuzidi kutangaza mambo ya ujambazi ambayo yatatishia watalii na wananchi kwa ujumla. Ukurasa wa kwanza majambazi, ukurasa wa kwanza majambazi, maendeleo ya nchi ukurasa wa tisa, dhana hiyo siyo nzuri hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ili tuweze kujenga nchi yetu. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. ANNA M. KOMU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Hotuba ya Rais. Kwanza, naomba nikishukuru Chama changu kwa kunipa nafasi ya kuingia katika Bunge hili Tukufu. Pili, ninaishukuru Serikali ya Tanzania kwa kutoa ruhusa kuingiza wanawake wengi *per cent 30* katika Bunge hili. Tatu,

ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuitoa nafasi ya wanawake walio wengi kuongoza Wizara kama Mawaziri, Manaibu Waziri na Makatibu Wakuu. Napenda sana kusema wakina mama tuko katika hali nzuri na kusema hongereni nyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nichangie hotuba ya Rais kwa kuanzia kwenye kipengele cha demokrasia ya vyama vingi katika nchi yetu. Nikisoma hotuba ya Rais yenyewe, ukurasa wa saba una sema nchi yetu sasa ni ya demokrasia ya vyama vingi. Lakini ni wazi bado Utamaduni wa mfumo huu wa siasa ni mchanga na kwa ujumla haujaimarika vya kutosha. Anahitaji kutimiza wajibu wake katika kujenga na kuimarisha Utamaduni na mfumo wa siasa ya vyama vingi.

Mheshimiwa Spika, nina masikitiko ya kusema kwamba Mheshimiwa Rais alipoandika haya alikuwa anaelewa fika kwamba kweli nchi yetu iko katika uchanga mkubwa sana wa vyama vingi vya siasa. Ndugu zetu kule vijijini mpaka hii leo walio wengi hawajui matunda na raha ya kuwa na vyama vingi vya siasa katika Halmashauri zetu na katika Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, mpaka leo wao walio wengi kwanza hawajui thamani ya kura. Ningeomba kuisaidia hii kwa kumwomba Mtukufu Rais na watendaji wote tuchukue kwa makusudi nafasi na uwezo wa kwenda kule chini kabisa kwa ndugu zetu, tuwape ukweli na uhakika wa nini maana ya vyama vingi vya siasa.

Mheshimiwa Spika, tukiendeleza kuleta ushabiki wa kusema kwamba tulio wengi tunashinda, tunapendwa, kwa kweli tunawadhulumu Watanzania kwa kuwaweka kwenye kiza cha kutokuwapa elimu hii nzuri.

Mheshimiwa Spika, la pili, ningependa kuzungumzia kuhusu wazee, wakina mama na vijana. Katika hotuba ya Rais alisikitishwa pia kwa hali ya wazee. Wazee wetu wanakuwa na hali ngumu sana wakati wanapostaafu wakirudi vijijini.

Mheshimiwa Spika, kuna mambo ambayo yanawakwaza wazee hawa. Wazee hawa katika kustaafu kwao kulipwa yale mapato yao ya kustaafu, inawawia ngumu. Wakishakustaafu wakirudi vijijini, panda shuka ya kudai haki yao inawapa ugumu. Kwa hiyo, wanajikuta wanarudi kwenye hali ya umaskini wa ajabu. Mimi kama mtoto sintaweza kuwasaidia kwa sababu tayari na mimi nina majukumu ya watoto. Kwa hiyo, ningeiomba Serikali na wale wahusika tuwaangalie hawa wazee katika kustaafu kwao na pia tusiache kuwaangalia wakishastaafu wanakwenda kila wakati unapofikia kupata ruzuku zao au kupata posho zao kwa wakati muafaka bila ya kusumbuliwa. Pia, tuangalie hii pensheni wanayolipwa wazee hawa iendane na wakati wenyewe, kwa sababu unapompa mzee shilingi 30,000/= kwa mwezi au 20,000/= kwa mwezi, sidhani kwamba zinaendana na wakati wa leo.

Kwa hiyo, hii nayo inachangia. Kila tunapofika wakati mambo yanapobadilika, tuangalie na hawa wazee tunawapa pensheni yao ya kuwatosha kuweza kumudu maisha wanapoishi kule.

Mheshimiwa Spika, wakinamama. Wakinamama ni wachangiaji wakubwa wa uchumi wa nchi. Wakinamama ni wafanyaji wakubwa wa kazi za mikono. Wakinamama ni wacharukaji wakubwa wa siasa.

Mheshimiwa Spika, lakini, kuna masikitiko pia. Wakinamama hawa wanatengeneza kazi za mikono za matenge, wanatengeneza kazi za mikono za kusuka, wanatengeneza kazi za mikono za kila namna. Masikitiko, hawana soko, wala hawajawekwa pamoja kuangaliwa katika utendaji wao huo wa vitu vyao. Kwa hiyo, wanajikuta wanatengeneza vitu ambavyo pengine Serikali ingewaweka pamoja ikawatafutia soko, ikawatafutia mbinu za kuweza kuuza vitu vyao na kupata faida zao halafu wagawane, nina hakika kwamba wakinamama hawa wangecharuka zaidi na hali ya utalii nchini kwetu ingekwenda vizuri kwa sababu na wao wangepata njia ya kuuza vitu vyao ili waweze kuishi. Naomba tuwatafutie njia hawa wakinamama, tuwape elimu ili wajiendeleze kwenye kazi zao za mikono na wasione wanafanya kazi ya bure isiyokuwa na faida.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vijana. Kuna wimbi kubwa sana la vijana wanaotoka vijijimi kukimbilia Mijini. Hatima ya vijana hawa ni nini? Nashukuru Mheshimiwa Rais anasema atafanya kila aina ya mikakati ili vijana hawa waweze kupata ajira. Ajira zitakuwa ngapi? Wataajiriwa hawa vijana kwa elimu ipi? Kwa sababu leo kuna mtu alichangia hapa akasema kwamba, wale wanaweza wakaajiriwa kutokana na elimu yao. Je, tuna hakika wanaokimbia vijijini kuja Mijini wana elimu? Hawana. Kwa nini wakimbie? Kilimo ndiyo uti wa mgongo, tunazungumza. Baba zao ni wakulima, mama zao ni wakulima, amekuwa kijana miaka 18/20 shauri ya kilimo. Lakini kila akiangalia anaona baba ni mkulima, mama ni mkulima umaskini umetanda, amekosa elimu, amekosa kuendelea kwa sababu yeye ati ni mkulima. Anakimbilia Mjini anakimbia kazi ya kilimo kwa sababu anaona kilimo hakina tija. Lakini je, vijana hawa wangeona kwamba baba na mama wanalima lakini wanapata tija kutokana na kilimo chao na yeye angepata ushawishi na kuwa na hamu ya yeye kuwa mkulima kwa sababu angekuwa anajua kuwa analima, kuna masoko na mimi mwenyewe nitafaidiaka. Turudi tena kuiangalia tena upya Wizara ya Kilimo na kuipa nguvu mpya Wizara ya Kilimo ili tuijenge katika hali ya kwamba kilimo siyo umaskini, lakini kilimo ni utajiri.

Mheshimiowa Spika, vijana wetu wanahangaika sana. Vijana wetu wameingia kwenye hali mbaya. Sisi Ofisi yetu ya chama iko Kinondoni, ni masikitiko makubwa sana kuona vijana wameathirika kwa mambo ya ajabu wanayoyafanya kama kutumia madawa ya kulevya, ulevi wa bangi na kadhalika. Lakini yote ni kukosa dira ya namna ya kuwasaidia vijana wetu wanaoongezeka kila kukicha.

Mheshimiwa Spika, hii yote, hatuna tena Mashirika, hatuna tena ajira, hatuna tena mielekeo ya kuwawezesha hawa vijana. Kwa hiyo, wanakwisha hawa vijana. Turudishe yale Mashirika. Njia gani tutayarudisha yale Mashirika, sijui mimi lakini wale wanaoweza wakae kitako chini wafikirie kurudisha Mashirika yale *either* kwa wanaohusika wenye utajiri ambao ni Watanzania waeleweshwe kwamba wanaweza wakawa na *shares* wapewe ushawishi wa hali ya juu, zitungwe nyimbo, ziwepo ngonjera kwamba kuwekeza ni jambo zuri kwa wewe Mtanzania ili wawe na ushawishi waingie

katika kuwekeza. Tuimarishe Mashirika yetu, vijana wetu wapate ajira na pia wapate elimu.

Mheshimiwa Spika, ninakwenda kwenye Muungano. Nimefurahi sana kumsikia Mheshimiwa Masilingi akizungumza Muungano. Mheshimiwa Masilingi ameuzungumza Muungano, lakini mimi ninaongea hivi; hakuna anayenung'unika yeyote akawa hana kitu kinacho-m-*pinch*. Yeyote anayeota manung'uniko, ana kitu kinamwumiza. Sidhani kwamba watu wanaounung'unikia Muungano hawapendi ushirikiano au Muungano. Sote tunapenda Muungano, sote tunapenda kushirikiana. Mimi Mzanzibari nimeolewa bara, ni Muungano. Lakini je, hawa ambao wananung'unika, hawa ambao wanasema, hawa ambao wanalia, waliitwa wakaulizwa? Hapana. Tuwaite, tuwaulize kwa nini mnasema Muungano mbaya?. Kwa nini mnalalamika? Tutoe vikaratasi, kila mmoja atoe maoni yake kuhusu Muungano anataka uwe Muungano wa aina gani, anataka Muungano usukwe vipi, anataka Muungano upi ili na wao wachangie kama alivyosema aliyepita kwamba hapo tutapata yale ambayo ni yakinifu kwa wale wanaonung'unika. Lakini tukikaa tu tukimpa Mheshimiwa Mwinyi kazi ya kumwambia basi wewe shughulikia Muungano wakati Mheshimiwa Mwinyi hajui hao wanaosikitika wanasikitika kwa maana gani. Nafikiri itamwia ngumu. Tukianza kutoa vikaratasi vya toa maoni yako. Kila unayeona hayo ni maoni yako ya kurekebisha Muungano. Basi hata kama kwenye viboksi tupu tutapeleka Posta. Kila mmoja atatoa maoni yake jinsi ya kurekebisha Muungano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa neno moja tu. Masikitiko yangu makubwa sana pia yanakuja kwenye huo mpasuko. Mpasuko wa nini? Na kwa nini mpasuko uwe kwa Wazanzibari? Kwa nini mpasuko uwe wa Unguja na Pemba, usiwe wa Unguja Visiwani na wa Bara? Kwa nini? Wakati Wapemba na Waunguja wote ni Wazanzibari! Lakini, kama alivyosema Mheshimiwa Hamad Rashid asubuhi kwamba usitafute mchawi. Wachawi tunawajua na amewataja. Tuulizane kwa nini kuna mpasuko huu? Basi nina hakika tukikaa pamoja Wazanzibari wenyewe, Wapemba na Waunguja tukajadiliana, basi tuwekewe na hao ndugu zetu ili tujue huu mpasuko unaletwa na nini na haraka sana utafutiwe dawa ili watu hawa wakae pamoja. Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kuwasilisha. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hotuba ya Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyo wasilishwa asubuhi na Waziri Mkuu wetu.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba kwa niaba yako niwapongeze sana wananchi wa Jimbo la Sumve kwa kunipa kura nyingi. Mimi nauita ushindi wa heshima. Wa kishindo najua upo, kila mtu anasema kishindo lakini huu nasema ni ushindi wa heshima kwa mimi mwenyewe, chama changu kwa ujumla na Rais wangu.

Ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward N. Lowassa. Ameonyesha jinsi gani anaweza kuisimamia Serikali, tangu hapo awali na mimi nilishampongeza kabla hajawa Waziri Mkuu kwa sababu wakati yuko Wizara ya Maji, kazi aliyofanya ni kazi kubwa kweli kweli ya kuamua maji ya Ziwa Victoria yatumike kwa manufaa ya Watanzania wote na siyo kwa nchi zingine peke yake. Kwa hiyo, nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nitazungumzia mambo matatu, kama siyo manne. Nitaanza na suala la Mazingira. Limetajwa kwenye hotuba ya Rais. Mheshimiwa Rais ameomba karibu kila mji, kila kaya ipande miti. Lakini, mimi naomba kwa sababu ukizungumza tu kwamba kila kaya au kila mji wapande miti, nafikiri hawawezi kupanda. Mimi naomba hili ili nchi yetu baada ya miaka 10/20 ijayo isiwe jangwa, naomba iwe sheria. isiwe tu maneno ya kuzungumza humu ndani na kuzungumza kwenye vituo mbali mbali. Iwe sheria kwamba kuanzia sasa, kila kaya lazima kila mtu apande mti mmoja mmoja. Mheshimiwa Spika, nina hakika tutafika.

Mheshimiwa Spika, la pili, naomba nizungumzie elimu. Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu la Sumve na Wilaya yangu ya Kwimba, tuna tatizo kubwa kweli kweli la walimu hasa wa sekondari. Ninazo shule zaidi ya 10, sina walimu wa sekondari. Nina upungufu wa walimu 22. Vijana wangu mwaka jana waliingia kidato cha kwanza na mwaka huu wanaingia kidato cha pili na mwishoni mwa mwaka huu watafaya mtihani ili waweze kufaulu kuingia kidato cha tatu. Kwa sababu hawana walimu, hawatafaulu. Matokeo yake watarudi nyumbani. Jitihada zetu zote pamoja na wananchi na Serikali zitakuwa ni kazi bure. Naiomba Serikali kwa dhati kabisa, walimu hawa 22 tupatiwe ili waweze kwenda kuwafundisha vijana wetu waweze kupata elimu nzuri na waweze kufaulu kwenda kidato cha tatu na baadaye kidato cha nne.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kilimo. Kilimo chetu tulikuwa tukisema kila siku hapa kwamba kilimo chetu sasa ni kilimo cha kujikimu. Lakini, sana sana tunatumia jembe la mkono. Mheshimiwa Spika, nenda popote pale, wananchi wanalima kwa jembe la mkono. Hatuwezi kufika popote pale hata ikinyesha mvua namna gani, sana sana tutakachofanya ni kupata chakula cha kujikimu peke yake. Hatuwezi kuuza nje, kwa sababu ukilima kwa mkono hasa kwa kipindi hiki. Watanzania wengi kwa kweli wamekuwa wavivu kwa kulima, ni kwa sababu kwanza; maeneo ni madogo. Mimi naiomba Serikali, limesemwa , limesemwa hapa na mimi naomba nirudie. Iko haja sasa ya Serikali kuamua kwamba kwa mwaka huu kwa mfano katika kipindi cha Bajeti kijacho 2006/2007, Serikali iamue iagize matrekta. Inaweza aikaanza na matrekta 500 kwa sababu lazima tuamue. Matrekta 500, lakini limesemwa hapa na mchangiaji mmoja, si vibaya sana kwa sababu labda uwezo kwamba wananchi matrekta yakija haya bei inakuwa kubwa. Basi tuagize au tuwape wafanyabiashara walete matrekta yaliyotumika yaje yasaidie kuinua kilimo chetu ili tuweze kulima zaidi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine. Naomba nizungumzie suala la Ukimwi na suala hili nafikiri wengi bahati nzuri wachangiaji wote tangu asubuhi hawajaligusa. Mimi naomba niligusie. Naam!

Mheshimiwa Spika, suala la Ukimwi ni janga la kitafa, ni janga la dunia nzima. Watanzaia wenzetu wanapukutika, vijana wenye nguvu zao wasomi wanapukutika. Mheshimiwa Spika, ukitazama leo idadi ya wanaokufa au wanaoathirika na Ukimwi ni wengi zaidi, idadi haipungui hata siku moja. Pamoja na makongamano na mabango, idadi haipungui hata siku moja. Naomba Serikali kwa sasa ipeleke semina vijijini. Huku Mjini wameishatosha na bahati mbaya wakiiugua huku Mjini wanatoka huku wanakwenda vijijini ambako hakuna semina, hamna makongamano, hamna vipeperushi.

Mheshimiwa Spika, naomba sana hili Serikali ilione na ilifanyie kazi. Lakini si vibaya, tunaweza tukasema kwamba labda itakuwa ni udhalilishaji, si vibaya kwa manufaa maanake kitu hiki si cha kuogopa, si vibaya ikiwezekana hata sinema za wale walioathirika ikiwezekana nasema tuangalie zikaonyeshwa kule vijijini jamani hali halisi ni hii kwa sababu wengine hawajaona tatizo kwamba mtu akiugua ugonjwa huu anakuwaje. Lakini sinema zikienda kule vijijini mbali na haya matangazo na haya makongamano, nina uhakika Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu inaweza ikasaidia kwa njia moja au nyingine. Janga la Ukimwi si lele mama, nina uhakika Waheshimiwa Wabunge tukiambiwa humu kwamba tukapime sote humu, wengine watakimbia. Mheshimiwa Spika, lakini naomba kwa dhati kabisa hili si la mzaha hata kidogo. Mwisho, naomba nizungumzie michezo. Nampongeza sana Rais wetu kwa kumteua Mheshimiwa Joel Bendera Nkaya. Nina uhakika atasimamia michezo vizuri. Lakini kwa sababu humu ndani ya Bunge tumo wanamichezo wengi, tutakushtaki endapo hutatekeleza yale majukumu uliyopewa. Uwanja wa Taifa unajengwa pale, wa Kimataifa na ili ufaye kazi, lazima uboreshe michezo. Vinginevyo *brother*, itakuwa ni tatizo uwanja ule hautafanya kazi kama inayotakiwa.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo ni la muhimu zaidi. Mheshimiwa Waziri Mkuu Wilaya ya Kwimba mpaka sasa hivi imepata tani 1000 za chakula cha njaa. Mheshimiwa Waziri Mkuu, hakitoshi. Wilaya ya Kwimba ni kubwa na bahati nzuri nimeisha kuandikia vinoti vingi tu tangu tuko kwenye semina pale *Ubungo Plaza.* Lakini, nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kutoa tani 540, lakini naomba kiasi hicho hakitoshi. Najua ni maeneo mengi yana matatizo lakini tunapishana kwa matatizo. Wilaya ya kwimba ina matatizo zaidi ya tatizo la njaa. Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba sana utusaidie ili wananchi wetu waweze kupata chakula hicho wasife kwa njaa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja na nawatakia kila la heri Waheshimiwa Wabunge wenzangu katika shughuli zao zote pamoja na Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu na Wenyeviti wa Kamati. Ahsanteni sana nawashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika hotuba hii ya Mheshimiwa Rais. Kabla ya yote napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza wanachama wa chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) pamoja na viongozi kwa heshima yao kubwa waliyoweza kunipa na kuweza kunirudisha tena humu Bungeni kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, pia, nichukue nafasi hii kukupongeza wewe pamoja na Naibu wako, Waziri Mkuu, Mawaziri na Manaibu wao kwa uteuzi walioupata na ninawatakia kila la kheri na tunawaahidi ushirikiano ili kuleta maendeleo katika nchi yetu. Kipekee napenda kumpongeza Naibu Spika, mama yetu Anna Makinda. Mimi binafsi amechangia kuweza kunirudisha katika Bunge hili. Pamoja na kuwa tumetofautiana kwa itikadi, lakini hakuwa mchoyo wa fadhila. Pale tulipokwama tulimwendea na aliweza kutusaidia, ndiyo maana katika wale wanawake saba wa Kambi ya Upinzani waliokuwemo, ni mimi peke yangu nimeweza kurudi. Ninampongeza sana na ninamtakia kila la kheri katika uteuzi alioupata na kazi yake mpya ya Unaibu Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kwenda kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais. Katika ukurasa ule wa saba (7) Mheshimiwa Rais ameonyesha nia yake kuhusu Vyama vya Upinzani kwamba anataka viwe vyama vyenye nguvu na hana nia ya kuviua vyama hivyo. Hapa ninapata wasiwasi. Ninaamini Rais ana nia njema, lakini sina hakika na viongozi hasa wa Chama cha Mapinduzi ambao wanakiuka ahadi aliyotoa Mheshimiwa Rais.Hivi karibuni lilitokea tatizo kule Kigoma na walioshiriki kufanya njama hizo ni Viongozi wa Chama cha Mapinduzi. Walitaka kumtorosha Diwani wetu na tulifanikiwa kumwokoa *airport* akiwa chini ya Mwenyekiti wa Wilaya wa Chama cha Mapinduzi wa Kigoma Ujiji. Sasa napenda kuuliza, kama kweli Rais wenu anatoa kauli ..….......

**WABUNGE FULANI:** Rais wetuuu! *(Kicheko)*

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Rais wetu ametoa kauli na ameamua kabisa kuunda Wizara …

**MHE. BALOZI GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mongella, kanuni ipi kuhusu utaratibu?

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Kanuni ya 50. Kanuni zetu zinataka tutumie lugha nadhifu kwa ajili yetu sisi wenyewe na kwa ajili ya wasikilizaji na hasa inapohusu Rais wa nchi ambaye sasa siyo Rais wa chama kimoja, ni Rais wetu wote baada ya uchaguzi kama tulivyo Wabunge. Ukishakuwa Mbunge, ni Mbunge wa vyama vyote katika eneo lako. Kwa hiyo, kauli ile ningemwomba, wala siyo kumwomba, kufuatana na taratibu aifute. *(Makofi)*

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, ninafuta kauli hiyo. *(Makofi)*

Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikubali na akaunda Wizara ya Mahusiano na akateua Waziri wa kushughulikia mahusiano ya vyama, lakini baadhi ya Viongozi wa Chama cha Mapinduzi wanakuja kinyume na kauli aliyoitoa Mheshimiwa Rais na kuwarubuni Viongozi wa Vyama vya Upinzani ili wao waweze kushinda. Hii inaonyesha kabisa ndugu zetu au watani wetu hawako tayari kuungana na Rais katika kuviimarisha Vyama vya Upinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaiomba Wizara husika iingilie kati suala hili kwa sababu mpaka sasa Halmashauri ile imeshindwa kufanya kazi, wameshindwa kufanya uchaguzi kwa sababu tu ya vyama viwili hivi kupingana. Ninaomba Waziri alifanyie kazi suala hili haraka ili wale waliochaguliwa na wananchi waweze kufanya kazi maendeleokwa wananchi wao. Napenda pia niongelee suala la rushwa ambalo Mheshimiwa Rais aliligusia katika hotuba yake. Kumekuwa sana na malalamiko kutoka kwa wananchi kwamba rushwa imekithiri katika nchi yetu. Wabunge pia tumesema sana katika Bunge lililopita, lakini sasa ninaomba tushirikiane na Mheshimiwa Rais katika suala hili la rushwa, maana rushwa hii nayo imeingia hata katika uchaguzi ambapo imepewa jina kwamba ni takrima. Kambi ya Upinzani tulilisema hili kwamba takrima ni rushwa likapingwa vikali, lakini kinyume na matarajio yetu wapo wale wa Chama cha Mapinduzi nao wanalalamika kwamba takrima imetumika na haki haikutendeka kwa sababu hawakuwa na takrima ya kutosha ya kuwawezesha wao kushinda. Kwa hiyo, tunaomba suala hili la rushwa lifanyiwe kazi pamoja na lile la mikataba ambayo wananchi wameipigia kelele, hasa ile ya madini tunaomba iletwe Bungeni ipitiwe upya ili tuone haki inatendeka kwa wawekezaji na hata kwa sisi wananchi wa Tanzania tuweze kunufaika na mali asili ambazo Mwenyezi Mungu ametujaalia sisi katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili napenda kulisema sasa kwa sababu lilisemwa kwenye semina kwamba Waheshimiwa Wabunge tumeshindwa kuwatetea wananchi tukajali maslahi yetu. Lakini hapa napenda kulisema pia kwa sababu Mheshimiwa Rais alizungumzia mishahara ya watumishi na ninaomba suala hili lifanyiwe kazi ili wananchi wasituelewe kwamba sisi tunajali maslahi yetu bila kuwajali wao. Tunaamini kuwa watumishi wapo kwenye mazingira magumu, wanafanya kazi kwenye mazingira magumu hasa Madaktari, Wauguzi, Polisi na Walimu mishahara yao hairidhishi. Kwa hiyo, tunawaomba Mawaziri wanaohusika katika hili walifanyie kazi ili wafanyakazi hao waliopo katika Sekta hizi waweze kupenda kazi zao na wasijihusishe na vitendo vya rushwa kwa sababu mshahara wanaoupata haukidhi mahitaji yao.Pia ningependa kuongelea suala la michezo ambalo pia Mheshimiwa Rais alilizungumzia. Hivi karibuni lilikuja kombe la dunia, Watanzania tulijitokeza wengi na wengine wakapiga nalo picha. Sijui tumejifunza nini kwa kombe hili kuingia nchini mwetu na tuna mipango gani! Nchi yetu iko nyuma sana katika michezo tujitahidi tufikie michezo ya Afrika kama hili kombe la dunia bado lipo mbali kwetu sisi. Lakini michezo hii pia inahitaji viwanja kwa ajili ya mazoezi ya hao wanamichezo.

Pia napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Rais aliyemaliza muda wake kwa uwanja ambao unajengwa Dar es Salaam. Ni uwanja wa kitaifa na ni uwanja mmoja tu tutakaokuwa nao kwa sasa, ila tuna viwanja vingine vilivyoko mikoani wa CCM. Viwanja hivi vimechukuliwa na ndugu zetu wa Chama cha Mapinduzi. Sina tatizo vikiwa chini ya Chama cha Mapinduzi, tatizo langu ni kwamba viwanja vile havifanyiwi ukarabati, viwanja vimekuwa kama mahame. Tunawaomba ndugu zetu wa CCM waviangalie viwanja hivi na kama hawawezi kuvitunza basi wavirejeshe kwa wananchi kwenye Halmashauri au *Councils* za miji ili viwanja hivyo viweze kuhudumiwa na

tuweze kupata viwanja vizuri. Hatuwezi kupata wachezaji kama hatuna viwanja. Kwa hiyo, nawaomba ndugu zangu hili mlijadili, likishindikana basi muwarejeshee wananchi mali zao.

Mwisho napenda kuongelea suala la ulinzi na usalama. Kumetokea matukio mbalimbali ya ujambazi katika nchi yetu, yanatisha na sana sana yanatokea katika mabenki yetu na sasa inatutia woga hata kwenda kwenye mabenki maana tunahofia tukiingia humo tutavamiwa na majambazi.

Mheshimiwa Spika, kama walivyokwishasema wenzangu, tunaliomba Jeshi la Polisi walifanyie kazi suala hili, si kwa askari peke yake, hata wananchi tushirikiane na Jeshi la Polisi kwa sababu tunajuana, majirani zetu tunafahamiana. Pale tunapoona watu wanaingia katika mitaa yetu au vijiji vyetu ambao hatuwajui ni vizuri tungetoa taarifa kwa vyombo husika maana hao ndiyo majambazi wenyewe wanaoingia na kutuvamia.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ELIATTA N. SWITI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika hoja ya hotuba ya Mheshimiwa Rais. Awali ya yote ninapenda kukupongeza wewe kwa kushinda kwa kishindo. Pili, ninapenda kumpongeza Rais wetu ambaye kama nilivyosoma kwenye gazeti moja lilisema kwamba alishinda kwa kishindo cha kufuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, nawapongeza Wabunge wote kwa sababu nao wameshinda kwa mtindo huo huo, ndiyo maana tuna Wabunge wengi sana hapa katika Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mtovu wa fadhila kama sitaweza kuwashukuru akinamama wa mkoa wa Rukwa kwa kuniwezesha kufika hapa Bungeni na kwa kuonyesha kwamba wana imani na mimi, nami naamini nitaweza kuchangia na kuwasaidia kadri ya uwezo wangu. Nitawasaidia akinamama hao, wanawake, watoto na akina baba wote wa mkoa wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mimi natoka katika mkoa wa kilimo, napenda kwanza kuchangia hoja kuhusu kilimo. Mkoa wa Rukwa kama sisi wote tunavyofahamu ni mkoa unaozalisha chakula na hasa mahindi. Lakini wazalishaji wa mkoa huu hawana vitendea kazi vya kisasa, wanalima kwa kijiko, yaani kwa majembe ya mkono. Kwa hali hii, sisi watu wa Rukwa tungependa sana kuwasaidia wenzetu ambao si kwa uvivu basi kwa matashi ya Mungu hawawezi kuzalisha chakula cha kuwatosha. Lakini ninaomba Serikali katika miundombinu yake ya kilimo basi iwawezeshe wana-Rukwa kuweza kupata mabwawa ya kumwagilia ili waweze kulima mwaka mzima na pia waweze kuzalisha chakula chao wenyewe na waweze kukuza uchumi wao.

Mbali na hayo, kama sisi ndiyo mkoa unaozalisha chakula katika *the big four*, tunaomba sana Serikali itusaidie. Pamoja na kusafirisha mahindi na nafaka nyingine, basi waweze kututengenezea *national millings* tuweze kutengeneza unga badala ya kuuza tu mahindi na tuweze kukuza uchumi wetu. *(Makofi)*

Pamoja na hayo, miundombinu imekuwa ni kikwazo kikubwa kwa wana-Rukwa, barabara zote zinazoelekea vijijini hazitamaniki! Ukienda kwa Mheshimiwa Mzindakaya kule Kwela, barabara zake zina miti mikubwa ambayo unaweza hata ukachana mbao, ni gari gani itapita kule? Ukienda barabara ya kutoka Sumbawanga kwenda Mambwekenya tangu walipotengeneza sijui watu gani huko, labda wakati mimi nikingali mtoto mdogo, basi hali yake haijabadilika mpaka leo! Kwa hiyo, ninaiomba Serikali iyatazame upya masuala ya miundombinu ili huu mkoa ambao unachangia chakula cha wananchi uweze kufanya vizuri zaidi kuliko unavyofanya sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa pili ni kuhusu ulinzi na usalama wa raia. Kwa sababu majambazi walioko sasa hivi nao wamekuwa ni wa kisasa, nina machache tu ya kuchangia kwamba Serikali yetu itafute miundombinu ya kuwawezesha walinzi wote wa namna zote, yaani polisi na walinzi wa namna nyingine zozote waweze kupata mafunzo ya kisasa ili waweze kupambana na hao wahalifu wa kisasa.Napenda kuchangia pia kuhusu njaa. Ndugu zangu njaa si mchezo. Nilipokuwa nafanya kazi *US Information Service* miaka hiyo ya nyuma, wenzetu wa Chad walikosa mvua kwa miaka mitano mfululizo, sisi leo walau tuna walau chakula kidogo japo hatujui mwaka kesho kama kutakuwa na mvua. Ninaiomba Serikali hizi *regions* ambazo zinatoa chakula kwa sasa na mvua inanyesha basi nguvu zote zielekee kule ikiwemo Rukwa. Bonde la Rukwa lina maji, lina Ziwa Rukwa, tunaweza tukafanya umwagiliaji kwa urahisi kabisa. Naomba Serikali iliangalie suala hilo ili tuweze kunusurika na tuwe tumejiandaa kwa miaka mingine ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu waandishi wa habari, kama nilivyosema, mimi nimefanya kazi *US Information Service,* ku-*extract information* ni kitu muhimu sana. Wenzetu wanapokea *information* halafu wanachuja *information* kwa manufaa yao na si kwa manufaa ya umma au kwa manufaa ya wale ambao wanapaswa kuutetea umma. Kwenda kusema kwamba Wabunge wanataka maslahi ni kitu ambacho ni *broad* yaani ni kipana mno. Ninavyokumbuka, au nilivyoelewa katika ile semina yetu ni kwamba hawa Wabunge walisema kuwa: "Ingefaa nao waweze kupata kifungu ambapo watakapowafikia wananchi nao waweze kuchangia katika maslahi ya wananchi, isionekane kwamba Wabunge wanachukua mishahara yao wakawadhiki watoto wao wakawapekea wananchi." Nayo hiyo itakuwa si bora. Nawaomba waandishi wa habari wabadilike, wa-*extract information* zao vizuri ili wafikishe taarifa nzuri kwa wananchi wetu bila kuleta mgongano kwa wananchi na Wabunge. Napenda kusema tu mimi siyo mtaalum, lakini nimefanya kazi katika mashirika hayo. Mahakama zetu zimekuwa zikiajiri mahakimu wastaafu. Sijui wanalipwa kwa kesi au kwa mwezi kiasi gani. Lakini suala hili limeonekana kwamba linaweza kuwa ni chanzo cha rushwa mahakamani kwa sababu hawa watu wameonekana kutaka kupata chochote kutoka kwa wale wanaotaka kupendelewa. Naiomba Serikali iangalie hilo na ione kama kuna umuhimu wa watu

hawa ambao wameishastaafu kurudi wakati vijana wetu wengi wamesoma sheria na wangependa kwenda kufanya kazi hizo wakatusaidia.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho napenda kuchangia kuhusu UKIMWI. Suala la UKIMWI limekuwa ni tatizo. Ni tatizo kwa uzalishaji, maana ni kikwazo cha maendeleo, lakini pia ni tatizo kwa wananchi kwa sababu tunapokuwa na *home based caretakers*, hao *home based care* wengine wanakuwa hawana *training* yoyote, wanakuwa hawana ujuzi wa kuwasaidia hawa wagonjwa, wamekuwa ni chanzo cha kuhamisha magonjwa kutoka katika majumba yao na kupeleka mahali pengine kwa sababu wanapata magonjwa kutoka kwa wale wanaowauguza. Kwa hali hiyo, ninaiomba Serikali itoe mafunzo mengi kwa wale ambao wanawalea watu walio majumbani ili ugonjwa huu usiendelee kusambaa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga hoja ya Mheshimiwa Spika kwamba si kweli ukiongea sana ndiyo unalisaidia Bunge, tuweze kufupisha maneno yetu tunapozungumza. Naomba kumalizia hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu muda uliopo hauturuhusu yeyote tena kuchangia kwa muda ule tuliokubaliana, sasa naomba niahirishe Bunge kabla ya muda wake hadi tutakapokutana kesho tena saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.16 usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumatano*
*Tarehe 08 Februari, 2006 Saa Tatu Asubuhi)*